# UFUMBAJI KATIKA RIWAYA ZA KATAMA MKANGI

NA

ELIJAH ARASA AYIERA

TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA MAASAI MARA

CHUO KIKUU CHA MAASAI MARA

SEPTEMBA, 2017

**Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi yangu na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Sahihi________________________________ Tarehe______________________________

Elijah Arasa Ayiera

(AM01/6016/12)

**Idhini**

Tasnifu hii inawasilishwa katika Chuo Kikuu cha Maasai Mara kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu.

Sahihi________________________________________ Tarehe ______________________

Dkt. James Omari Ontieri

Idara ya Lugha, Isimu na Utamaduni

Chuo Kikuu Cha Maasai Mara

Sahihi________________________________________ Tarehe_________________________

Dkt. Nancy Ayodi

Idara ya Lugha, Isimu na Utamaduni

Chuo Kikuu Cha Maasai Mara

## HATILINZI

Elijah Arasa Ayiera © 2017

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa, kutafsiri au kuitoa tasnifu hii kwa jinsi yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

## TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa wazazi wangu. Natabarukia pia mtoto wangu Adeline  na mke wangu Betty kwa kunivumilia nilipokuwa masomoni.

# IKISIRI

Utafiti huu umechunguza ufumbaji katika riwaya mbili za Katama Mkangi: *Mafuta* na *Walenisi*. Utafiti huu umelenga: Kwanza, kubainisha aina mbalimbali za ubunifu wa ufumbaji uliojitokeza katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi*. Pili, kudhihirisha jinsi ufumbaji ulivyotumiwa na mwandishi kama kichocheo cha zinduko katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi*. Tatu, kudhihirisha namna ufumbaji umeendeleza au kukwamiza usawiri wa wahusika wa mtunzi. Nne, kutathimini jinsi mazingira ya mwandishi yalivyochangia matumizi ya mafumbo katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi*. Utafiti huu umebainisha kuwa, wakati ambapo Mkangi alikuwa akiandika riwaya hizi, uhuru wa kuikosoa serikali iliyokuwa mamlakani haukuwepo na kwa hivyo, alilazimika kutumia ufumbaji kuwasilisha ujumbe wake ili kuhepa rungu ya serikali. Pili, alikosomea na waandishi wengine, walimwathiri katika matumizi ya mbinu ya ufumbaji katika uandishi wake. Tatu, kutokana na kazi hii, ni dhahiri kuwa Mkangi alitumia mbinu ya ufumbaji kumzindua msomaji kuhusu athari za utabaka, ubepari, unafiki wa viongozi, sheria na nafasi yake katika jamii, umuhimu wa utu na usawa, umuhimu wa mapinduzi katika ujenzi wa jamii mpya, elimu na utafiti, mchango wa vijana katika ujenzi wa taifa miongoni mwa mengine. Aidha, imebainika kuwa Mkangi alitumia taswira, jazanda na istiari katika kufumba ujumbe wake. Hali kadhalika, imedhihirika kuwa ufumbaji ulimsaidia Mkangi katika usawiri wa wahusika wake kwa kuwapa majina ya majazi na lugha ya kimafumbo. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia Amali ambayo hupima umuhimu wa kitu kwa kuangalia matokeo ya matumizi ya hicho kitu. Nadharia hii hujishughulisha zaidi na matokeo na athari za hayo matokeo. Kwa hivyo, tumechunguza umuhimu wa ufumbaji kwa kuangalia matokeo na athari zake kwenye kazi za Mkangi. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani na kwenye mtandao. Kwa jumla mafumbo yamechunguzwa na kuwekwa katika makundi kutegemea namna yalivyojengwa. Ukusanyaji wa data ulifanywa kupitia kwa mbinu ya uchanganuzi wa matini au yaliyomo. Data iliyokusanywa na kuchanganuliwa imewasilishwa kwa njia ya maelezo. Utafiti huu ni muhimu kwa njia mbalimbali. Kwanza, utakuwa kama mwongozo kwa waandishi wa baadaye kuandika kazi nzuri zaidi kimafumbo. Pili, utawasaidia wasomi kuelewa kazi hizi zilizoandikwa kimafumbo. Tatu, utafiti huu unachangia pia katika kuangalia riwaya za Kiswahili kitaaluma hasa kwa misingi ya ufumbaji kwa kutumia Nadharia Amali.

## SHUKRANI

Waama kazi hii pevu imefika ukamilifu huu wake, na kwa jinsi hiyo, ningependa kutoa shukrani zangu kwa Maulana kwa kunipa afya, uwezo na ari ya kuendeleza masomo yangu.

Natoa shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu wawili, Dkt. James Omari Ontieri na Dkt. Nancy Ayodi kutokana na mwongozo wao wenye busara pamoja na ushauri wao ulioniwezesha kuikamilisha kazi hii. Wao ndio wameniauni katika kuichonga kazi hii na kuipa makali hata ikatokea ilivyo. Nawashukuru kwa ustahimilivu wao na moyo wao wa kujitolea bila kinyongo.

Tatu ningependa kuwashukuru wahadhiri wangu wote katika Idara ya Lugha, Isimu na Utamaduni kwa kuniongezea maarifa na kunitia moyo masomoni.

Natoa shukrani zangu kwa mwalimu Julius Matini na Zachary Onsarigo kwa ustahimilivu wao na kujitolea kwao kunisaidia nilipokuwa nikipiga chapa tasnifu hii.

Ningependa pia kuwashukuru wenzangu tuliosoma nao: Onsabwa, Lydia, Martha na Beatrice. Tuliweza kujadiliana na katika kisomo hiki kigumu, waliweza kunitia moyo pakubwa kwa kuifanya akili yangu daima iwe mbioni ikidadisi na kupekua malimwengu. Na Mungu awashehenezee baraka zake.

Ewe Bw. Motio John kumbuka kwamba msaada ulionipa wa kunitafutia riwaya ya *Mafuta* ulinifaa pakubwa. Urafiki wetu haujakuwa wa bure. Nawe Maroko Christopher, weka kwenye taamuli yako kwamba, uchangamfu wako uliniepusha na ukavu na uchovu wa dunia tangu urafiki wetu katika shule ya upili, chuo kikuu kwa shahada ya kwanza na tena shahada ya pili.

Mwisho, ningependa kuwashukuru marafiki zangu wote wale ambao nafasi haikuruhusu kuwataja hapa kwa kunitia shime nasema ahsanteni sana.

## YALIYOMO

Ungamo na Idhini ……..…………………………………………………………………..ii

Hatilinzi………………………………………………………………………………….iii

Tabaruku…………………………………………………………………………………...iv

Ikisiri ……………………………………………………………………………….....v

Shukrani…………………………………………………………………………………vi

Yaliyomo..………………………………………………………………………………vii

Vifupisho…………………………………………………………………………….....xi

Istilahi zilizotumika katika Utafiti huu……………………………………………………xii

**SURA YA KWANZA**……………………………………………………………………..1

**UTANGULIZI**……………………………………………………………………………1

1.0 Usuli wa Mada………... ……………………………………………………………1

1.1 Suala la Utafiti……………………………………………………………………..2

1.2 Malengo ya Utafiti ………………………………………………………………..2

1.3 Nadharia Tete.……………………………………………………………………..3

1.4 Upeo na Mipaka …………………………………………………………………..3

1.5 Sababu za Kuchagua Mada ……………………………………………………… 4

1.6 Umuhimu wa Utafiti ……………………………………………………………....4

1.7 Msingi wa Kinadharia ……………………………………………………………5

1.8.0 Mapitio ya Maandishi…………………………………………………………....7

1.8.1 Kuhusu Riwaya za Mkangi ………….…………………………………..........7

1.8.2 Mbinu za Uwasilishaji………………………………………………….........9

1.8.3 Taswira ……………………………………………………………...........9

1.8.4 Jazanda …………………………………………………………………...11

1.8.5 Istiari ……………………………………………………………………...12

1.8.6 Wahusika…………………………………………………………………….....13

1.9.0 Mbinu za Utafiti ………………….………………………………………….14

1.9.1 Eneo la Utafiti……………………………………………………………….14

1.9.2 Eneo Lengwa…………………………………………………………...….14

1.9.3 Uteuzi wa Sampuli…………………………………………..…………………15

1.9.4 Ukusanyaji wa Data………………………………………….…………..15

1.9.5 Uchanganuzi wa Data………………………………………………..………15

1.9.6 Uwasilishaji wa Data…………..……………………………………………15

1.9.7 Kiishilio………………………………..…………………………………..16

**SURA YA PILI**…………………………………………………………………...17

**MCHANGO WA MAZINGIRA YA MWANDISHI KATIKA MATUMIZI YA MAFUMBO**………………………………………………………………...17

2.0 Utangulizi……………………………………………………………………....17

2.1 Kuhusu Mwandishi wa Riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*……….………………………17

2.1.1 Kisomo………………………………………………………………………….17

2.1.2 Kazi…………………………………………………………………..………18

2.1.3 Uandishi Wake………………………………………………………………….19

2.1.4 Hali ya Kisiasa dhidi ya Waandishi Wakati wa Uandishi wake…..……………………19

2.1.5 Watu Waliomwathiri……………………………………………………...….20

2.2 Mchango wa Mazingira Katika Matumizi ya Mafumbo………………………………….21

2.3 Aina za Mafumbo ………………………………………………………………...23

2.4 Kiishilio…………………………………………………………………………...25

**SURA YA TATU**……………………………………………………………………….27

**MATUMIZI YA UFUMBAJI KAMA KICHOCHEO CHA ZINDUKO KATIKA RIWAYA YA**
***MAFUTA***…………………………………………………………………….…...27

3.0 Utangulizi……………………………………………………………………………27

3.1 Taswira………………………………………………………………………...…….27

3.1.1 Taswira ya Mhusika Matope…………………………………………………………28

3.1.2 Taswira ya Wateule na Wachochole…………………………………………………33

3.1.3 Taswira ya Mwenye Mkunazi………………………………………………………..40

3.1.4 Taswira ya Wanamapinduzi…………………………………………...…………..41

3.2 Jazanda……………………………………………………………......………..…42

3.2.1 Kitanda na Mafuta(Mikojo ya Paka)…………………………………………………43

3.2.2 Safari ya Ti……………………………………………………………………..……..46

3.2.3 Vidimbwi vya Maji na Matope…………………………………………...…….48

3.2.4 Uchi wa Matope……………………………………………………………...………49

3.2.5 Mkunazi……………………………………………………………………...…53

3.3 Sitiari…………………………………………………………..…………...….55

3.3.1 Mbuni……………………………………………………………………………...55

3.3.2 Njuzi…………………………………………………………………………………57

3.3.3 Ukame…………………………………………………………………………...…58

3.3.4 Nyoka Mkoko………………………………………………………………..…59

3.4 Namna Ufumbaji Umeendeleza au kukwamiza Usawiri wa Wahusika katika *Mafuta*…..61

3.5 Kiishilio……………………………………………………………………..….66

**SURA YA NNE**………………………………………………………………………68

**MATUMIZI YA MAFUMBO KAMA KICHOCHEO CHA ZINDUKO KATIKA RIWAYA YA *WALENISI***……………………...………………………………….........................68

4.0 Utangulizi……………………………………………………………………………68

4.1 Taswira…………………………………………...……………………...………..68

4.1.1 Mwanamke………………………………………………………………...…68

4.1.2 Vijana……………………………………………………………………………...…73

4.1.3 Mapenzoni……………………………………………………………………………77
4.1.4 Mapacha………………………………………………………..……………………80
4.1.5 Dzombo……………………………………………………………………………86
4.2 Jazanda……………..……………………………………………………………92
4.2.1 Majabali……………………………………………………………...………92
4.2.2 Trimi, Sayari na Kreshi……………………………………………………....95
4.2.3 Kidundu……………………………………………………………………………97
4.2.4 Safari ya Utu…………………………………………………………..………..99
4.2.5 Uchawi, Moto na Mabavu…………………………………………………………..103
4.3 Istiari……………………………...……………………………………..………106
4.3.1 Vijana Kulinganishwa na nzige na Makapi………………………………………...…106
4.3.2 Madaktari Kulinganishwa na Hirizi za Viunoni………………………………………108
4.3.3 Binadamu Kulinganishwa na Popo…………………………………………………....110
4.4 Namna Ufumbaji Umeendeleza au Kukwamiza Usawiri wa Wahusika Katika *Walenisi*………………………………………………………………………………...112
4.5 Kiishilio……………………………..…………………………………………………114

**SURA YA TANO**…………………………………………………………………..116
**MUHTASARI, MATOKEO, MAHITIMISHO MPENDEKEZO**………………..1I6
5.0 Muhtasari………………………………………………...………………...116
5.1 Matokeo…...………………………………………………………………………117
5.2 Mahitimisho……………………………………………………..…………………121
5.3 Mapendekezo…………………………………………………..………………..121
Marejeleo…………………………………………………………………………...122
Viambatisho………………………………………………………………………127

## VIFUPISHO

**TUKI**: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

**CEE**: Common Entrance Examination.

**KAPE**: Kenya Advanced Primary Examination.

**NARC**: National Rainbow Coalition.

.

## ISTILAHI ZILIZOTUMIKA KATIKA UTAFITI HUU NA VIFUPISHO

Katika utafiti huu, istilahi zifuatazo zimetumika kwa kuzingatia maana ifuatayo:

**Sanaa:** Ufundi wa hali ya juu wa kuwasilisha jambo kupitia kwa maandishi, mazungumzo, ufumbaji miongoni mwa njia nyingine.

**Uchanganuzi wa Yaliyomo**: Kuchambua mambo yaliyo katika maandishi au makala.

**Kushonwa mdomo**: Kuzuia kwa vyovyote mtu/ watu wasiweze kusema.

**Mbinu ya ustahilivu:** Hii ni mbinu ya utafiti ambayo huwa haitumii tarakimu sana. Mara nyingi utafiti wa aina hii hutumia maelezo tu.

**Trimi**: Chombo cha kusafiria ambacho huenda kwa kasi sana.

**Jehanamu:** Dunia alikotoka Dzombo imefananishwa na jehanamu kulingana na matendo mabaya ya huko.

**Kichocheo**: Ni jambo linalotia hamaki, hamu au shaka ya kuchukua hatua fulani.

**Kreshi**: Mahali panapofunziwa watoto.

**Mwakenya:** kundi la kisiri lililopinga serikali nchini Kenya kati ya mwaka wa 1980 na 1995. Pia, kulikuwepo na chapisho kwa jina hilo. Kundi hili lilipigwa marufuku na serikali ya KANU kwa kutuhumiwa kuwa na nia ya kupindua serikali.

**Zinduko:** Ni kutoa mtu katika kutoelewa, bumbuwazi au usahaulifu. Ni kumfanya mtu awe na habari kuhusu jambo fulani.

**Mafumbo**: Ni semi za kufikirisha, yaani vichemshabongo. Ni maelezo yanayouliza swali linalomhitaji msikilizaji kufikiri.

**Taswira:** Picha iundwayo na maneno au maelezo ili kuleta athari maalum katika mawazo ya msomaji au msikilishaji. Katika utafiti huu, taswira ni picha ya vitu au mahali katika akili ya msomaji.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Mada

Riwaya ina vijenzi viwili vikuu: maudhui na fani. Kazi ya fasihi hukamilishana kwa mambo haya mawili ya msingi ambayo hushirikiana na kukamilishana katika kuijenga fasihi na kuipa muonekano wake wa kifasihi. Fani ni ufundi wa kisanaa au ubingwa au mbinu ambazo msanii wa kazi ya fasihi hutumia katika kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Fani katika sanaa ni jumla ya vipengele vya lugha vilivyowekwa katika mpangilio mahususi ili kutoa kwetu maana fulani. Aidha, fani ni kipengele pekee ambacho humtofautisha msanii mmoja na mwingine. Ufundi huu wa fani hujitokeza katika mambo kadhaa kama vile: matumizi ya lugha, muundo, mtindo, wahusika na hata maudhui.

Lugha ndiyo mzizi wa kazi za fasihi. Ni malighafi muhimu ambayo msanii huitumia kwa ustadi mkubwa katika kuyaibusha mawazo yake kwa jamii. Msanii hutumia muda mwingi kuisuka na kuifuma lugha kiufundi na kuifanya lugha hiyo ionekane kuwa ya fasihi. Mwandishi hawezi kusema analotaka kulisema bila ya kuitumia lugha. Hii ni kweli hasa tukizingatia kwamba wazo au mawazo aliyonayo mwandishi huhusu jamii na wanajamii huweza kupata mawazo haya kupitia kwa lugha. Ikiwa mwandishi atataka kuwasiliana na msomaji wake vyema pamoja na hata kumshawishi na kumwathiri ipasavyo, lazima aiteue lugha yake vyema au ahakikishe kuwa lugha yake ina uwezo wa kuuwasilisha ujumbe huo.

Lugha ya fasihi huwa na sifa fulani kwa mfano, ina vikolezo au vitia ladha fulani. Imesheheni au kujaa mbinu za kila aina. Lugha ya kifasihi ni tofauti na lugha ya kawaida kwa kuwa lugha ya fasihi hujivimbisha au hujiashiria yenyewe. Lugha ya kifasihi husisitiza njia mahsusi za kuzungumzia jambo kuliko jambo lenyewe linalozungumziwa. Hivi ni kusema kwamba lugha ya kifasihi hujibainisha kwa kusisitiza miundo fulani ambayo huipa upekee.

Ufundi wa lugha anayotumia msanii hujidhihiisha katika vipengele vya msingi vitatu ambavyo ni tamathali za usemi, semi pamoja na mbinu nyingine za kisanaa. Mwandishi mzuri wa fasihi ni yule anayeweza kutumia msamiati, tamathali za usemi na miundo mingine ya lugha kumfanya msomaji awe na hisia fulani: hasira, furaha, huzuni na huruma kuhusu tabia na vitendo vya wahusika wake na matokeo ya maisha yao. Fasihi huandikwa na lugha ikitumia vipengele kama toni, mafumbo, maelezo na maongezi. Kwa hivyo, ni jukumu la mhakiki kutazama na kuchunguza lugha ya mwandishi kwa makini.

Mkangi amejitokeza kama mwandishi mmojawapo wa riwaya nchini Kenya. Kazi zake zinajitokeza kama kazi za kimafumbo. Lugha ya mafumbo ni ile ambayo huficha mawazo yake. Hapa mawazo hayawasilishwi waziwazi bali huandikwa kwa kufumbwa ili msomaji au msikilizaji aweze kutafakari kwa dhati. Ufumbaji huchangia upekee wa lugha ya kisanaa. Aidha, lugha ya mafumbo humsaidia mtunzi kuwasilisha ujumbe wake kwa njia fiche kwa wanajamii iwapo ukitolewa kiwazi huenda ukamtia matatani.

Katika utafiti huu, hali tukizingatia marejeleo maalum, tumelenga kuangalia kazi za Katama Mkangi kitaaluma kwa kujikita kwenye ufumbaji.

## 1.1 Suala la Utafiti

Lugha ya mafumbo ni mojawapo ya nyenzo wazitumiazo wasanii ili kufanya kazi zao ziwe hai zaidi. Kutokana na udurusu wa maandishi ya watafiti na wahakiki mbalimbali wa riwaya za Mkangi, ni dhahiri kwamba kazi za Mkangi zimewavutia wengi. Hata hivyo, kuna pengo linalohitaji utafiti zaidi. Imebainika kwamba mbinu ya ufumbaji haijashughulikiwa kama mada mahsusi ya utafiti katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*.

Aidha, ukweli kuwa mawasiliano hutokea iwapo msomaji ataelewa alichowasilisha mwandishi ni dhihirisho kuwa, kulikuwa na haja ya kufanya utafiti huu ili kubainisha namna mbinu ya ufumbaji ilivyotumiwa na Mkangi kuwasilisha ujumbe mzito kwa wasomaji wake kwa nia ya kuwazindua ili wafahamu hali zao halisi.

Swali ambalo tumelijibu hapa ni je, mafumbo aliyotumia Mkangi, yamemsaidia vipi kuwasilisha ujumbe wake unaolenga kuleta zinduko barabara?

## 1.2 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umelenga:

i. Kubainisha aina mbalimbali za ubunifu wa ufumbaji uliojitokeza katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi.*
ii. Kudhihirisha jinsi ufumbaji ulivyotumiwa na mwandishi kama kichocheo cha zinduko katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi.*
iii. Kudhihirisha namna ufumbaji umeendeleza au kukwamiza usawiri wa wahusika wa mtunzi.
iv. Kutathmini jinsi mazingira ya mwandishi yalivyochangia matumizi ya mafumbo katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi.*

## 1.3 Nadharia Tete

Nadharia tete zilizoongoza utafiti huu ni:

i. Mkangi ametumia mbinu mbalimbali za kisanaa katika ubunifu wa ufumbaji wa aina mbalimbali katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi*.
ii. Mkangi ametumia ufumbaji kama chombo cha kusafirisha mawazo yake akiwa na shabaha ya kuwazindua wasomaji wake.
iii. Kufaulu kwa mwandishi katika usawiri wa wahusika kunategemea uteuzi na ujenzi wa ufumbaji wake.
iv. Mazingira ya mwandishi yalichangia matumizi ya ufumbaji katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi.*

## 1.4 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Kuna waandishi kadhaa wa riwaya nchini Kenya ila tumemchagua Mkangi. Mkangi ni mwandishi mmojawapo aliyewahi kuwasilisha hali mbili, maswala ya kijamii na kitamaduni katika *Ukiwa* na maswala ya kisiasa katika *Mafuta* na *Walenisi*.

Mkono wake katika utunzi wa riwaya za Kiswahili umemzalishia kazi tatu: *Ukiwa*, *Mafuta* na *Walenisi*. Tumechagua kazi mbili *Mafuta* na *Walenisi* kwa sababu maalum. Katika *Mafuta* na *Walenisi* kuna kina cha ndani zaidi cha falsafa kuliko *Ukiwa* (Kisurulia, 2000). Tofauti hii ni kubwa kiasi kwamba kama jina la mwandishi lingetolewa kutoka vitabu hivyo na mtu ambaye hajawahi kuvisoma avisome, si vigumu kwake kusema hao ni waandishi wawili tofauti. Riwaya za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995) zinafanana kwa kuwa zinahusu zaidi maswala ya kisiasa na hasa suala la ugavi na umilikaji wa mali ya taifa. Riwaya zote mbili zinachunguza jinsi mfumo wa kisiasa unaodhibitiwa na tabaka la watu wachache unavyoweza kuathiri maisha ya waliotawaliwa kijamii, kiuchumi na hata kisaikolojia. Riwaya hizi zinaonyesha uovu uliopo katika tawala ambazo hazitilii maanani masilahi ya wengi ilhali *Ukiwa* inahusu maswala ya kijamii na utamaduni. Aidha, katika *Mafuta* na *Walenisi* ufundi mwingi wa kiumbuji umetumika kuliko *Ukiwa*.

Vipengele muhimu vya riwaya ni maudhui, wahusika na lugha (Forster, 1993, Mlacha 1985, Marshall, 1962). Tumeangazia kipengele cha lugha hasa tukijikita kwenye ufumbaji. Ufumbaji ni nyenzo watumiayo wasanii ili kuwasilisha ujumbe wao na hata kuwafanya wasomaji wa kazi zao kuzinduka na kutambua hali zao halisi. Ufumbaji hutumiwa

kuwasilisha ujumbe. Ingawa tumehusisha ufumbaji na ujumbe, haina maana kuwa tumeangalia ujumbe kwa kina kirefu. Ufumbaji ndio tumeushughulikiwa hasa kuona aina na namna ulivyojengwa na mwandishi kuwasilisha ujumbe ili kuwazindua wasomaji wake.

Aidha, utafiti huu umechunguza iwapo mazingira ya mwandishi ya kisiasa, kijamii na kiuchumi wakati alipokuwa akiandika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* yana uhusiano na uteuzi wa ufumbaji ili kujenga maudhui yenye lengo la zinduko.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Mada hii ilichaguliwa kutokana na kugundua kuwa lugha hutumiwa ili kufanikisha mawasiliano kati ya mwandishi na msomaji. Mawasiliano hutokea iwapo msomaji ataelewa alichowasilisha mwandishi. Ujumbe wa mwandishi sharti umfikie msomaji bila utata wowote. Katama Mkangi ni mwandishi mmojawapo aliyewasilisha kazi zake kwa njia ya mafumbo. Uchunguzi huu unabainisha jinsi Mkangi anavyotumia fani za lugha hususani ufumbaji akiwa na lengo la kuwazindua wasomaji wake.

Aidha, ufumbaji kama mbinu ya kubebe ujumbe mzito wa kuzindua haijachunguzwa kama mada mahsusi ya utafiti katika riwaya za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Wengi walioshughulikia riwaya hizi wameegemea upande wa maudhui mathalani (Vunyoli, 2004), mtiririko wa hadithi (Wamitila, 1998), wahusika (Kisurulia, 2000) na taswira (Musembi, 2008). Kuchunguza ufumbaji katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* kutarahisisha ufahamu wa maudhui mazito ambayo Mkangi alidhamiria kuyapitisha kwa jamii yake.

Sababu nyingine iliyochangia uchunguzi wa mada hii ni ugunduzi kuwa, riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* ni kazi muhimu za kisanaa. Katama Mkangi ameshughulikia maswala nyeti na mazito yanayozikumba nchi nyingi za bara la Afrika, ikiwemo Kenya. Baadhi ya maswala aliyozungumzia ni kama vile udhalimu na ukatili, matumizi mabaya ya mamlaka, uasi wa dini katika jamii, nafasi ya mwanamke, ujenzi wa jamii mpya, sheria na nafasi yake katika jamii.

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umechangia katika kuweka msingi wa kuchanganua riwaya ya Kiswahili kitaaluma kwa kujikita kwenye kipengele cha lugha hasa kwa kuangazia zaidi ufumbaji wa habari. Kwenye utafiti huu tumechunguza ufumbaji: aina, ubunifu wake na uamilifu wake katika kuwasilisha ujumbe mbalimbali wa mwandishi kwa lengo la kuzindua. Hivyo basi,

kazi hii itakuwa kama mwongozo kwa waandishi wa baadaye wa riwaya ya Kiswahili kuandika kazi nzuri zaidi kimafumbo.

Lengo la uhakiki ni kudhihirisha kusudi la mtunzi kwa kuondoa vikwazo vyovyote ambavyo vyaweza kutatiza uelewaji. Kwa jumla utafiti huu ni muhimu kwa wasomaji wa riwaya. Unawawezesha kuelewa kwa nini msanii akabuni mafumbo na kuyatumia. Wasomaji wanaweza pia kufahamu ufundi unaotumiwa katika kufinyanga mafumbo ili kutekeleza jukumu la kuwasilisha ujumbe kwa nia ya kuzindua wasomaji wake. Aidha, kwa sababu tumeangalia ufumbaji kitaaluma kwa kutumia misingi ya kinadharia, utafiti huu utampa msomaji mshawasha wa kusoma upya kazi hizi za Mkangi zilizoandikwa kimafumbo. Hili hufanya kazi inayosomwa kueleweka zaidi.

Umuhimu wa kutumia mbinu ya ufumbaji katika kazi ya fasihi ni kusawiri mawazo ya mtunzi kwa kina kirefu zaidi kwa sababu matumizi ya ufumbaji humpa msomaji au mtazamaji viwango vingi vya ufasiri na ufahamu. Matumizi ya ufumbaji hulenga kufikia maana mpya, pana na ya kipekee kwa kutumia mbinu ya uhamisho. Hivyo, utafiti wetu umebaini kuwa Mkangi amefikia malengo haya.

Tumesema katika sehemu ya usuli kuwa, kazi za kiuchambuzi na uhakiki zilizowahi kutokea kuhusu riwaya hizi mbili za *Mafuta* na *Walenisi* hazijashughulikia ufumbaji kama mada mahsusi. Tahakiki za kitaaluma zilizowahi kutokea zimehusu hasa maudhui (Vunyoli, 2004), wahusika (Kisurulia, 2000), mtiririko wa hadithi (Wamitila, 1998) na taswira (Musembi, 2008). Utafiti huu wetu pia umeweka misingi ya kuhakiki riwaya za Kiswahili kitaaluma hasa tukizingatia ufumbaji.

Utafiti katika uwanja wa fasihi ni njia mojawapo muhimu ya kuikuza na kuhifadhi lugha. Hii hutokana na msamiati thabiti wa kiuchambuzi unaotokana na nadharia mbalimbali za fasihi. Aidha, dafina ya maandishi ya Kiswahili inakuwa kubwa mbali na kuipa hii lugha msamiati mgeni au kuimarisha istilahi zilizopo za kifasihi na za kiuchambuzi.

## 1.7 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu umejengeka kwenye misingi ya Nadharia Amali. Nadharia hii huhusu kile ambacho sanaa yaweza kufanya kwa hadhira na athari za sanaa kwa hadhira. Kwa muhtasari, misingi ya Nadharia Amali ni: matokeo au athari, kazi au wajibu na muktadha wa matumizi.

Holman (1936:411), anadai kuwa dhana ya uamali ilitumiwa mnamo 1878 ili kuelezea mkabala wa kifalsafa unaotambua umuhimu na maana kupitia kwa kutazama na kujaribu matokeo au umuhimu wa kimatumizi. Waama, Nadharia Amali huzingatia hasa matokeo au mwisho wa kitu fulani ili kutathmini umuhimu wa kitu hicho. Hii ina maana kuwa ili kupima ufumbaji wa kazi fulani ya sanaa sharti kuona kama unafaulu au kushindwa kutekeleza wajibu uliopewa. Kwa kusisitiza nafasi hii kuu ya matokeo au utekelezaji, Holman (1936), anasema kuwa mwananadharia Amali husisitiza kuwa maswali yoyote hayana umuhimu wowote isipokuwa tu kama matokeo ya kuyajibu kwa njia moja au nyingine yana athari zinazoonekana katika masuala ya kijamii. Kwa msingi huu tunaona umuhimu wa ufumbaji tu iwapo utaweza kuathiri sanaa fulani kwa njia maalum na hivyo kusababisha matokeo fulani.

Kulingana na Holman (1936:411), Nadharia Amali imeendelezwa na William James na John Dewey. James (1879), aliona kuwa maana nzima ya wazo huonekana katika matokeo halisi, matokeo ambayo hujitokeza ama kama tabia nzuri za kufuatwa au tajriba inayotarajiwa iwapo hilo wazo ni sahihi. Wananadharia amali basi hujishughulisha na vitu katika ukamilifu wake, hupendelea kuzingatia muktadha, hawajihusishi na udhahania bali na matokeo halisi tu.

Naye Abrams (1983:39), anasema kuwa uhakiki wa kiamali hutimiza kazi kama kitu kilichoundwa ili kuwa na athari fulani kwa hadhira (athari kama vile kuburudisha, kufunza au kuibua mihemko) na huelekea kupima umuhimu wa kazi kulingana na kufaulu katika kufikia lengo hili. Hivyo basi, nadharia hii imetufaa kwa sababu utafiti wetu ulilenga kuchunguza jinsi ufumbaji hutumiwa na mwandishi kuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji kwa lengo la kuwazindua na kuona hali zao halisi za maisha.

Katika kufikia malengo tofauti tofauti ya mwandishi, mafumbo hutofautiana. Hii imetusaidia kuainisha ufumbaji katika makundi tofauti kulingana na zile mbinu za lugha zilizotumika kuziunda. Aidha, ufumbaji katika ubunifu wa majina ya wahusika waweza kuwa ishara au kiashiria cha maana fulani. Nadharia Amali imetusaidia kuchunguza jinsi ufumbaji umeendeleza au kukwamiza usawiri wa wahusika wa mtunzi katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*.

Imeelezwa kuwa Nadharia Amali pia hujihusisha sana na muktadha ( Levinson, 1983:9). Ni kweli kazi yoyote ya sanaa hutungwa katika muktadha fulani. Uelewaji wa muktadha huu ni muhimu sana katika kuelewa maana alizokusudia mwandishi katika ukamilifu wake. Ni huu muktadha unaotuwezesha kutambua kwa nini mafumbo fulani yaliteuliwa, yakajengwa na kutumiwa na mwandishi kama yalivyotumiwa. Aidha, muktadha umetusaidia kutathmini jinsi

mazingira ya mwandishi yalivyochangia matumizi ya ufumbaji. Miktadha hii hutofautiana: ya kijamii, ya kisiasa, ya kielimu na ya kidini.

Kisurulia (2000), ametumia Nadharia Amali katika kusawiri wahusika katika kazi za Mkangi. Ameainisha wahusika katika makundi mbalimbali kulingana na wajibu wao katika kazi ya sanaa. Aidha, ameangalia ujenzi na ukuzaji wa wahusika katika kutekeleza wajibu wa kusababisha athari fulani kwa hadhira. Utafiti huu umetusaidia ili kuchunguza uteuzi na ujenzi wa ufumbaji katika uwasilishaji wa ujumbe kwa nia ya kuzindua wasomaji wake. Wafula (1994: 69-73), naye ametumia Nadharia Amali katika kuainisha kundi moja la methali za Kiswahili. Anasema kuwa baadhi ya methali zaweza kufahamika barabara kupitia kwa ujuzi wa kimuktadha. Kazi yake Wafula (mtaje), ni muhimu katika Nadharia Amali tuliyotumia katika utafiti wetu. Imetusaidia kuelewa ujumbe uliowasilishwa kimafumbo kupitia kwa kutumia ujuzi wa kimuktadha.

### 1.8.0 Mapitio ya Maandishi

Sura hii imeshughulikia yaliyoandikwa kuhusiana na mada. Maandishi yamepitiwa katika mada zifuatazo: kuhusu riwaya za Mkangi, mbinu za uwasilishaji, taswira, jazanda, istiari na wahusika. Sura hii pia imeonyesha mwanya uliopo katika maandishi, ambao ulichochea utafiti huu.

### 1.8.1 Kuhusu Riwaya za Mkangi

Wamitila (1998:83) ameonyesha jinsi kazi ya Mkangi *Walenisi* (1995) ilivyojikita katika mtiririko wa hadithi. Mhakiki huyu kamwe hakujishughulisha na ufafanuzi wa matumizi ya ufumbaji katika riwaya hii. Utafiti huu wetu umechunguza mbinu ya ufumbaji aliyotumia Mkangi akiwa na lengo la kuzindua wasomaji wake kupitia riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Kazi ya Wamitila ni tofauti na utafiti huu. Yeye ameshughulikia riwaya ya *Walenisi* pekee kwa upande wa mtiririko wa hadithi ilhali utafiti wetu umechunguza matumizi ya ufumbaji katika riwaya mbili za *Mafuta* na *Walenisi.* Utafiti wake Wamitila (mtaje), umekuwa wa manufaa kwetu sana kwa sababu, umetuwekea msingi wa kuchunguza na kuelewa riwaya ya Walenisi iliyoandikwa kimafumbo.

Vunyoli (2004), amehakiki riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* akizingatia hadithi kama chombo cha maudhui. Utafiti huu wa Vunyoli (mtaje), umechanganua hadithi tofauti katika riwaya hizi na kubainisha maudhui ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yaliyojitokeza katika hadithi hizo. Utafiti wake pia umeonyesha jinsi hadithi za jadi zilivyotumiwa na Mkangi kama nyenzo ya

kutoa maudhui ya kisiasa. Utafiti wa Vunyoli (mtaje), ni tofauti na huu kwa njia kadhaa. Kwanza, utafiti wetu umechunguza matumizi ya lugha, mathalani ufumbaji kama nyenzo ya kuwasilisha ujumbe wa kuzindua katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi.* Utafiti wa Vunyoli (mtaje), haujajishughulisha na matumizi ya lugha kama ilivyo katika utafiti wetu. Yeye ameegemea upande wa hadithi. Pili, utafiti wetu umeongozwa na Nadharia Amali ilhali yeye ametumia nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa. Hata hivyo, utafiti wa Vunyoli (mtaje), umetufaa sana kwa upande wa maudhui ambayo kwayo Mkangi alilenga kuwazindua wasomaji wake kupitia kwa mbinu ya ufumbaji.

Kisurulia (2000), amechunguza usawiri wa wahusika katika kazi mbili za Mkangi: *Ukiwa* na *Mafuta*. Alizingatia hasa uchaguzi, uumbaji na makuzi ya wahusika na mwandishi. Kusudi kuu lilikuwa ni kutambua jinsi mwandishi alivyowatumia wahusika ili kufanikisha malengo ya kazi yake. Aligundua kwamba uchaguzi, uumbaji na makuzi ya wahusika yanaathiri ujumbe wa mwandishi kwa kiwango kikubwa. Aidha, ameonyesha kuwa uchaguzi mbaya wa wahusika na kuwakuza kwa njia mbaya kunadhoofisha kazi na hasa ujumbe wa mwandishi. Utafiti wake Kisurulia (mtaje), ni tofauti na wetu kwa njia mbili. Kwanza, yeye alichunguza usawiri wa wahusika ilhali sisi katika utafiti wetu tumeshughulikia ufumbaji. Pili, yeye ameshughulikia riwaya za *Mafuta* na *Ukiwa* na kwa upande wetu tumeshughulikia *Mafuta* na *Walenisi*. Hata hivyo, utafiti wake umetufaa sana katika utafiti wetu kwa njia mbili. Kwanza, Kisurulia (mtaje), katika utafiti wake ameongozwa na Nadharia Amali ambayo hupima umuhimu wa kitu kwa kuangalia matokeo ya matumizi ya hicho kitu na utafiti wetu umeongozwa na nadharia hii pia. Pili, utafiti wake umetusaidia katika kufikia lengo letu la kuchunguza jinsi ufumbaji huendeleza au kukwamiza usawiri wa wahusika wa mtunzi.

Musembi (2008), amehakiki matumizi ya taswira na ukinzano katika riwaya za Mkangi: *Mafuta* na *Walenisi.* Katika kazi hiyo amefafanua jinsi Mkangi alivyotumia taswira za kuonekana na za hisi ili kubainisha maudhui ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yaliyojitokeza katika taswira hizo. Musembi (mtaje), alilenga kubainisha aina za taswira zinazojitokeza katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Aidha, alitaka kuonyesha jinsi taswira alizotumia mwandishi zilivyomsaidia kuwasilisha maudhui mbalimbali ili kuonyesha wasomaji wake hali halisi ya maisha yao na wakati huo huo kuwatolea suluhu la kurekebisha hali hizo. Musembi (mtaje), katika utafiti wake aliongozwa na Nadharia ya Uyakinifu wa Kijamaa na Nadharia ya Kimtindo. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu yeye amehakiki taswira na ukinzano ilhali sisi tumehakiki ufumbaji. Aidha, yeye alitumia Nadharia ya Uyakinifu wa Kijamaa na Nadharia ya Kimtindo katika utafiti wake huku sisi tumetumia Nadharia Amali.

Utafiti huu umefanana na wetu kwa sababu tumehakiki pia riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Kwa upande mwingine Musembi (mtaje), amehakiki matumizi ya lugha akiegemea kipengele cha taswira na ukinzano. Utafiti wetu pia umehakiki matumizi ya lugha, tukiegemea kipengele cha ufumbaji.

### 1.8.2 Mbinu za uwasilishaji

Ngara (1982, 1985) anaonyesha kwamba, lugha ndicho kigezo muhimu cha kupimia ufanisi wa kazi ya fasihi. Kazi ya sanaa huwa na sehemu kama ploti, dhamira, maudhui na wahusika lakini bila lugha vipengele hivyo haviwezi kuwasilishwa vilivyo kwa sababu, sehemu hizi hupewa umbo kupitia kwa lugha. Maelezo yake Ngara (mtaje), ni muhimu katika utafiti wetu kwa kuwa, yameweka msingi wa kuchunguza ufumbaji kama kipengele cha lugha katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*.

Wafula (1990) anachambua mawazo na mbinu za uwasilishaji alizotumia Chacha katika tamthilia ya *Marejeo*. Anaonyesha jinsi ukoloni mamboleo unavyodunisha utumishi wa bara la Afrika kwa Ulaya. Anasawiri uhusiano wa Mwafrika; uhusiano unaomweka Mwafrika katika hali ya uhitaji kila kunapokucha. Anaonyesha kuwa Mwafrika amejitakia msiba huu kwa hiari yake mwenyewe. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwa njia mbili: Wafula (mtaje), ameegemea katika swala la maudhui nasi tumeegemea katika swala la ufumbaji. Kwa upande mwingine, Wafula (mtaje), ameshughulikia tamthilia ilhali sisi tumeshughulikia riwaya. Utafiti wake Wafula (mtaje), unafanana na wetu kwa sababu hata sisi tumeshughulikia mbinu za uwasilishaji huku tukijikita katika mbinu ya ufumbaji.

Miriji (1991) na Mwangi (2005), wamechunguza vipengele vya mtindo na fani katika tamthilia za Kiswahili. Hawa wawili wamejadili tu kwa jumla kuhusu mtindo na fani. Utafiti wao ni tofauti na wetu kwa sababu sisi tumejikita katika kipengele mahsusi cha kimtindo ambacho ni ufumbaji na ambacho tumekijadili kwa kina. Hata hivyo, utafiti wao umetufaa katika kutuwekea msingi wa kuanza utafiti wetu.

### 1.8.3 Taswira

Momanyi (1991), amehakiki matumizi ya taswira kama kielelezo cha uhalisia katika *utenzi wa Al-inkishafi*. Katika kazi hiyo, amefafanua taswira zinazojengeka ndani ya tamathali za usemi katika kuonyesha kuanguka kwa mji wa Pate. Utafiti wake umeongozwa na nadharia ya Uhalisia. Utafiti huu wa Momanyi (mtaje), ni tofauti na wetu kwa njia hizi: utafiti wake umeongozwa na Nadharia ya Uhalisia, tofauti na huu ambao umeongozwa na Nadharia

Amali. Pili, Momanyi (mtaje), amejikita katika kuonyesha jinsi uhalisia wa kuanguka kwa mji wa Pate unavyojitokeza katika matumizi ya taswira. Utafiti huu ni tofauti na wake, kwani umechunguza matumizi ya ufumbaji ili kuwasilisha ujumbe wenye lengo la kuzindua wasomaji. Tatu, utafiti wa Momanyi (1991), umeshughulikia utanzu wa ushairi ilhali utafiti huu umeshughulikia utanzu wa riwaya. Hata hivyo, utafiti wa Momanyi (mtaje), umechangia utafiti huu kwa kuchunguza ufumbaji kupitia kwa taswira.

Nyanchama (2004), amehakiki matumizi ya taswira na ishara katika *Sauti ya Dhiki* diwani ya Abdilatif Abdalla. Katika uhakiki wake, ameshughulikia matumizi ya taswira na ishara ili kubainisha jinsi Abdalla anavyozitumia mbinu hizi katika kuwasilisha maudhui yanayohusu dhuluma dhidi ya wanyonge na uozo katika serikali iliyokuwepo akiandika. Utafiti wa Nyanchama (mtaje), ni tofauti na huu. Yeye amehakiki matumizi ya taswira za kuonekana na za hisi ilhali sisi tumehakiki taswira kama nyenzo ya ufumbaji. Aidha, utafiti wa Nyanchama (mtaje), umeongozwa na Nadharia ya Semiotiki na Nadharia ya Uhakiki wa Kitamaduni ilhali utafiti huu umeongozwa na Nadharia Amali. Hata hivyo, utafiti wake Nyanchama (mtaje) unafanana na huu kwa sababu tafiti hizi zote zinahakiki matumizi ya lugha.

Karanja (1990), amehakiki tamthilia za kikombozi ambapo ameangazia taswira ya Mwafrika katika vita vya ukombozi dhidi ya ukoloni. Amehakiki tamthilia tatu ambazo ni *Mukwawa wa Uhehe* (1979), *Kinjekitile* (1969) na *Mzalendo Kimathi* (1974). Lengo lake kuu lilikuwa kubaini taswira yakinifu ya Mwafrika katika vita dhidi ya ukombozi. Utafiti wa Karanja (mtaje), ni tofauti na huu kwa sababu yeye alishughulikia tamthilia na sisi tumeshughulikia riwaya. Aidha, yeye amehakiki taswira tu ilhali utafiti huu umehakiki taswira kama aina moja ya ufumbaji. Utafiti wake Karanja (1990), umetufaa kwa kuweka msingi wa kuchunguza matumizi ya lugha hasa ufumbaji ili kufikia lengo letu la kubainisha aina na ubunifu wa ufumbaji.

Wamitila (2004), akizungumzia lugha ya fasihi, anasema kuwa taswira ni picha inayomjia msomaji akilini anaposoma kazi ya sanaa kwa kufananisha hali halisi ya maisha. Anahitimisha kwa kusema kuwa taswira huchangia katika ufumbaji wa habari. Mawazo haya ya Wamitila (mtaje), ni muhimu kwa utafiti wetu kwa sababu ndiyo yamekuwa kitovu cha utafiti wetu ili kubainisha aina na ubunifu wa ufumbaji katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Utafiti wetu utakuwa tofauti kwa njia mbili. Wamitila (mtaje), alishughulikia uhakiki wa fasihi kwa jumla kwa kufafanua vigezo vya kuzingatia wakati wa kuhakiki kazi ya fasihi ilhali utafiti wetu umejikita kwenye riwaya hasa za Mkangi. Kazi hii, imehakikiwa kwa

misingi ya Nadharia Amali, kwa upande wake, hakutumia nadharia yoyote bali alitoa maelezo ya kinadharia tu.

### 1.8.4 Jazanda

Wafula (1989), ameshughulikia vipengele vya jazanda katika tamthilia. Wafula (mtaje), anasema kwamba, sifa muhimu katika tamthilia ni matumizi ya kunga zinazofungamana na mazingira ya kiafrika. Anaendelea kusema kwamba, tamthilia zinazotumia tamathali kama jazanda huwa tata sana katika kufahamika kwa vile zinamzamisha msomaji katika vina mbalimbali vya ufahamu wa uhalisia unaomzingira. Anasema kwamba tamthilia za *Wingu Jeusi* (1987), *Lina Ubani* (1984), *Kivuli Kinaishi* (1990) *na Mashetani* (1971) zimejengwa kijazanda. Utafiti huu umetofautiana na wetu kwa njia hizi: kwanza, Wafula (mtaje), alishughulikia tamthilia ilhali sisi tumeshughulikia riwaya. Pili, yeye amejadili aina mbalimbali za jazanda ilhali sisi tumejadili jazanda kama aina mojawapo ya ufumbaji. Hata hivyo, utafiti huu umetufaa katika kutuwekea msingi utafiti wetu ili kubainisha aina na ubunifu wa ufumbaji katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*.

Malenya (2008), ameangazia jazanda katika nyimbo za Jacob Luseno. Malenya (mtaje), ameonyesha jinsi huyu mtunzi amefanikiwa kutumia jazanda katika nyimbo zake. Mtafiti huyu aliongozwa na Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa. Utafiti wake umetusaidia kuchunguza aina mbalimbali za ufumbaji. Hata hivyo, utafiti huu umetofautiana na wetu kwa kuwa sisi tumechunguza ufumbaji tukiongozwa na Nadharia Amali ilhali yeye ameongozwa na Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa. Aidha, tumehakiki riwaya za Mkangi ilhali mtafiti amehakiki nyimbo za Luseno.

Okwena (2013), ameshughulikia matumizi ya jazanda katika riwaya tatu za Timothy Arege. Amechanganua na kubainisha aina mbalimbali za jazanda ambazo Arege ametumia. Anasema kuwa upo uhusiano baina ya lugha ya kijazanda anayotumia mtunzi na ujumbe anaowasilisha kwenye tamthilia. Okwena (mtaje), katika utafiti wake aliongozwa na Nadharia ya Kimtindo. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu yeye amehakiki kipengele kimoja cha ufumbaji (jazanda) ilhali sisi tumehakiki ufumbaji kwa jumla. Kwa upande mwingine, utafiti wetu ni tofauti kwa sababu tumeongozwa na Nadharia Amali ilhali Okwena (mtaje) ameongozwa na nadharia ya Kimtindo. Hata hivyo, utafiti huu umetufaa sana katika kubainisha aina za ufumbaji na kuonyesha jinsi Mkangi alivyotumia ufumbaji kama kichocheo cha zinduko la jamii.

Akishughulikia uhakiki wa kazi za fasihi, Mwenda (2004), anaelezea kuwa jazanda ni mafumbo ambamo maana ya kitu imefichika. Wakati mwingine mwandishi huwa anawapatia wasomaji wake kazi ya kutafuta na kung'amua maana ya kitendo au hali fulani au kisa kwa kutumia fumbo au kwa kutumia jambo ambalo laeleweka kuwa la kawaida lakini kumbe pana ujumbe uliofichika. Msanii anaweza kuwa ametumia maneno na visa ambavyo kwa msingi ni vya kawaida kumbe vile visa vyatoa ujumbe mwingine ambao umefumbwa kama jazanda. Maelezo ya Mwenda (mtaje), yamekuwa ya manufaa kwetu kwa namna mbili. Kwanza, kusema kuwa jazanda hutumia maneno na visa ambavyo kwa msingi ni vya kawaida ni kujaribu kuonyesha kuwa jazanda huchora picha ya kawaida na hivyo basi jazanda hujenga taswira. Pili, Mwenda (mtaje), kushikilia kuwa jazanda ni mafumbo ambamo maana ya kitu imefichika ni kuonyesha kuwa taswira ambazo hujengwa kupitia kwa jazanda huwasilisha ujumbe uliofichika au uliofumbwa. Mawazo haya mawili ndiyo yanayojenga kitovu cha utafiti wetu.

### 1.8.5 Istiari

Istiari ni matumizi ya ishara ambazo maana yake hujitokeza katika masimulizi mengine (Msokile, 1993). Anachokimaanisha mtaalamu huyu ni kuwa, msanii hutumia kitu au dhana fulani ili kumaanisha kitu au dhana tofauti. Tukidhukuru mawazo haya ya Msokile (mtaje), kwa undani, tunapata kuwa istiari huchora picha yenye maana tofauti na picha yenyewe. Maelezo haya ni muhimu kwetu kwa sababu yametusaidia kuchunguza ufumbaji wa habari.

Wamitila (2004:154), anashikilia kuwa, istiari ni mbinu ya fasihi ambapo mwandishi hulinganisha vitu, wahusika au hali kwa njia ya moja kwa moja, pasi kutumia maneno ya ulinganisho. Anaendelea kusema kuwa istiari ni msingi wa mafumbo au kufichwa kwa maana ambayo msikilizaji au anayetegewa anapaswa kutegua. Maelezo haya yanahusiana na utafiti huu na yametusaidia kuchunguza ufumbaji katika riwaya za Mkangi.

Wangari (2011), akishughulikia mbinu mbalimbali za mawasiliano katika runinga nchini Kenya, ameangazia mbinu kadhaa ikiwemo istiari. Amechunguza mbinu za mawasiliano zitumikazo nchini Kenya hususani ya biashara. Anaelekea kusema kuwa istiari ni namna ya kiubunifu ya kurejelea kitu kingine kilicho na sifa zinazofanana na zile za kile kinachoelezwa. Anaendelea kusema kuwa, ujumbe hutolewa kwa njia iliyofichika. Utafiti wake uliongozwa na Nadharia ya Semiotiki. Ugunduzi wa Wangari (mtaje), kuwa istiari huwasilisha ujumbe kwa njia ambayo ni fiche, umetufaa sana katika utafiti wetu. Umetusaidia kuchunguza istiari kama njia mojawapo ya ufumbaji wa habari. Hata hivyo,

utafiti wake ni tofauti kwa sababu yeye alishughulikia mbinu za mawasiliano ya runinga ilhali sisi tumeshughulikia ufumbaji katika riwaya za Mkangi. Aidha, yeye aliongozwa na Nadharia ya Semiotiki ilhali sisi tumeongozwa na Nadharia Amali.

### 1.8.6 Wahusika

Mule (1991), alijishughulisha na swala la mwanamke katika tamthilia za Kiswahili kwa kutumia Nadharia ya Mtazamo – kike. Mule amezihakiki tamthilia ambazo zimeandikwa na mwanamke kama Mwachofi (1987)- *Mama ee*, Kyanga (1975) – *Zinduko*, Muhando (1972) – Hatia, *Pambo*, *Nguzo Mama* na *Lina Ubani*, Angelina (1984) – *Kortini Mtu Huyu*. Katika kazi hizi, Mule (mtaje), anajaribu kuzichambua taswira za mwanamke kama zinavyojitokeza katika kila kazi. Kupitia kwa taswira hizi alijaribu kuhakiki mitazamo na misimamo ya waandishi aliowachagua kuhusu swala la mwanamke na ukombozi wake. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwa njia kadhaa. Kwanza, Mule (mtaje), alitumia Nadharia ya Mtazamo – kike ilhali sisi tumetumia Nadharia Amali. Pili, Mule (mtaje), ameshughulikia tamthilia za Kiswahili lakini sisi tumeshughulikia riwaya. Aidha, Mule (mtaje), amejikita katika swala la mwanamke yaani wahusika ilhali sisi tumejikita katika ufumbaji. Utafiti wake umetusaidia kwa kutuwekea msingi wa kuangalia dhana ya uhusika.

Syambo na Mazrui (1992), Mohamed (1992) na Wamitila (2002, 2003), wanaeleza namna wahusika wa tamthilia hudhihirishwa na watunzi. Wanaeleza kuwa ni vigumu kwa msanii wa tamthilia kutoa maelezo mengi kuhusu wasifu, tabia na saikolojia za wahusika wake. Kwa hivyo mtunzi hulazimika kutumia baadhi ya kaida zinazokubalika katika usanii wa tamthilia kama vile uzungumzi nafsia na mbinu ya majazi miongoni mwa nyinginezo. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu wanaelezea namna wahusika wa tamthilia hudhihirishwa na watunzi ilhali sisi tumehakiki ufumbaji. Aidha, wao walishughulikia tamthilia ilhali katika utafiti wetu tumeshughulikia riwaya. Lakini utafiti wao ulitufaa kwa kuchunguza namna ufumbaji huendeleza au kukwamiza usawiri wa wahusika.

Dhahabu (1994), amechunguza uumbaji na uendelezaji wa wahusika katika tamthilia kuu za Penina Muhando. Tamthilia ambazo mtafiti huyu alichunguza ni: *Tambueni Haki zetu* (1972), *Talaka si Mke Wangu* (1976), *Nguzo Mama* (1982) na *Lina Ubani* (1984). Mhakiki anataka kuonyesha namna ambavyo hali za wahusika zimeathiri uwasilishaji wa masuala makuu yaliyojadiliwa. Utafiti wa Dhahabu (mtaje), unatofautiana na wetu kwa njia mbili. Kwanza, utafiti wake umejikita kwa wahusika ilhali wetu umejikita kwa ufumbaji. Pili, Dhahabu (mtaje), alihakiki tamthilia lakini sisi tumehakiki riwaya. Kwa upande mwingine utafiti wake

unafanana na wetu kwa kuwa, pia sisi tumechunguza uumbaji na uendelezaji wa wahusika kupitia kwa mafumbo.

Kisurulia (2000), alishughulikia usawiri wa wahusika katika riwaya za Katama Mkangi: *Ukiwa* na *Mafuta*. Mhakiki alionyesha namna uchaguzi, uumbaji na makuzi ya wahusika yanaathiri moja kwa moja ujumbe wa mwandishi. Utafiti wa Kisurulia unafanana na wetu kwa njia mbili. Katika kazi yake alitumia Nadharia Amali ambayo tumetumia pia katika utafiti wetu. Pili, ameshughulikia riwaya mbili za Mkangi ambapo tumeshughulikia mojawapo katika utafiti wetu. Kwa upande mwingine utafiti wake unatofautiana na wetu kwa kuwa yeye amejikita kwa usawiri wa wahusika ilhali sisi tumejikita kwa ufumbaji.

Kati ya maandishi na kazi nyingi tulizozipitia hamna inayoshughulikia ufumbaji kama mada ya utafiti. Aidha, hakuna utafiti uliofanywa kuhusu ufumbaji katika riwaya hizi mbili za Mkangi: *Mafuta* na *Walenisi*. Ugunduzi huu ndio uliotupa ghera na hamasa kuangalia ufumbaji katika riwaya hizi za Mkangi.

### 1.9.0 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii imeshughulikia eneo la utafiti, eneo lengwa, sampuli na uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uwasilishaji wa data na uchanganuzi wa data.

### 1.9.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyiwa katika maktaba za vyuo vikuu mbalimbali. Maandishi mbalimbali yamepitiwa maktabani yakiwa ni pamoja na vitabu vya fasihi vilivyouteliwa kwa minajili ya mada hii. Majarida, makala, vitabu vya kinadharia na vitabu vinavyozungumzia ufumbaji pia vimesomwa. Utafiti umefanywa pia kwenye mtandao ili kupata data inayofaa. Tafiti za awali zimesomwa ili kuelewa nadharia, mbinu za kukusanya data, uwasilishaji na uchambuzi wa matokeo ya utafiti.

### 1.9.2 Eneo Lengwa

Ingawa Mkangi ameandika riwaya tatu *Mafuta, Ukiwa* na *Walenisi,* riwaya mbili pekee yaani,*Walenisi* na *Mafuta* ndizo zimeshughulikiwa katika utafiti huu. Riwaya hizi zilichaguliwa kimakusudi kutokana na sababu zilizotolewa katika sehemu ya upeo na mipaka ya utafiti (sehemu 1.4).

Kilichochunguzwa katika utafiti huu ni ufumbaji. Mafumbo yameteuliwa kwa njia ya uchunguzi wa maandishi. Riwaya hizi zimesomwa kwa kina huku tukizingatia zaidi ufumbaji ili kuonyesha uhusiano uliopo kati ya ufumbaji na ujumbe katika kazi ya sanaa.

### 1.9.3 Uteuzi wa Sampuli

Vitabu vilivyolengwa ni *Mafuta* na *Walenisi*. Riwaya hizi ziliteuliwa kimakusudi. Mafumbo yameteuliwa kwa njia ya makusudi na kuwekwa katika makundi kulingana na jinsi mafumbo hayo yalivyojengwa. Kila fumbo lilochaguliwa limeweza kutusaidia katika kufikia malengo yetu ya utafiti.

### 1.9.4 Ukusanyaji wa Data

Kusoma na kuchanganua data ndiyo mbinu kuu iliyotumiwa katika utafiti huu. Riwaya za *Walenisi* na *Mafuta* zilisomwa kwa kina na mafumbo mbalimbali yaliweza kudondolewa huku yakiwekwa katika makundi mbalimbali. Aidha, data imekusanywa kupitia kwa kusoma vitabu vyovyote vinavyohusiana na Nadharia Amali. Mbinu nyingine iliyotumiwa ni kudondoa baadhi ya maandishi maalum ambayo kulingana na utafiti huu yanatumia mbinu za lugha hususani ufumbaji ili kupata data.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data umefanywa kwa kuongozwa na mbinu ya uchanganuzi matini kwa kuzingatia aina za mafumbo aliyotumia mwandishi pamoja na kuonyesha jinsi mafumbo hayo yalivyotumiwa na Mkangi kwa nia ya kumzindua msomaji.

Data imechanganuliwa kwa kuzingatia sehemu za riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi* zilizo na aina za mafumbo ambayo yametumiwa kuzindua jamii. Data iliyokusanywa imechanganuliwa kwa kuongozwa na malengo na Nadharia Amali. Uchanganuzi wa yaliyomo umefanyika ili kutoa muundo unaofaa kwa utafiti huu. Mbinu ya ustahilifu imetumika. Hii ni mbinu ambayo inamruhusu mtafiti kufanya au kupata jambo au kitu fulani maalum.

### 1.9.6 Uwasilishaji wa Data

Data iliyokusanywa na kuchanganuliwa imewasilishwa kwa njia ya maelezo. Data hii imenukuliwa na kuwasilishwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti.

### 1.9.7 Kiishilio

Sura hii imeshughulikia usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete, upeo na mipaka ya utafiti, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, msingi wa kinadharia, mapitio ya maandishi na mbinu za utafiti.

## SURA YA PILI

## MCHANGO WA MAZINGIRA YA MWANDISHI KATIKA MATUMIZI YA MAFUMBO

### 2.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia historia ya mwandishi na mchango wa mazingira yake katika matumizi ya mafumbo ili kumzindua msomaji. Katika kushughulikia historia ya mwandishi tumezingatia mambo sita: kuzaliwa kwake, kisomo chake, kazi aliyoifanya, uandishi wake, hali ya kisiasa dhidi ya waandishi wakati wa Uandishi wake na watu waliomwathiri katika maisha yake. Kushughulikia maisha ya mwandishi ni muhimu kwa sababu husaidia kuweka msingi bora wa kuelewa namna tajriba yake ya maisha ilivyoathiri falsafa, imani na mtazamo wake katika uandishi wake. Aidha, sehemu hii imesaidia kuonyesha mahali ambapo mwandishi alipata mafumbo. Hali kadhalika, sehemu hii imeshughulikia aina ya mafumbo yanayopatikana katika mazingira ya Mkangi.

### 2.1 Kuhusu Mwandishi wa Riwaya za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995)

George Katama Mkangi alizaliwa mkoani pwani, nchini Kenya, mnamo mwezi wa Machi, Tarehe ishirini, mwaka wa 1944, sehemu ya Ribe.

#### 2.1.1Kisomo

Mkangi alianza masomo yake katika shule moja ya Kiarabu ambapo alifanya mtihani wa C.E.E (Common Entrance Examination). Baada ya kuupita mtihani huu, alijiunga na shule ya msingi ya Mariakani katika darasa la tano na sita. Huu ulikuwa mwaka wa 1956 na 1957. Baadaye alijiunga na St. Michael Giriama, akasoma huko mwaka wa 1958 na 1959. Alifanya mtihani wa KAPE. Hapa alifaulu na kujiunga na St. George Giriama mwaka 1960-1963.

Alifanya mtihani wa kidato cha nne uliojulikana kwa jina Cambridge Examination. Alipita katika daraja la kwanza. Alijiunga na Strathmore school mwaka wa 1964 katika kidato cha tano na kufanya mtihani wa kidato cha sita mwaka wa 1965. Baada ya mtihani huu uliojulikana kama Cambridge Higher Examination, alifaulu na kujiunga na Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki huko Dar-es salaam (sasa Chuo Kikuu cha Dar-es salaam). Huko alisomea jiografia, Isimu, Elimu jamii na Kiswahili.

Kati ya mwaka wa 1972-1973, alijiunga na chuo kikuu huko Uingereza ambako alipata shahada ya Uzamifu katika Elimu jamii.

**2.1.2 Kazi**

Baada ya mtihani wa kidato cha sita, Mkangi alifanya kazi na East African Harbours mjini Mombasa, kabla ya kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar-es salaam. Huu ulikuwa mwaka wa 1967. Baada ya kumaliza masomo ya chuo kikuu, alisomesha katika shule ya upili ya Ribe. Huu ulikuwa mwaka wa 1971. Mwaka wa 1972 alipandishwa cheo na kuwa mwalimu wa shule ya upili ya Dr. Aggrey. Hapa alikaa kwa muda wa miezi sita na akapata udhamini kwenda kusomea shahada ya uzamili huko Uingereza. Katika chuo hiki pia aliweza kusomea shahada ya uzamifu na kuhitimu mwaka wa 1978.

Baada ya kupata digrii ya Uzamifu, Mkangi alikuwa mhadhiri katika Idara ya Sosiolojia, Chuo Kikuu cha Nairobi. Wakati huu ndipo alipojitokeza kama mhakiki wa jamii na katika mihadhara yake, alizungumza waziwazi juu ya maovu ya kijamii na kisiasa ambayo yalitokana na uongozi mbaya. Baadhi ya maonevu aliyoyazungumuzia Mkangi ni kama vile uovu uliokuwepo katika utawala usiotilia maanani masilahi ya wengi, dhuluma, mateso, ukandamizaji, matumizi mabaya ya asasi kama mahakama na polisi, harakati za kitabaka, unyanyasaji wa wafanyakazi, ubaguzi katika viwango tofauti miongoni mwa maovu mengine. Kitendo cha kuzungumzia maovu ya kijamii na kisiasa kilikuwa kitendo cha ujasiri mkubwa kwa sababu wakati huo, uhuru wa kujieleza ulidhibitiwa nchini Kenya.

Maoni na mawazo ya Mkangi yalijitokeza katika mihadhara yake na makala yake yalichapishwa magazetini na vitabuni. Ilibainika kwamba, msingi wa upinzani wa Mkangi ulijikita katika tofauti za kiitikadi. Itikadi yake ya kijamaa iligongana na mfumo wa kibepari uliotawala jamii yake. Hakuficha chuki yake dhidi ya mfumo wa kibepari. Mwelekeo huu unadhihirika waziwazi katika riwaya zake *Mafuta* na *Walenisi*. Toni ya uchungu inayotawala riwaya hizi na inayotiliwa nguvu na uteuzi wa istiari za uchafu na uovu mathalani sumu, ujambazi, uigaji, matapiko, nyute, kinyesi na mikojo inaakisi uchungu aliokuwa nao mwandishi. Mbinu aliyotumia Mkangi ya kupanua mandhari au kuyarefusha ni mbinu zinazotumiwa na waandishi wengi wanaoandika katika mazingira sawa na aliyoandika.

Kitendo cha kuzungumzia maovu ya kijamii na kisiasa katika mihadhara yake akiwa mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Nairobi, ambayo yalitokana na uongozi mbaya kilimpelekea kukamatwa na kutiwa kizuizini na serikali ya KANU. Mkangi alipoteza kazi yake kama

mhadhiri wa chuo kikuu cha Nairobi baada ya kutiwa kizuizini. Alipoachiliwa kutoka kizuizini, Mkangi alinyimwa kazi katika vyuo vyote vikuu vya kitaifa (Vunyoli, 2004, Chacha, 2003). Baadaye Mkangi aliajiriwa katika Chuo Kikuu cha USIU kisicho cha serikali jijini Nairobi ambapo alifunza mpaka alipofariki katika ajali ya barabarani mwaka wa (2004).

### 2.1.3 Uandishi wake

Uandishi wa Mkangi ulianza akiwa katika Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam. Akiwa huko, aliandika riwaya ya *Ukiwa* (1975). Mwandishi aliungama kwamba alitiwa hamasa kujitupa katika ulingo wa uandishi na mwalimu wake Profesa George Mhina. Kuna mambo kadha yaliyomtia motisha ya kuandika *Ukiwa* kulingana na mahojiano ya Mkangi na Chacha (2003). Aliungama kuwa *Ukiwa* ni tawasifu yake. Alikuwa akiandika matukio yake mwenyewe ya ujana.

Riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* ni riwaya zinazojihusisha kwa kiasi kikubwa na suala la siasa. Mkangi anasema riwaya hizi za kufikirisha na zinazochochea msomaji ajitazame upya pamoja na kuichunguza jamii yake kwa jicho pevu na la ndani. Kazi zake zingine ambazo ameandika ni kama, Hadithi za Mfalume Tapwaratapwara (2003). Hii ni hadithi fupi. Kazi zake ambazo hazijachapishwa ni :

1) Mlo (Maskini Liberation Organizotion)
2) Mswada wa-Ningekuwa Mungu (Tamthilia)
3) Mazingaombwe
4) Matunda Sita Mtini (Hadithi za watoto)

### 2.1.4 Hali ya kisiasa dhidi ya waandishi wakati wa Uandishi wake

Utawala wa Kenya, Mkangi akiandika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*, haukuweza kuvumilia kukosolewa. Wasomi na wanaharakati kama Mkangi ambao walikuwa wazalendo na waliotoa maoni yao kwa lengo la kurekebisha jamii walionekana kuwa wasaliti. Serikali iliwaona kama maadui na ikatangaza vita dhidi yao. Makachero walisambazwa katika vyuo vikuu ili kufuatilia matamshi ya wasomi wenye mawazo ya kimaendeleo (Ogoti, 1995). Makachero walijiunga na wanafunzi katika mihadhara na kurekodi kisiri kauli zilizotolewa na wahadhiri za kuikosoa serikali (Ogoti, 1995). Wahadhiri wengi wakati huo, akiwemo Mkangi walikamatwa na kuwekwa kizuizini kulingana na Chacha (2003) na Vunyoli (2004). Mkangi alihojiwa kwa muda wa siku sabini na tano (75) kabla ya kuwekwa kizuizini. Alihitajika kukiri kuwa ametubu. Mahojiano haya yaliongozwa na aliyekuwa mkuu wa polisi

marehemu Philip Kilonzo. Alipokuwa kizuizini ndipo alipoandika riwaya ya *Walenisi*. Katika riwaya za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995) Mkangi ameeleza mateso ya wafungwa wa kisiasa kulingana na tajriba yake alipokuwa kizuizini kwa miaka miwili.

Sababu rasmi iliyotolewa kwa kukamatwa kwa Mkangi ilikuwa kwamba alikuwa mwanachama wa kundi la kisiri la *Mwakenya* liloendesha Shughuli za chini kwa chini kuiangusha serikali ya KANU. Lakini Wakenya wengi waliamini kwamba sababu hasa ya kukamatwa kwake ilikuwa ni mawazo, itikadi na msimamo wake ambao ulipingana na ule wa utawala (Mbatiah, 2003). Baada ya kuachiliwa kutoka kizuizini, Mkangi aliadhibiwa kwa kunyimwa kazi katika vyuo vikuu vya kitaifa (Vunyoli, 2004, Chacha, 2003). Hivi ndivyo serikali ya wakati huo ilivyokuwa ikiwaadhibu maadui zake miongoni mwa adhabu nyingine.

Kwa muhtasari, dhuluma zilizokuwa nchini na kuzuiliwa kwa Mkangi kulichangia katika uandishi wa riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Kwa hivyo aliaandika riwaya hizi kiuamilifu ili kuwamulikia Wakenya dhuluma zinazofanywa dhidi yao na viongozi dhalimu. Lengo la kuwamulikia maovu haya ni kuwazindua ili wapiganie mapinduzi katika jamii.

### 2.1.5 Watu Waliomwathiri

Mawazo ya Mkangi yaliathiriwa na watu wafuatao kulingana na mahojiano yake na Chacha (2003) na Vunyoli (2004). Mwalimu Nyerere, Karl Marx, Walter Rodney, Fidel Castro, Shaaban Robert na Yesu Kristo (hasa mtindo wake wa kutumia mbazi).

Wengine waliomwathiri ni wanamapinduzi kama Mao Tse Tung, Augostino Neto wa Angola, Kwame Nkurumah wa Ghana, Nelson Mandela aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Thomas Sankara aliyekuwa wakati mmoja Rais wa Burkina Faso na Muamar Gadhafi wa Libya. Wengi wa waandishi waliomwathiri kuhusu uongozi ni watu walioshikilia mawazo ya mrengo wa kushoto. Siasa zao ziliegemea katika ujamaa, mfumo ambao Mkangi ameupendelea sana katika maisha yake na ambao umeathiri dhamira za riwaya zake *Mafuta* na *Walenisi.*

Katika kutoa sababu iliyomsukuma kuandika riwaya ya Mafuta Mkangi anasema:

> ‘‘Niliandika Mafuta mwaka wa 1984, wakati wa serikali ya ukandamizaji. Niliandika kuonyesha udhalimu mkubwa uliokwepo. Wakati huo, nilikuwa katika mapambano ya kuona kuwa katika nchi yetu imejitoa katika hali iliyokuwepo (ukandamiziji, udhalimu, ukatili wa viongozi na idhilali za kila aina). Ilinibidi niandike Mafuta

> kimafumbo. Kitabu chenyewe ni kigumu.''(Chacha 2003:47)

Kutokana na dondoo hili, Mkangi amesema mtindo wa kimafumbo ni mgumu. Hata hivyo, ni wazi kuwa alitumia mafumbo kimakusudi kupitisha ujumbe wake kwa wasomaji wake ili wazinduliwe kuhusu hali zao halisi na waweze kuchukua hatua zifaazo kujinasua kutoka katika ukandamizaji uliokuwepo. Mawazo katika dondoo hili yanaafikiana na msingi wa Nadharia Amali unaohusu kazi za uamilifu wa kitu fulani. Kwa hivyo, Mkangi aliandika riwaya hizi ili kumulika maovu yanayotendewa wanajamii na watawala. Ikiwezekana wapiganie haki na usawa katika jamii yao.

Uandishi wa riwaya za *Mafuta* 1984 na *Walenisi* 1995, ulichochewa na jinsi mambo yalivyokuwa humu nchini. Riwaya hizi zinaiponda serikali kwa vitendo vya udhalimu kwa wananchi. Mkangi alitumia mafumbo kuelezea uhalisi wa mambo akiwa na lengo la kuwazindua wasomaji wake wapiganie taifa lenye usawa. Mwito huu ni nguzo ya Nadharia Amali inayosisitiza athari au uamilifu wa kazi fulani kwa hadhira (athari kama vile kuburudisha, kufunza au kuibua mihemko) na kupima umuhimu wa kazi kulingana na kufaulu katika kufikia lengo hili.

**2.2 Mchango wa Mazingira Katika Matumizi ya Mafumbo**

Wakati Mkangi alipokuwa akiandika riwaya hizi, uhuru wa kuikosoa serikali iliyokuwa mamlakani haukuwepo. Kazi zilizoonyesha uozo wa serikali na jamii zilipigwa vita. Waandishi kama Ngugi wa Thiong'o, Alamin Mazrui, Oyugi Okong'o na wengine walitiwa kizuizini kuhusiana na maandishi yao yaliyokuwa yakitoa shutuma dhidi ya serikali (Vunyoli, 2004). Alamin Mazrui aliandika tamthilia ya *Kilio cha Haki* (1981). Wakati huu kulikuwa na dhuluma serikalini dhidi ya wanaharakati wakitetea haki katika nyanja mbalimbali za maisha.

Mkangi amehiari kutumia mafumbo kwa sababu muhimu, kama alivyosema Abdilatif Abdalla (1973 : 23), katika shairi lake KUNO KUNENA, ubeti wa pili:

> Kuna na huku kunena, kunena hakutakiwi,
> Kunena wanakuona, kunena kwamba si kuwi'
> Kunena wakikuona, kukuita hawakawi,
> Kunena kani kwanuka, nikome kukunena?

Abdilatif alisema mambo haya baada ya kuwekwa kizuizini kutokana na yale aliyokuwa amesema katika makala ya ''Kenya Twendapi?'' Hapa anaeleza kuwa kunena hakutakiwi na

ikiwa watakuona basi watakutia na kukutenga na jamii. Maneno ya mdomo yanatoa hisia kuliko maandishi. Kutokana na mazingira haya ya kisiasa yaliyokuwepo nyakati hizo nchini Kenya, waandishi walioandika kuzindua umma kutokana na maovu ya mfumo wa kibepari uliojaa unyonyaji na dhuluma za kila aina, walilazimika kutekeleza haya kichinichini, kimafumbo, kwa minajili ya kuikwepa mitego ya makachero wa chama tawala cha wakati huo KANU; na kutokana na sababu kuwa utawala wa Kenya wakati huo haukuvumilia kukosolewa. Wasomi kama Mkangi ambao walikuwa wazalendo na waliotoa maoni yao kwa lengo la kurekebisha jamii walichukuliwa hatua ya kutiwa kizuizini (Ogoti, 1995). Serikali iliwaona kama wachochezi.

Kutokana na ufafanuzi huu ni dhahiri kuwa Mkangi alihiari kutumia mbinu za lugha hususani mafumbo ili yachukuane na mazingira ya wakati huo. Aliamua kutumia mafumbo katika uandishi wake ili kuepukana na mkono wa serikali. Chini ya mbinu hii, mafumbo, aliwasilisha maana nzito zenye kukabili maswala mbalimbali nyeti ya kisiasa, kijamii, kidini na kiuchumi. Mkangi aliungama katika mahojiano yake na Chacha (2003 ) na Vunyoli (2004) kwamba, aliandika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* kuichambua serikali ya KANU kutokana na udhalimu wake kwa wananchi. Kupitia kwa mafumbo, Mkangi analenga kuwamulikia wanajamii maovu ya serikali ya KANU na kushindwa kwake kutekeleza matakwa ya wananchi. Mafumbo anayotumia yanaonyesha migogoro iliyomo katika jamii ya kitabaka ili msomaji afafanukiwe na hali halisi katika maisha.

Mazingira ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii yaliyomzingira Mkangi alipokuwa akiandika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* yalimsukuma kuwazindua wanajamii kuhusu hali halisi iliyokuwepo nchini na wakati uo huo kuwatolea suluhu la kukabiliana na hali hizo kupitia kwa mapinduzi. Mazingira ya mwandishi hayana budi kuoana na yale anayoandika. Hivyo basi, fasihi haina budi ichunguzwe katika muktadha wa kumhusisha binadamu sio tu na nguvu za kimaumbile, bali pia na nguvu zinazotokana na jamii yake ambazo huweza kuathiri mawazo ‘na mielekeo yake kama anavyosema Candwell (1947: 29):

> Ulimwengu huu wa kisanaa ni ulimwengu wa hisia za kijamii, ulimwengu wa maneno na picha ambao umejengwa kutokana na tajriba ya maisha ya wote, hisia za utangamano kwa wote.

Kutokana na mawazo haya utafiti huu uliwajibika kutilia maanani nguvu mbalimbali za kimazingira ‘ambazo ni chimbuko la kazi ya sanaa, nguvu ambazo hujenga tajriba ya msanii

inayompa hamasa ya kuifuma kazi yake. Haya ni kulingana na msingi wa Nadharia Amali kwamba nadharia hii hujishughulisha sana na muktadha (Levinson, 1983: 9). Kazi yoyote ya sanaa hutungwa katika muktadha fulani na uelewaji wa muktadha ni muhimu sana katika kuelewa maana alizokusudia mwandishi.

Willet (1964: 107) akimnukuu Brecht, anasema kwamba ni kwa maslahi ya jamii ambapo fasihi inatakiwa kutoa vielelezo kwa ukweli wa maisha, vielelezo ambavyo vina manufaa kwa umma. Haya ni kulingana na Nadharia Amali tukidhukuru msingi wa matokeo au mwisho wa kitu fulani ili kutathmini umuhimu wa kitu hicho. Mkangi kutokana na mazingira yake alitoa mafumbo katika uhalisia wa maisha wakati alipoandika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi.* Hali ya kutumia mafumbo yenye uhalisi kulingana na Nochlin (1971: 42) ni kama kuondoa shuka la njozi lililofunika uhalisi kwenye mambo yanayozungumziwa. Stronberg (1968), akinukuliwa na Momanyi (1968), alikiri maoni haya aliposema kuwa, mwandishi anayeandika kutokana na uhalisia wa mambo anachota maudhui yake kutoka kwa watu halisi na mazingira halisi.

Aidha, watu waliomwaathiri Mkangi walichangia katika matumizi ya mafumbo mathalani, Shabaan Robert ambaye alipendelea mno mtindo wa uandishi alioutumia Mkangi wa kutumia hadithi na motifu ya safari kutolea maudhui yake. Shabaan Robert alipendelea pia kuandika kimafumbo, mtindo ambao ulimwathiri Mkangi katika kazi yake.

Vilevile, tajriba ya Mkangi alipokuwa kizuizini ilichangia katika matumizi ya mafumbo hasa dhuluma zilizotendewa wafungwa wa kisiasa. Halikadhalika, kusomea kwake katika Chuo Kikuu cha Dar-es-saalam nchini Tanzania kulimwathiri kuhusu mafumbo yanayosawiri uzuri wa ujamaa aliyotumia katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*.

Katika sehemu inayofuata utafiti huu umeshughulikia aina za mafumbo yanayopatikana katika mazingira ya mwandishi na ambayo baadaye yanabainika katika kazi zake.

### 2.3 Aina za Mafumbo

Mafumbo hutumiwa kuelezea kauli ambazo huficha maana fulani (Wamitila, 2004). Wamitila (mtaje), anaendelea kusema kuwa, huwa kuna jambo ambalo limefumbwa ambalo msikilizaji anahitajika kufumbua labda kwa kujibu swali au kutoa ufumbuzi unaotakiwa. Aidha, anamaliza kwa kusema kwamba mafumbo pia huweza kuwa maelezo marefu ambayo yamefumba kitu (au jibu) ambacho msikilizaji anaweza kukifumbua au kukielewa.

Wataalamu wa fasihi wameibuka na njia mbalimbali za kuainisha mafumbo. Senkoro (1982:37) anatambua makundi matatu makuu ya mafumbo: jazanda, taswira na istiari. Anasema kuwa mafumbo yaliyojengwa ndani ya tamathali za usemi huwezesha ujumbe kuganda vizuri akilini mwa msomaji. Hivi ndivyo alivyofanya Mkangi katika kuteua tamathali za istiari, tashbihi, jazanda na nyingine ili kutupa ule uhalisi katika mafumbo anayoibua.

Aina ya mafumbo hutokana na jinsi yalivyobuniwa na kutumiwa kulingana na wajibu yaliyopewa. Leech (1969:147, 150, 152, 156), Mwenda (2004), Wamitila (2004), Musembi (2005) na Wangari (2011), wanaafikiana kuwa ujumbe hufumbwa katika tamathali mbalimbali za usemi kama vile: taswira, jazanda, istiari, ishara, mbazi tashbihi na hata methali. Hivyo ni kusema kuwa wasanii hutumia mbinu za taswira, jazanda, istiari na hata methali kama nyenzo za ufumbaji.

Leech (1969), akifafanua taswira hasa za kiishara (zionekanazo), anasema kuwa taswira hizi hujengwa katika akili ya msomaji kutokana na uteuzi wa lugha ya mwandishi. Taswira hizi ni zile zinazohusiana na kusimama kwa ‘‘niaba ya’’. Leech (mtaje), anaendelea kusema kwamba taswira za kiishara huunda picha iliyo na ujumbe uliofichika au ujumbe wa ziada. Hivyo taswira hizi huhitaji kufumbuliwa kwani huwa na maana nasibishi ambayo ni tofauti na maana asili ya neno. Aidha, anamalizia kwa kusema kuwa, kwa jumla taswira za kiishara zina uwezo wa kubeba maana tofauti kutegemea jamii husika. Kutokana na maelezo haya ya Leech ni dhahiri kuwa taswira ni aina mojawapo ya mafumbo aliyotumia Mkangi katika kazi yake.

Mwenda (2004), anaeleza kuwa jazanda ni mafumbo ambamo maana ya kitu imefichika. Anaendelea kueleza kuwa, wakati mwingine mwandishi huwa anawapatia wasomaji wake kazi ya kutafuta na kung’amua maana ya kitendo au hali fulani au kisa kwa kutumia fumbo au kwa kutumia jambo ambalo laeleweka kuwa la kawaida lakini kumbe pana ujumbe uliofichika. Aidha, msanii anaweza kuwa ametumia maneno na visa ambavyo kwa msingi ni vya kawaida kumbe vile visa vyatoa ujumbe mwingine ambao umefumbwa kama jazanda. Tukiangazia maelezo ya Mwenda (mtaje), ni wazi kuwa Mkangi alitumia jazanda kama nyenzo ya kufumba ujumbe wake kwa lengo la kuwazindua wasomaji wake.

Istiari ni namna ya kiubunifu ya kurejelea kitu kingine kilicho na sifa zinazofanana na zile za kile kinachoelezwa (Wangari, 2011). Aidha, anasema kuwa ujumbe kupitia kwa istiari hutolewa kwa njia iliyofichika. Naye Wamitila (2004: 154), anasema kuwa istiari ni msingi

wa mafumbo au kufichwa kwa maana ambayo msikilizaji au anayetegewa anapaswa kutegua. Hivi ndivyo alivyofanya Mkangi katika kubuni mafumbo yake ili kuwapa wasomaji wake uhalisi wa maisha na kuzinduka ili kupigania haki zao.

Msokile (1993:45) anasema kwamba mafumbo hujengwa kutokana na matumizi ya tamathali za usemi, hasa jazanda, istiari, tashbihi, taswira na ishara zenye kuhusu mawazo, dhana, vitu au maumbile. Jazanda, istiari na ishara huwa na ujumbe uliofichika na huhitaji kufumbuliwa. Halikadhalika, Musembi (2005), anatambua aina tatu kuu za mafumbo: jazanda, taswira na istiari. Musembi (mtaje), anasema kuwa Mkangi alitumia tamathali hizi za usemi ili kushughulikia maswala nyeti na mazito yanayozikumba nchi nyingi za bara la Afrika, ikiwemo Kenya.

Hivyo, kutokana na msingi wa maelezo haya, utafiti huu unaakisi maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu aina za mafumbo na unajikita katika mafumbo aina tatu: taswira, jazanda na istiari.

### 2.4 Kiishilio

Sura hii imeshughulikia historia ya mwandishi, mchango wa mazingira yake katika matumizi ya ufumbaji na aina za mafumbo ambayo yanapatikana katika mazingira ya mwandishi na katika tahakiki nyinginezo, ambazo huenda Mkangi alitumia kuwasilisha tajriba zake katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*.

Sura hii imebainisha kwamba, hali ya kisiasa nchini Kenya wakati Mkangi alipokuwa akiandika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* ilirutubisha matumizi ya ufumbaji. Sio tu mazingira ya kisiasa yaliyoathiri matumizi ya ufumbaji, bali pia mazingira ya kijamii na kiuchumi, ambapo nyenzo kuu za kuzalisha mali zilimilikiwa na tabaka la juu wengi wakiwatumikia kama vile utafiti huu utakavyobainisha katika sura ya tatu na ya nne.

Tajriba ya ndani na nje ya jela, pamoja na kisomo chake ni baadhi ya mambo yaliyomsukuma kutumia aina za mafumbo yapatikanayo katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Kutokana na maelezo haya imedhihirika wazi kwamba fasihi huzuka kutokana na mwandishi kuingiliana na mazingira yake.

Aidha, sura hii imeainisha mafumbo mbalimbali na maoni ya wataalamu wa fasihi. Imedhihirika kwamba, kuna makundi matatu makuu ya mafumbo: taswira, jazanda na istiari.

Mafumbo haya yote yamejengeka ndani ya tamathali za usemi. Mafumbo haya huwezesha ujumbe kuganda vizuri akilini mwa msomaji.

Katika sura ya tatu utafiti huu utafafanua mafumbo aliyotumia Mkangi, katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* ili kuwazindua wasomaji wake katika jamii.

# SURA YA TATU

# MATUMIZI YA UFUMBAJI KAMA KICHOCHEO CHA ZINDUKO KATIKA RIWAYA YA *MAFUTA*

## 3.0 Utangulizi

Sura hii imeangalia jinsi ufumbaji ulivyotumiwa na Mkangi kama kichocheo cha zinduko katika riwaya ya *Mafuta*. Mafumbo yameweza kuangaliwa katika makundi matatu: Taswira, jazanda na istiari. Pia tumeangalia namna ufumbaji umeendeleza au kukwamiza usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Mafuta*. Imekuwa muhimu kutoa ufafanuzi kuhusu dhana 'mhusika' ili tuonyeshe kile tunachozungumzia.

## 3.1 Taswira

Wamitila (2003b: 22b), anatambua aina mbili kuu za taswira: taswira za kimaelezo na za kiishara. Taswira za kimaelezo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi na hazihitaji kufumbuliwa kwani hazina maana fiche au maana ya ziada. Taswira za kiishara nazo huunda picha iliyo na ujumbe uliofichika na huhitaji kufumbuliwa. Taswira za kiishara hufumwa ndani ya tamathali za usemi. Pia Wamitila (2003a; 2003b) anataja aina nyingine za taswira kama vile: taswira za mwendo, taswira za joto, taswira ya harufu, taswira za uoni, taswira za mguso na taswira za usikivu.

Taswira za hisi hushughulikia mielekeo ya mhusika au msomaji kuhusu hali fulani. Huweza kumfanya msomaji awe na wasiwasi, aone woga au apandwe na hasira kwa vile hujihusisha na hisi za ndani (Momanyi, 1991). Taswira hizi zina nguvu kubwa ya kuganda akilini na kumwezesha msomaji kuupata ujumbe wake vizuri.

Hali kadhalika, Msokile (1993:45) anasema kwamba taswira hujengwa kutokana na matumizi ya tamathali za usemi, tashbihi na ishara zenye kuhusu mawazo, dhana, vitu au maumbile. Ujenzi wa taswira humfanya msomaji apate aina mbalimbali za hisi zinazoshughulikiwa na kazi ya kifasihi za kunusa, kuona, na kusikia. Maelezo haya ya Momanyi na Msokile (wataje), yanafafanua athari zinazosababishwa na kazi ya sanaa kwa wasomaji au wahusika. Haya ni kulingana na Nadharia Amali inayoongoza utafiti huu.

### 3.1.1 Taswira ya Mhusika Matope

Matope ni raia anayeishi katika kidimbwi cha matope kama makazi yake. Jina lake la kimajazi linatangaza sifa za wazi na za kuonekana za mhusika anayeitwa hivyo. Anapoletwa mahakamani kutokana na tuhuma ya kuwaosha wateule kwa maji, hulka yake inatisha. Tunaelezwa:

> ‘‘Matope alikuwa yu bado tulii…mate aliyotemewa yakiwa sasa yaanza kumdenwa ute, damu zikimchuruzika, maumivu yakimchoma kama miba, huku mashavu na viungo vikimwiva kwa shauri ya makofi, mateke, bakora na marungu…’’(uk.43).

Taswira ya matope inaashiria mateso aliyotendewa katika uhalisia wa maisha, kumtemea binadamu mate ni kitendo cha kutomthamini kama binadamu. Pia taswira ya kuonekana kwa damu iliyokuwa ikimchuruzika Matope inaonyesha athari ya kichapo alichokipata kutoka kwa watesaji wake. Maumivu ya Matope yanalingalishwa na maumivu yampatayo mtu anapochomwa na miiba kuonyesha uchungu wa maumivu yale. Mashavu ya Matope yalikuwa yamevimba na kubadilika rangi kutokana na makofi na mateke. Matumizi ya bakora na marungu kumchapia binadamu ni ithibati ya kumnyanyasa bila kujali mahali ambapo rungu hiyo itakapoangukia. Taswira nzima ya Matope inampelekea msomaji kulengwalengwa na machozi. Pia inazindua ujuzi wa msomaji kuhusu mikakati inayotumiwa na watawala kuwadhulumu watawaliwa. Aidha, mitafaruku kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa inaangaziwa. Huu ndio uzinduzi unaowasilishwa na taswira hii. Tunaambiwa kuwa hata waliohudhuria mahakama waliajabia hali mbaya mno ya Matope. Mwandishi anasema:

> ‘‘…kuingia kwake kwa ghafula, kulikomesha kuteswa, kupigwa na kudharauliwa kwa Matope. Umati wote ulisinyaa na kumatamata kule kumwona; ilikuwa mfano wa jibwa lijionapo uso kwa uso na pande la satu- mbele hakuendeki na nyuma hakurudiki bali kujilizaliza kwa kutapatapa. Kimoyomoyoni, alimshukuru mfadhili wake. Ni kweli alikuwa ameshasikia sifa za mtu kama huyu, lakini leo hii, ilikuwa ni kumpasha macho. Kwa kufuatia tabia za wasulubishi wake, kutisha kwa jibaba hili hakukuweza kufichika…’’(uk. 42).

Waliohudhuria mahakama hii hali zao ni sawa na Matope. Walipomwona katika hali ile ya kusikitisha, walishtuka kiasi kwamba hawangejizuia kujamba ovyoovyo na kuendesha papohapo. Maelezo ya mwandishi kuhusu hali ya Matope inaibua taswira ya kiumbe ambaye

hali yake ilikuwa mbaya mno. Alikuwa uchi kama mnyama. Kipande cha tambara alichokivaa kusitiri uchi wake kilitupiliwa mbali na watesaji wake (uk. 43).

Uchi wa Matope ni taswira inayomzindua msomaji. Inaonyesha tofauti za kitabaka zilizopo katika jamii. Dubwana mmoja wa watesaji wa Matope anamkagua kama vile mnunuzi wa kipande cha nguru anavyofanya. Mwandishi anatumia tashibihi kusawiri jinsi Dubwana alivyomwona Matope kama kiumbe asiyekuwa na thamani yoyote. Mwandishi anasema:

> ‘‘Macho ya Dubwana yalimpekua ingawaje alikuwa yu uchi tuputupu. Yakiwa kama darubini na sindano mumo kwa mumo, yalimpekesheni na kumpekecha kwa undani sana kwa minajili ya kutafuta kijisababu. Mwisho, alimkodolea macho kana kwamba kiwiliwili cha Matope kilikuwa kimekaa kama cha zimwi’’ (uk.43).

Kitendo cha Dubwana cha kumkagua Matope aliyekuwa uchi kinaonyesha kwamba katika utawala wa kimabavu watawaliwa hupimwa kwa mizani moja na wanyama. Kawaida binadamu aliye na akili timamu huona haya anapomwangalia binadamu mwingine aliye uchi wa mnyama. Dubwana hakumwangalia tu bali alimkagua kama vile kifaa kinachoitwa darubini hufanya. Kuwa uchi machoni pa wengi kulimtia Matope uchungu ambao mwandishi anaumithilisha na ule wa kudungwa na sindano. Mara nyingi binadamu aliye na akili timamu akivuliwa nguo hadharani hujaribu kujisitiri kwa mikono sehemu zake za siri zisije zikaonekana.

Taswira nzima ya Matope na Dubwana inazua ukinzano. Tofauti yao inalenga kuleta uzinduzi wa mikinzano ya kitabaka kati ya watawala na watawaliwa. Taswira hii inadhihirisha dhima ya mahakama za namna hii zinazotumiwa udhalimu katika jamii. Ni mahakama za wenye nguvu na huwa hazina jukumu la kulinda haki kwa mujibu wa sheria zilizowekwa. Taswira ya mahakama tuliyochorewa na Mkangi inalenga kumzindua msomaji dhidi ya mfumo wa kisiasa ambao unamdhalilisha binadamu kama mnyama, na mfumo ambao hautambui haki za kibinadamu. Mahakama za aina hii hazikujengwa kumtetea mtawaliwa. Lengo la Mkangi anapotuchorea taswira ya Matope ni kuwazindua wasomaji wa Mafuta wafafanukiwe na hali halisi ya hukumu inayowakumba wafungwa. Waliokuja kuhudhuria mahakama walishangazwa na mkasa wa Matope. Waliweza kulipuka kama *volcano* kwa mayowe ya hasira ‘‘ Twambiee Twambieee... Twambieee…(uk. 35). Hii si sauti ya kutaka kufahamu zaidi. Kulipuka kwa wanajamii hawa waliohudhuria kikao hiki cha mahakama, kunaafikiana na msingi wa Nadharia Amali unaohusu matokeo ya kitu fulani.

Hisia hizi zilizoonyeshwa na wahusika hawa, zilitumika kiuamilifu ili kumchochea msomaji ili kuhakiki mfumo mzima wa mahakama. Moja ya malengo ya Mkangi anapomchora Matope katika hali ile ni kubainisha mgogoro wa kitabaka.

Taswira ya mateso aliyofanyiwa Matope inampelekea msomaji kufahamu mzizi wa hali yake, na wakati huo huo anapata mwamko mpya wa kubadilisha hali mbaya inayosababishwa na mikinzano ya kitabaka katika jamii. Mwandishi anasema:

> ‘’Sasa ikiwa mate, halafu makohozi na mwisho, mateke. Ikiwa sasa na mashindano ya yupi angeweza kuja na utesaji wake wa kubuni ambao ulikuwa tofauti kabisa. Mshindi ni yule ambaye alijitokeza na kumkagua juu chini kana kwamba alikuwa hasadiki alichokuwa akikiona…’’ (uk.41).

Mateso ya Matope mahakamani yanachochea uzinduzi. Yanaonyesha wazi migongano ya kitabaka anayozungumzia mwandishi. Jambo hili halihitaji kimya. Linahitaji raia kuungana pamoja na kuyapindua machungu yanayowasakama katika jamii. Taswira ya kuonekana ya mate, makohozi, ute unaomdenwa Matope yanamfanya msomaji ashikwe na kinyaa na wakati huo huo anapata msukumo wa kutaka kubadili hali hii inayochukiza.

Binadamu hapaswi kutendewa vitendo vya aina kama ile kama mnyama. Na anapotendewa vitendo kama hivyo hatarajii virudiwe. Taswira hii inasaidia katika kujenga dhamira kuu ya Mkangi ya uzindushi dhidi ya mikinzano ya kitabaka na dhima ya mahakama. Bila shaka, Mkangi alikuwa na tajriba ya kutosha kumwezesha kuchora taswira zinazoonyesha ukosefu wa haki na dhuluma kwani hata yeye alifungwa kwa miaka miwili kama vile utafiti huu ulivyobainisha awali.

Wakati alipoandika riwaya ya Mafuta (1984) mateso kwa wafungwa katika jamii yake yalikuwa njia ya kuwatia hofu ili wasiweze kusema ukweli (Ogot, 1995). Mtue anaeleza mateso ambayo wafungwa hupitia kwa kusema:

> Ndio mwisho wangu leo, wazo moja lilimjia. Na jingine, watanitia kitanzi, kunipiga marungu ama kunilipua kwa risasi. Hatua hivi, jingine likamjia; hata kamwe, nadhani wanaenda kunitesa tu. Mmmm nitavumilia kweli mimi moto wa spaki uumeni; sindano vidoleni; kutoswa mapipani yaliyojaa maji machafu; kuogofya na majoka ama kupelekwa msituni; Kufungwa kidoto na kutishwa na mabastola; kukemewa; kupondwa na matako ya mabunduki;

> kusukumwa; kutukanwa; kudadisiwa; kufyandwa;
> Kudungwa ku- (uk. 83).

Taswira ya kutiwa kitanzi ili kumtoa binadamu uhai inaleta hisia za waoga na ari ya kutaka kubadilisha mfumo unaopendelea kitendo hiki. Pia kule kupigwa kitutu kwa moto wa spaki uumeni, sindano vidoleni kufyandwa, kutishwa na majoka na mengine mengi ni njia ya kutisha wapinzani wa watawala. Watawaliwa wakijua au wakigundua hivyo hawatakata tamaa katika harakati za kutetea tabaka lao. Mkangi alilenga kuwazindua wanaharakati wasikate tamaa hata wanapotendewa vitendo vya kidhalimu kama hivi kwani ni njia moja ya kuwatisha ili kukomesha vita dhidi ya watawala. Mkangi alilenga kuleta mapinduzi dhidi ya ukosefu wa haki za binadamu kama za wafungwa. Taswira hizi zinaweza kuihangaisha nafsi ya mtu na hivi ndivyo alivyokusudia Mkangi. Taswira za mateso ya Matope zimetumiwa na Mkangi pia kuonyesha dhuluma, ukatili na uhusiano ulio katika mahakama. Mahakama, kanuni yake ni kutunza haki na kulinda washtakiwa lakini mahakama tunayoiona katika riwaya ya Mafuta imekiuka kaida za kutoa haki. Licha ya Matope kuwa kizimbani, aliteswa na kunyimwa haki za kibinadamu. Pia hakuruhusiwa kujitetea. Wakati mwingine watu hucheka mahakamani kutokana na maswali au majibu yanayotolewa. Lakini mahakama hii, Mtue na Ti walipocheka majibizano baina ya Matope na Dubwana walikuwa wanajichongea. Walionekana kama wasaliti, watu wasiotaka kuendeleza dhana ya Mafuta. Wanyanyasaji hutumia vyombo kama mahakama kuonyesha kuwa wanatenda haki ilhali ni uongo mtupu. Kutokana na dhuluma hizi zote, kuna wazo la kuzingatia mapinduzi katika jamii. Mapinduzi haya yatakuwa katika mfumo wa kisiasa, kiuchumi na kijamii kama vile utafiti utakavyobainisha baadaye. Sera ya jamii kuhusu mateso ya wafungwa na sera za mahakama inatakiwa kubadilika. Huu ndio uliokuwa mwito wa Mkangi alipochora taswira ya Matope na aina ya mateso aliyoyapata kule mahakamani.

Mateso ya Matope hayakuwa tu mahakamani bali pia katika jamii ya tabaka la juu. Alipokuwa mahakamani, Matope anaeleza shida zake ambazo zinampelekea msomaji kupata ari na ilhamu ya kutaka kubadilisha hali hiyo. Maelezo ya shida zake yanachora taswira ambazo zinamzindua msomaji. Matope na wengine walikula mapipani. Hii ni ishara ya ulitima au umaskini wa kiwango cha juu. Wateule waliajiri askari ili kulinda uchafu huu ili kina yakhe wasiule. Chakula hiki kinachovunda kinang'ang'aniwa na watu, nzi na kombamwiko. Taswira ya chakula hiki inamfanya msomaji ajiwe na hisia za harufu ya uozo na kushangaa ni vipi binadamu anadunishwa kiasi hiki na jamii. Kwa kawaida chakula kinapotupwa mapipani huvamiwa na wadudu kama nzi na kombamwiko na huwa hakimfai

tena binadamu. Chakula hiki kinaweza kumdhuru mtu iwapo wadudu wachafu kama nzi watakuwa wamekivamia. Maelezo ya chakula hiki na binadamu anayeking'ang'ania ni baadhi ya shida zinazowapata maskini. Taswira inayoibuliwa na mwandishi inalenga kuonyesha vile kina yakhe wamedhunishwa na tabaka la matajiri kiasi cha kuwekwa katika kundi moja na wadudu.

Matope alifanyiwa ukatili wa kila aina. Chakula alichokula alikipata katika pipa alilolizoea, siku moja kilipikiwa ndani ya sumu ya panya. Matope anaeleza mkasa huu:

> Chakula chenyewe, kilikuwa kimepikiwa ndani ya sumu ya panya. Isitoshe, dawa ya kunguni ikawa imepulizwa juu yake kama vile mchuzi… niliduwaa kwa kituo hivi huku nikitamani na kutazama hicho chombo cha mauti. Njaa ilikuwa ikinikata, kunisaga na kunikebei mno. Nile ni sile? Wacha nile nifilie mbali nina maana gani basi? Kwanza ni nani atajua kumekufa mtu? Si ni afadhali kujitoa katika hali hii ya unyonge na utesaji pengine huko ahera huenda nikaonewa huruma? Ni vicheko vya kwikwi ndivyo vilivyonizindua na kunitoa ganzi moyoni. Kutazama furaha hizo zilitoka wapi, niliona wenyeji wangu mtu na mkewe na watoto wao wawili, mmoja mke na mmoja mume-, wamesimama dirishani yenye pazia hafifu nyeupe, wakinicheka undwele wangu (uk.40).

Mwandishi anatuchorea taswira mbili kinzani katika dondoo hili. Taswira moja ya Matope aliyedhoofishwa sana na njaa na taswira ya wenyeji wake wakimchungulia kwa dirisha wakifurahia ushindi wa kunaswa kwa mhusika wao. Taswira hii inamhamasisha msomaji kuhusu wenyeji hawa wa Matope ambao hawana tabia za kiutu kwa kiumbe asiyebahatika. Mbinu ya balagha imetumika hapa kwani maswali ya Matope hayahitaji majibu. Msomaji anafafanukiwa na wazo kwamba mfumo wenye utabaka usiowajali maskini huwapelekea maskini hao kukata tamaa maishani na kujiona kama kundi la watu wasiokuwa na jukumu lolote lile maishani. Madhila ''wenye nacho'' wanayowatendea ''wasio nacho'' ni taswira yenye athari katika jamii ya msomaji. Mkangi alilenga kuwazindua wasomaji kuhusu mfumo wa kitabaka usio na usawa na ambao hukandamiza maskini.

Aidha, Mkangi ametuchorea sura ya Matope. Ngozi yake Matope imesinyaa na amekonga kabla ya siku zake. Akiwa na umri wa miaka ishirini na mitano tu, yuaonekana shaibu aliyebugia chumvi nyingi tofauti na Mtue mwenye umri wa miaka thelathini na mmoja lakini yuaonekana kijana tu. Sababu ya tofauti hii ni taabu zinazowasakama wanyonge. Taabu zote hizo zinaletwa na ubaguzi na kunyimwa 'Mafuta' (kur. 10-11). Kwa hiyo taswira ya Matope

imetumiwa kiuamilifu kuonyesha hali ya wanyonge katika jamii yenye matabaka. Maudhui ya tabaka la chini na ukombozi kupitia taswira ya matope yanatufikia kwa athari kubwa mno. Hali yake inatuonyesha udhaifu wa wanyonge kwa njia ya kusikisha. Zile fikra zinazompita akilini akiwa kizimbani kuhusu wanavyong'ang'ania makombo yaliyotupwa mapipani zina mguso wa kuchukiza na unaoamsha hisia zetu za masikitiko (kur. 36-40). Jinsi alivyovaa magwanda na ngozi kumnyauka kama jani lililokauka anatufanya tuhuzunikie wanyonge wote kwa taabu zinazowapata.

Waama tunapoangalia taswira nzima ya Matope kwa msingi wa Nadharia Amali unaohusu matumizi ili kufunza na kuzindua, anayofanyiwa Matope yamekusudiwa kuonyesha uovu wanaotendewa wanyonge. Mbali na hilo hayo matendo yamekusudiwa kutufanya tulione tabaka la juu kama lenye dhuluma nyingi kwa wanyonge. Hali hii inazua chuki kwa msomaji inayomfanya alione tabaka tawala kama nyanyasaji. Kwa hivyo, taswira ya Matope imetumiwa kiamilifu kuonyesha hali ya mateso ya wanyonge.

Kwa upande mwingine, taswira inayoonyesha msimamo wake imara wa kupigania ukombozi kwa kuwaambia madhalimu ukweli unatufanya turidhike kwamba tumekutana na mwanamapinduzi shujaa asiyetetereka katika nia yake. Hili linatupa tumaini la ushindi wa haki na ukweli dhidi ya dhuluma na uongo. Matope si mwoga. Yeye ni mnyonge aliyezinduka kutoka kwenye usingizi uliowavumbika wengi na kuwafanya wasimtambue adui yao halisi. Huu uzinduzi umemfanya aamue kupigania haki ya wanyonge kwa kuwaambia wateule ukweli wa yale wanayowafanyia.

### 3.1.2 Taswira ya Wateule na Wachochole

Taswira za wateule na makazi yao ya kifahali ikilinganishwa na wachochole wanaoishi katika vidimbwi vya matope inasisimua ari ya wasomaji ya kutaka kuangusha mfumo wa kisiasa wenye matabaka. Jamii yoyote yenye matabaka haishi migongano. Taswira ya wateule walio na Mafuta na walio na uwezo wa kukilalia kitanda ni ya watu wenye nyuso zinazoonyesha kuridhika na maisha. Kuwa mteule ni kuingia katika tabaka la matajiri viongozi. Uteule huu unawapelekea kuwa na nyuso zinazometameta kutokana na kuridhika kwao. Mwandishi anasema:

> Mbeleni kwake kulisimama pande la mtu lililokuwa likimetameta kama jongoo…mashavu yake yalikuwa makubwa na ya kuvimba…tumbo kubwa la kutondoroka na la kufura kana kwamba alikuwa

> amebeba mimba nne. Kizingiti cha shingo kilichopakata kichwa cha kusangika utosini namna ya kiwanja cha ndege, macho meupe yaliyokuwa yakimng'ara mfano wa bundi, yalikuwa yamejishindika kwake kikomoni (uk. 16).

Taswira ya mteule huyu imejengwa ndani ya tamathali ya tashbihi. Mtu huyu anametameta kama jongoo. Jongoo ni mdudu ambaye ngozi yake hung'ara kiasi kwamba inametameta kutokana na wororo huo. Kwa kawaida, binadamu ambaye anapata mahitaji muhimu ya maisha kama chakula, mavazi na ana pesa za kutosha huwa pia na wororo wa ngozi. Baadhi ya wateule katika riwaya ya *Mafuta* wamesawiriwa kuwa na ngozi nyororo kutokana na uteule wao. Pia uvimbe wa tumbo lake unamithilishwa na mama aliyebeba mimba nne ili kubeza sura za viongozi walio na vitambi kutokana na tabia ya uporaji. Taswira ya wororo wa mteule huyu kinyume na jongoo unaotokana na utajiri wa mali. Wororo huu wa ngozi yake unaashiria kuridhika maishani. Shibe yake nayo imesababishwa na unyonyaji wa wanyonge. Macho makubwa meupe kama ya bundi yanaashiria kutisha kwake na ishara ya bahati mbaya. Watu wengi wana imani kwamba ndege huyu aitwaye bundi huashiria kifo, hivyo macho ya mteule huyu yanaashiria kifo kwa mhasiriwa ambaye ni Matope. Taswira ya mteule huyu inachochea uzindushi. Kwanza, kuvimba kwake ni ishara ya unyanyasaji kwa wanyonge. Pia hawa wanyanyasaji huwa radhi kumtia yeyote yule hatiani atakayetuhumiwa na kisirani cha kujaribu kumtoa mamlakani. Mkangi ametumia mbinu ya kejeli kumsawiri mteule huyo ambaye anamfananisha na mdudu, na mama aliyebeba mimba nne - kuonyesha kwamba sura yake ni mbaya na inatisha. Sio wengi wa wasomaji watakaotaka sura kama ya mtu huyo. Kwa hivyo taswira ya mteule huyu imetumika kiuamilifu ili kuibua hisia za zinduko kwa wasomaji wa riwaya hii.

Aidha, Mkangi anatuchorea taswira ya watuele kupitia kwa Mtue kuingia mahakamani. Mshangao wake, anapoingia kwenye jumba la mahakama na kuona yote anayoyaona tunaelezwa hivi:

> ''Umati wa watu, wenye Mafuta, na majumba kubwa kama lile, lilimpoteza fahamu Mtue, mdomo wake ulikuwa wazi na macho kayakodoa kama mtoto aliyekuwa ameona kinyonga. Alikuwa yu katika hali hii ya kuduwaa aliposikia mtu akimsabahi Ti… Alizinduka na kuona jibaba la mtu'' (uk. 16).

Hawa ni watu wenye nyuso zinazometameta kwa Mafuta waliyojipaka. Ni vipande vya watu waliokula vinono vikawanenepesha kama nguruwe. Ni watu wenye uwezo na wanaogofya

hata kwa kuwatazama tu (kur. 16-17). Ila Mtue haogopi hilo. Anapojulishwa kwa njemba moja, analilinganisha na nyoka mkoko (uk. 17), jambo ambalo linamkasirisha mwenzie Ti. Mtue hachelei kuonyesha dharau kwa hayo manjemba. Anamdadisi Ti kuhusu haya manjemba ambapo anaelezwa nyadhifa zao: njemba moja ni waziri wa mguu wa kulia wa mbele ya kitanda (uk. 18). Kwa kuyachora manjemba kwa sura hizi za ajabu, mwandishi anatuonyesha uovu wote wa wateule. Sura zao zimetumiwa kiuamilifu kuonyesha uovu wao. Kinadharia Amali na hasa tukizingatia kipengele cha athari ya kuzindua, chuki anayokuwa nayo Mtue inaibua athari za chuki pia kwa msomaji. Kwa kuibua hisia namna hii, mwandishi anatekeleza alilokusudia – kuamsha ari ya wanyonge katika jamii kupigania haki yao ili wafaidike kutokana na malighafi ya nchi yao.

Mwandishi hahitaji kuwaeleza zaidi hawa wateule. Wamenenepa kutokana na jasho la wanyonge. Wamewanyonya ili kujaza matumbo yao ambayo sasa ni vitambi. Wamewanyofoa wanyonge nyama zote hata na mafuta ya miili yao kiasi kwamba wakati ngozi za wanyonge zimekauka na kuparara kama walio na ukoma, wateule wanametameta kama majongoo. Hata nywele vichwani zinadondoka kwa ajili ya mafuta mengi ambayo hayaziruhusu kushikilia kwa nguvu (uk. 16). Taswira kuhusu wanavyoonekana wateule imetiwa chumvi nyingi mno na mwandishi. Hili limefanywa kimakusudi ili kuleta athari kwa wanyonge. Taswira hii yaweza kueleza kwa msingi wa Nadharia Amali kwamba umuhimu wake unatokana na sababu kwamba mwandishi alitaka kuonyesha tofauti kati yao na wanyonge.

Uteule wao pia unasawiriwa kupitia majumba ya kifahari wanamoishi. Taswira za mandhari wanapoishi wateule zinaashiria utajiri mkubwa wa mali. Majumba yao ni ya kifahari. Tunaambiwa:

> Akumbukacho ni kuingia garini na kujikuta akipitia njia ambayo ilikuwa imenakshiwa na bustani ya kudirwa na yenye kuvutia. Hakusahau jibwa ambalo ingawaje lilikuwa lasemwa kali lilikuwa limejikunja kibandani mwake likikoroma. Chumba alichojikutamo kilikuwa cha kuvutia sana. Kilikuwa na madirisha mawili mapana sana yenye urefu wa kuanzia sakafuni mpaka darini… Nje mandhari za kijani kibichi mara kwa mara ulikatizwa na majumba yaliyojificha.(uk. 14)

Taswira ya jumba hili na mandhari yake yaonyesha utajiri mkubwa. Taswira ya bustani iliyodirwa vizuri na mandhari ya kijani kibichi inaashiria picha ya kupendeza. Jibwa nalo lilikuwa limelala kuashiria kutokuwa na hatari yoyote ile karibu na jumba hilo. Matajiri huwa na mbwa wanaowalinda usiku ili wao wapate usingizi mwororo usiokuwa na tisho lolote lile.

Taswira nzima ya makazi ya kifahari kwa msomaji wa *Mafuta* si ngeni. Hapa nchini Kenya, matajiri huwa na mitaa yao ya kifahari ambayo langoni utasoma maandishi ‘‘MBWA KALI’’. Ni watu wa tabaka lao tu ambao hutengamana nao. Maskini hawaruhusiwi hata kuona mijengo hiyo kutokana na nyua na ulinzi mkali wa mbwa na askari mlangoni. Hali hii ni sawa na aliyoiona Mtue. Hao wateule ndio wanaoweka sheria za mahakama ya ‘waungwana’, sheria zinazotetea upande mmoja tu. Ndio wanaodumisha uwongo wa ‘Mafuta’ na ‘Kitanda’. Ni waongo, wanafiki, madhalimu na wanyanyasaji wanaotesa wanajamii wenzao. Wanaogopa ukweli. Matope anapowatokezea na kuwatajia wanayoyatenda karibu wamue. Hawataki kuambiwa kuwa wanayoyatenda ni mabaya.

Inabainika kuwa hawa viongozi mamwinyi wanafahamu kuwa wanaishi katika uwongo. Dubwana au Dubwasha anapomtembeza Mtue kwenye chumba cha siri zao anamfunulia hizi ‘siri’ za kiuongo (kur. 83-88) kumthibitishia kuwa anayoyajua ndio ya kweli - kwamba ‘Mafuta’ na ‘Kitanda’ ni uongo tu.

Mwisho wa udhalimu huu daima si mzuri. Ndivyo waungwana hawa wanavyoishia kwa fedheha ya kung’olewa uongozini. Wanaachwa hawana chochote hawana lolote pale wanapokumbana na nguvu za wanyonge walioamua kutumia nguvu kujikomboa (kur. 88-89). Kwa tukio hili mwandishi anafaulu kulifikia lengo lake la kuleta ukombozi wa wanaonyanyaswa. Kung’olewa kwa madhalimu kunaweza kuangaliwa kiuamilifu kama kunakotekeleza kusudi la kuleta haki katika jamii.

Kwa upande wa pili, hali ya wachochole inasikitisha. Inazua hali kinzani kabisa na ya wateule. Taswira ya wachochole wakiwakilishwa na Matope, Msati, Jasho, Gweni na wengine, inaashiria umaskini mkubwa. Taswira hii ni kinyume sana na ya Dubwana na wateule wengine. Mwandishi kwa kuonyesha tofauti kati ya matabaka haya mawili, anatuchorea hali ya tabaka chochole. Anatuambia:

> Matope yalikuwa ni yaleyale: makavu na yaliyomkauka. Nywele zilikuwa vilima-vilima vya udongo mkavu ungedhani kichwa chake kilikuwa kichuguu. Mitiririko ya matope yalijisambaza kwake shingoni na huku michirizi yake ikionekana imevunjwavunjwa na kioo ya kuumbika. Kifuani, Matope yakiwa fulana; tumboni, yakiwa ukumbuu; kiunoni, kibobwe; Miguuni, mlongi; na nyayoni, sapata. Mabaki yaliyokuwa awali ni suruali fupi,

> yalionekana yamesitiriwa na ukambaa uliomwingia matakoni na kujitokezea mbele kinenani ambako kibambu cha nguo ndicho kilichoonekana kikimhifadhia heshima yake (uk. 35).

Taswira ya mhusika huyu maskini inamfunza msomaji mengi. Amechorwa kama kidude, sio binadamu. Anaishi katika hali asili. Matope makavu ndiyo yanayositiri uchi. Hii ni taswira inayozua hisia tofautitofauti. Msomaji anajulishwa kuhusu umaskini wa Matope kutokana na uchi wake. Sio tu taswira ya mavazi yake inayoonyesha umaskini wake bali pia makazi ya wachochole katika jamii ya *Mafuta.*

Mkangi ametuchorea taswira za mandhari wanamoishi kina matope. Wachochole wanaishi katika mabanda ya udongo yaliyo na paa zilizoezekwa na matambara ya plastiki, mabati mabovu, na mabaki ya makadibodi (uk.62). Banda la Msati ni mfano mzuri wa makazi haya kama alivyoyaona Ti. Taa ya kibatari iliyotumiwa kwa Msati ni ishara ya umaskini. Maskini hawana sitima kama wateule. Tunaelezwa:

> Mtue alizunguka hapa na pale, asijue pa kwenda. Alijikuta akizozana na vidimbwi vya matope. Bila kufikiri, alivuta makohozi na akawa yu tayari kuyatema humo kidimbwini. Badala yake– aliyameza. Hakuamini alichokiona. Mtu? Binadamu naye alikuwa fofofo usingizini…? Hakutaka kumruka – kwani si adabu njema. Kwa hivyo, alimzunguka huku akijiwazia ya kwamba ingekuwa ubora amwache ajilalie mbali – ya nini kumsumbua? Lakini wazo jingine lilimjia-akamregelea. Alimgusa kwa taratibu na huku moyo ukimwuma na kumwenda mbio (uk. 9).

Taswira ya binadamu aliyelala ndani ya kidimbwi cha matope inaonyesha ukosefu wa malazi bora kwa maskini. Katika uhalisi wa maisha, matope humchafua mtu kiasi kwamba yampatapo binadamu, atataka kuyaosha mara moja ili yamtoke. Pili, matope huwa na umaji maji na baridi kiasi kwamba kulala matopeni kwa binadamu ni kitendo cha kushangaza. Akina Matope walilazimika kulala katika vidimbwi vya matope. Vidimbwi hivi huwa wazi kiasi kwamba hawakusetiriwa kutokana na mvua, baridi na jua kali. Watu hutema mate na makohozi humo kwani ni sehemu iliyo wazi kwa kila mpita njia.

Taswira hii ya binadamu aliyelala ndani ya kidimbwi cha matope ni fumbo alilotumia Mkangi kumaanisha: kwanza, kulala ni hali ya kupumzika baada ya kushughulika siku nzima na shughuli za siku. Inamaanisha mhusika huyu alikuwa amepumzika baada ya kushughulika ili kudumisha ukweli katika jamii yake yenye matabaka. Pili, matope huwa na umajimaji na

baridi ambayo haiwezi kumruhusu binadamu kupata lepe la usingizi. Umajimaji huwakilisha ukweli. Tabaka la wachochole ndilo linalozingatia ukweli. Muda unavyozidi kupita wachochole wanatambua kuwa wamekuwa wakihadaiwa na wateule. Wanaamua kujikomboa kwa kutumia 'maji'-ukweli (kur. 88-89). Tatu, binadamu kulala fofofo matopeni na kutotaka kusumbuliwa inamaanisha tabaka la wachochole huridhika katika kuzingatia ukweli na wanauona uwongo kama usumbufu. Nne, Mkangi alitumia matope kumaanisha kitu kisichothaminiwa. Wateule hawathamini ukweli lakini wachochole huthamini ukweli na ndio sababu wanachagua kulala matopeni. Mwisho, kidimbwi cha matope huwa wazi. Mkangi alimaanisha kuwa ukweli unajulikana na kila mtu lakini wateule hawataki kuuzingatia ukweli huo.

Aidha, Ti anatuchorea taswira ya wachochole anapopelekwa kwa Msati. Nyumba wanazoishi si nyumba bali vibanda – ungesema vya kuku au hata mabata. Milango ya nyumba hizi ni mabamba matupu. Na humo ndimo wanamoishi si watu si kuku, si mabata si wanyama wao. Chakula ni kidogo sana na inawalazimu watu wazima kungoja watoto wale washibe ndipo wao wagawane kilichobakia kisha wajishibishe kwa makopo ya maji. Mkangi anatumia taswira hii kiuamilifu ili kuonyesha kuwa, kama Ti angeyamudu haya maisha mapya ya wachochole basi, huo ungekuwa 'ubatizo mpya' kwake. Lakini hatetereki katika nia yake (kur. 61, 62, 65). Kwa Ti kuyakubali haya yote kwenye taswira hii, pia kumetumika kiuamali kuonyesha kwamba ili kuleta ukombozi katika jamii, sharti waliojitolea kuupigania kwa kuyashinda majaribu mengi ambayo yanaweza kuwavunja moyo.

Tabaka la wachochole limeelezwa vizuri sana na Matope. Kina Zuka, Kazamoyo, Jali, Jasho, Msati, Gweni, Pakacha, Zaitu, Mbeyu na malofa wengine wengi wanaingia hapa. Hawa maskini wa Mungu wameonewa kwa kunyimwa kilicho cha adinasi wote. Wachochole hawa wanatumiwa na tabaka la juu kujizalishia mali zaidi (kur. 1-7). Wanatishwa na kuteswa na hata kufungwa wanapojaribu kupigania masilahi yao (uk. 40). Hali ya maisha yao ni duni mno. Wanalala matopeni wala hawana nguo za kuwasitiri. Nyumba zao zinawaangukia. Kwao chakula ni haba kiasi kwamba wanakunywa maji mengi ndipo washibe (uk. 65). Haya ni maisha ya kuelekea kaburini - 'lakini kifo cha wengi harusi' (uk. 65). Hizi taabu katika taswira hii ya wachochole ndizo zinazowafanya waanze kutafuta suluhisho kwa matatizo yao. Lazima kumwondoa yule anayewanyang'anya na kuwanyima haki zao.

Athari ya masaibu haya kulingana na Nadharia Amali, wachochole wamejifunza kushirikiana, kuungana na kuwa na umoja. Huu umoja ndio unaowasaidia kumudu maisha

magumu yanayowakabili. Kwa vile wao ni kama chungu, wanaenda kuhemara pamoja. Ndiyo maana wanakula pamoja (uk. 65), wanapanga mambo yao pamoja na wakiwa na nia moja (uk. 63). Hili ndilo lililokuwa lengo la Mkangi kwa wanajamii. Wanyonge wanafahamu kuwa umoja wao unaweza kusukwasukwa iwapo wasaliti wataingia kati yao. Kwa kujiepusha na hili, wako macho kwa yeyote mgeni anayekuja kati yao. Kuja kwa Ti kunachukuliwa kwa tahadhari kubwa asije akawa mbwa mwitu kati yao (uk. 56).

Mwandishi amewachora wachochole kama watu wanaoishi maisha ya kihalali na yanayozingatia ukweli. Hawana haja ya kuficha lolote. Wao wamejiosha na wanazingatia ukweli. Hayo maji yamewaosha macho na kuwawezesha kuona vitokako vita – si nje, ni ndani (uk. 78). Kwa jinsi hii wamechorwa kama watu walioamka kisiasa na kupevushwa na hali ya jamii yao. Hali hii inamwezesha mwandishi kufikia lengo lake la kuwaamsha wanaonyanyaswa katika jamii ili wapiganie haki zao. Aidha, haya ni matumizi ambayo yanaweza kuelezwa kiuamilifu. Nadharia Amali inatuwezesha kuwaona kama waliotumiwa kuonyesha mwamko katika jamii.

Aidha, wachochole hawa wanaonyeshwa kama watu wanaochangamkia maisha. Kuchangamkia kwao maisha kunaonekana baada ya chakula cha jioni. Wanatupiana hadithi na kukumbushana waliyowahi kuyaona awali. Hizi hadithi zao si za kuwapumbaza na kuwaliwaza tu. Zimetumika kiuamilifu ili kuibua athari za zinduko kwa wasomaji. Hadithi hizi zina mafunzo na zimekusudiwa kuwazindua wale ambao bado wamelala.

Mwishowe wachochole wanachorwa kama wanamapinduzi wanaoleta ukombozi kwa jamii yao. Hii ni baada ya kukusanyana na kuwa na nguvu. Wanazitumia hizi nguvu kuleta usawa na kutimiza haki. Wanataka ukweli utawale maisha yao. Kutokana na walivyochorwa basi wanyonge wanajitokeza kama watu wenye msimamo imara na moyo thabiti na hizi sifa ndizo zinazowaletea ushindi ili kuleta mapinduzi aliyokusudia katika kazi hii yake. Wanayatekeleza haya mapinduzi kupitia kwa umoja wao ambao ndio unaowapa nguvu.

Kutokana na taswira hizi, msomaji wa *Mafuta* anafafanukiwa na tofauti iliyopo baina ya matajiri na maskini katika jamii. Athari mbaya mno ya utabaka inajitokeza. Taswira hizi zinamzindua msomaji kwa kumpa ari ya kutaka kubadilisha hali ya wachochole na kujiingiza katika harakati za kupunguza pengo la utabaka lililomo katika jamii yao.

### 3.1.3 Taswira ya Mwenye Mkunazi

Mwenye mkunazi anawakilisha baadhi ya mapebari katika jamii wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Yeye anatajwa kama mzembe na anatumia vijana kama Zuka na Kazamoyo kutunda na kumlindia kunazi wakati yeye analala. Aliweza kuwalipa vijana hawa kwa kuwapa kunazi badala ya pesa. Hali hii inaonyesha kwamba maskini hawawezi kufaidika kutokana na mfumo wa kibepari uliopo katika jamii.

Taswira ya mwenye mkunazi na vijana wanyonye anaowatumia kujitajirisha huku yeye akijipumzisha inatuacha na swali moja kwamba, mbona mkunazi unamlikiwa na mtu mmoja na wengine hawana? Mwenye mkunazi anawakilisha mapebari wanaomiliki njia kuu za uzalishaji mali. Bepari huyu anaashiria unyonyaji na ukandamizaji wa wafanyakazi. Taswira hii inaonyesha ukosefu wa haki na usawa katika mfumo wa kibepari. Zuka anasema:

> ‘‘Ni kwa vipi ni yeye tu ndiye mwenye mkunanzi?’’Akawaelezea na akawaongezea,‘‘ inakuwaje ni yeye tu aruhusuye zitundwe, azipangaye mafingu, ayapaye bei…? Ni yeye… kila kitu ni yeye. Na ukiangalia, tusio na mkunazi tu wengi. Twendeni basi tukamwulize haya maswali kabla ya kumsomea,’’ Zuka akawashauri. Walikubali na wakaanza kupiga mbio kurudi walikotokea. Njiani, wakajikuta hawako peke yao…(uk. 92).

Maswali anayouliza Zuka yanazua zinduko. Jambo linalojitokeza kutokana na maswali haya ni harakati dhidi ya ubepari na unyanyasaji. Pili, kuna masimulizi yanayoelezea mgawanyiko wa jamii katika matabaka. Kutokana na taswira ya mwenye mkunazi baadhi ya migogoro ya kitabaka imefichuliwa. Pia matokeo ya migongano hii yanajulikana. Matokeo haya ni kama vile: wizi, ukosefu wa kazi na kuwepo na kundi la wazururaji wasiokuwa na lolote la kufanya katika jamii. Mkangi anawazindua wahusika wa makundi haya kwamba wanao uwezo wa kuleta mapinduzi. Aidha, msomaji anapata wazo kuwa kundi hili hulazimishwa kushiriki wizi na kuishi katika mazingira haya makali ya uchochole.

Pili, tabaka la wazururaji ndilo linamiliki adui wao. Mwenye mkunazi ndiye adui mkubwa wa jamii siyo wale wanaoshiriki katika wizi wa kunazi zake kama Jali. Jambo la kumiliki nyenzo za uzalishaji mali na wachache ndilo linalopingwa na wanaharakati ambao wanataka usawazishaji wa ugavi wa mali ya asili na kuondoa ukandamizaji na ukatili. Kutokana na taswira ya mkunazi, Mkangi ametumia maandamano ya kundi la wazururaji na wacheza kamari kuonyesha jinsi ambavyo umaskini umeshamiri katika jamii hii.

Mwenye mkunazi anaashiria chanzo cha baadhi ya matatizo katika jamii. Taswira hii inalenga kuwazindua malofa kuhusu hali yao na vilevile kudhihirisha chanzo cha hali hiyo. Taswira hii inalenga kuchachawisha mawazo ya msomaji ili ajue kwamba wanaodhamiriwa ndio wezi sio bali ni wale mabepari ndio wezi wa mali yao asili. Taswira hii inawakilisha unyonyaji unaotendewa kina yakhe na wenye mali. Wanatumikishwa lakini hawalipwi mishahara kutokana na jasho lao na mwenye mkunazi. Mkangi anatoa wito kwa wanajamii wapigane dhidi ya unyonyaji katika jamii unaoletwa na matajiri.

### 3.1.4 Taswira ya Wanamapinduzi

Mkangi anatuchorea taswira ya wanamapinduzi wanaosonga kwa ushujaa kwenda kubadilisha hali yao. Mwandishi anasema:

> Hakuwaona Bwagu na Bwaguzi – ama ni Bwaguzi na Bwagu? – pale walipokuwa wamesimama. Ilimbidi kugeuka kushotoni kwake; na hapo akawaona kipenyenyoni wamejikunyata kwa hofu dhidi yake. Ukubwa, ukaidi, ubarakala, kujinaki na kujiona kwao kote kukawa kumepotea. Kutisha kwao, haya yote yalikuwa matukio yao. Alikuwa yuko nusra kuwasemesha aliposikia kwa mbali mlio wa ‘‘MAJI TU MAJI TU MAJI TU…’’ Mlio huu ulikuja na mngurumo wa kutetemesha nchi na mavumbi kutimuliwa. Alisikia ngurumo za ‘‘MAJI TU’’ zikizidi kupaa na kusonga karibu. Na jinsi vile ulivyozidi kusonga karibu, ndivyo vile akina Dubwana na Dubwasha au ni Bwagu na Bwaguzi? Ama Bwaguzi na Bwagu? Tipwatipwa zao zilivyozidi kusinyaa…Huu ulikuwa ule wakati wa mtu kutaka ardhi ipasuke na immeze…(uk.88).

Picha ya wanamapinduzi wanaosonga kwa ushujaa kwenda kubadilisha hali yao ni chocheo kubwa la zinduko kwa wasomaji. Kutishwa kwa wateule na wanamapinduzi kunaonyesha kwamba, zinduko la makabwela huwaogofya mabepari sana. Siku ya mapinduzi ilikuwa imefika. Taswira ya kujikunyata kwa Bwagu na Bwaguzi huku wakifanana na sanamu kunaonyesha udhaifu na woga waliokuwa nao. Inawapa wasomaji msukumo wa kujijua kwamba wana nguvu za kuleta mabadiliko katika jamii. Msukumo huo unawapelekea kugundua kuwa wanateswa na kuwa wamo katika minyororo ya kiuchumi, kisiasa, kisaikolojia na kijamii na kwamba ni lazima wao wenyewe wajitahidi kujinasua. Mapinduzi kulingana na Mkangi huleta mshtuko na woga mkubwa kwa viongozi wadhalimu. Mwandishi anasema:

> Akina mama Fofi, Mama Shibe na wenziwao, hawakuwa na la kusema. Lao lilikuwa ni bumbuazi la kukumbana na bafe uso kwa uso. Mishindo ya ‘‘MAJI TU MAJI TU’’ iliwafanya kushirai na kuduwaa namna ya sanamu. Kwao, kulikuwa mwisho wa dunia, kwa kuwa, ukweli ukijidhihirisha, uongo hujitenga (uk.88).

Woga uletwao na nguvu za mapinduzi umemithilishwa na woga unaoletwa na kukutana na bafe uso kwa uso. Bafe si nyoka wa kawaida. Ana sumu nyingi inayoweza kuua mara moja. Mapinduzi hukatisha utawala wa mabepari mara moja na hili ndilo Mkangi alilolenga kuwazindua wasomaji kwalo. Taswira ya bafe huweza kumtia mtu woga sana. Iwapo viongozi wanaogopa mapinduzi kama vile mtu anavyomwogopa bafe, basi woga huo unawafanya kuwa wanyonge wasitende lolote. Taswira ya nguvu za mapinduzi iliyofumwa ndani ya tashbihi inaelezwa hivi:

> ‘‘…Mtue aliyafunga macho yake kwa woga na hofu. Kutisha kwa hali hii haikuweza kuzoeleka. Mvumo ulizidi kuja na kung’ong’a kama vile nyuki mzingani. Ardhi ilianza kutetemeka na akajua mwisho umefika. Sijui ni kitu gani kilichomwambia kufungua macho. Alipoyafungua, hakusadiki aliyoyaona.’’ (uk. 88).

Sauti za kusikika za wengi zinamithilishwa na sauti za nyuki mzingani. Hii ni mbinu ya tashbihi ambayo inatomelea nguvu za mapinduzi ambayo yanaletwa na wengi. Mapinduzi haya yana nguvu sana kiasi kwamba mwandishi anayamithilisha na nguvu za mtetemeko wa ardhi. Kupitia kwa taswira hii Mkangi anawazindua wasomaji kuhusu umuhimu wa muungano wa pamoja wa wanaodhulumiwa ili kuleta mapinduzi. Mapinduzi huleta ukombozi na ujenzi wa jamii mpya. Taswira nzima ya wanamapinduzi imetumika kiuamilifu kulingana na Nadharia Amali ili kuwaelimisha wanajamii kuwa, harakati za mapinduzi ni muhimu katika kuleta usawa na haki katika jamii yenye matabaka.

### 3.2 Jazanda

Jazanda ni mafumbo ambamo maana ya kitu imefichika. Wakati mwingine mwandishi huwa anawapatia wasomaji wake kazi ya kutafuta na kung’amua maana ya kitendo au hali fulani au kisa kwa kutumia fumbo au kwa kutumia jambo ambalo laeleweka kuwa la kawaida lakini kumbe pana ujumbe uliofichika.

### 3.2.1 Kitanda na Mafuta (Mikojo ya Paka)

Kitanda ni kifaa kinachotumiwa kwa kulalia. Kitanda na mikojo ya paka (mafuta) imetumiwa katika riwaya ya Mafuta kijazanda, ili kuwapa wasomaji mwamko mpya wa kuwafahamu baadhi ya viongozi ambao hutumia hila na ujanja kujiweka mamlakani.

Katika muktadha wa riwaya ya *Mafuta* kitanda kinawakilisha umwinyi au tabaka la umwinyi. Kuwa mteule ni utabaka na huku ndiko kukilalia kitanda. Kwa upande mwingine, kitendo cha kukilalia kitanda kinawakilisha mbinu za ujanja zilizotumiwa na wakandamizaji hasa watawala tajiri ili kujidumisha katika ngazi za utawala. Siri ya kitanda ilikuwa ikitumiwa na matajiri viongozi hasa ili kuwapumbaza na kuendelea kuwanyanyasa raia. Hili ndilo Mkangi alilenga kuwafafanulia wasomaji wake. Raia walinyimwa haki zao na kukandamizwa kupitia uongo huo wa siri ya kitanda. Mtue alielezwa kuwa:

> ‘‘… ukweli kwamba amefanywa mpumbavu, hapo hatakubali na ataficha. Kwa hivyo, ataeneza uongo. Na huo ndio mpaka wa leo ndio ukweli,’’Wakamwambia. ‘‘ Na pia usisahau ni uwongo huu ndio udumishao masilahi yao.’’ (uk. 85).

Kutokana na dondoo hili, kitanda ni jazanda inayomaanisha kasumba maluwaza wanayotumia watawala ili kuendelea kuongoza kisiasa. Kwa njia hii wanageuza ukweli kuonekana kama ni uongo na uongo ukawa ndio ukweli (kur. 84-87). Tunaweza kuona sumu hii pale raia wanapomwandama Jali na hukumu ya kifo wakichukulia kuwa yeye ndiye mwizi (kur. 5-6). Kutokana na tukio hili ni dhahiri shahiri kuwa wananchi wamechanganyikiwa, wanadanganywa na kuukubali uongo wa wale wanaomiliki njia za kuzalisha mali.

Jazanda ya kitanda ambacho wachochole waliaminishwa kwamba kipo na mpaka wajipake mafuta ili wakilalie inazua wasiwasi na hofu kubwa kwa Mtue. Aliona kitanda aina ya mwakisu kilichokuwa kikining’inia juu ya tagaa za mti uliokaa kama mbuyu. Kitanda hiki hakingeweza kulalika. Msimulizi anaeleza kuwa kukilalia kitanda ni uongo ambao umekuwa ukweli kwa sababu hakuna mteule yeyote ambaye angelitaka kueleza upumbavu wake. Uongo huu ndio uliodumisha masilahi ya watawala. Kutokana na maelezo haya, msomaji anapata hisia za kuhadaiwa na kupuuzwa na viongozi walio mamlakani. Kupitia kwa hisia hizi msomaji anatiwa mwamko wa kutaka kupindua mfumo wa siasa ambao umejengwa kwenye misingi ya uongo na unafiki kama vile mwandishi anavyosawiri. Msimulizi kwa kutumia mhusika Mtue anaeleza:

> ‘‘…na sasa tembea hadi ufike chini ya Kivuli cha KITANDA.’’ Akafanya hivyo. ‘‘Na sasa lala kifudifudi –haswa’’ wakampongeza. ‘‘Sasa lala kichalichali,’’ wakamwamrisha na akatekeleza. ‘‘ na sasa,’’ wakawa wanaye, ‘‘ fanya kinyume cha ulivyofanya sasa hivi.’’ Akawatii. Alipomaliza, wakamwambia, ‘‘na sasa tembea mpaka ufike ule mpaka ulio mbele yako.’’ Akatembea. ‘‘Geuka na urudi.’’ Alipitia tena chini ya KITANDA lakini juu ya kivuli chake na alikuwa yuko karibu kuingia ndani aliposema, ‘‘Hebu simama.’’ Akafanya hivyo. ‘‘Sasa tupa macho juu.’’ Kufanya hivyo, akaona maandishi yakisema: ‘‘KITANDA UMEKILALIA, NA KARIBU UTEULENI.’’ ‘‘Lakini sikukilalia. Ni mavumbi ya kivuli chake-’’ ‘‘ Hapo ni kweli,’’ wakamkubali. ‘‘ Lakini tuambie ni Mteule gani angetaka kukubali upumbavu wake…? Na ni kwa sababu hii, aondokapo huenda akitangaza kwamba sasa yeye ni Mteule kwa kuwa amekilalia. Na usisahau kwamba umefanywa mpumbavu, hapo hatakubali na ataficha. Kwa hivyo ataeneza uongo. Na huo ndio ambao mpaka wa leo ndio umekuwa ukweli,’’ wakamwambia. ‘‘na pia, usisahau ni uongo huu ndio udumishao masilahi yao (kur. 84-85).

Mkangi kwa kutumia jazanda hii ya kitanda, alilenga kuwazindua wasomaji kuhusu ushirikina unaojengwa na watawala ili kudumisha imani katika jambo fulani. Wale wanaopata jambo hili huwa wanajijua na huchelea kutoa siri hizo kwa wengine. Kwao huwa ni siri kali. Katika jazanda hii, unafiki wa viongozi walio katika serikali unawasilishwa. Mwamko huu mpya kwa msomaji unalenga kumtia hisia za kimapinduzi na ujasiri wa jamii mpya iliyo na haki na usawa.

Aidha, mafuta au mikojo ya Paka ni jazanda inayowakilisha uongo watumiao watawala tajiri. Uongo huu ndio unaotumiwa na viongozi walafi, katili na wenye kukandamiza jamii ili waweze kujisitiri katika utawala dhalimu. Mafuta na kitanda vinawakilisha falsafa ya uongo iliyotumiwa na kina Bwagu, Bwaguzi, Dubwana na Dubwasha, falsafa zinazoficha ukweli wa mambo ili kuendeleza dhuluma kwa wanyonge wasio na mafuta na uwezo wa kukilalia kitanda. Ni kwa kutumia falsafa kama hii ya mafuta ndipo wanyonge wanapumbazwa na kupofushwa kiasi cha kukiri kuwa wateule tu ndio wanaostahili kuwa nayo. Kukilalia kitanda au kuwa na mafuta ni jazanda inayomaanisha kujua siri za wateule. Kwa upande mwingine, kukosa mafuta au kutokilalia kitanda ni kutojua siri za wateule.  Siri ya kitanda na mafuta ilikuwa ikitumika ili kuwapumbaza raia.

Kutokana na jazanda hii ya mafuta tunaona Mtue akisumbuliwa na uwongo huu wa ‘mafuta’ kiasi cha kusema:

> ‘‘…nini uteule huu wa mafuta? Si kitanda chafaa kulaliwa na yule anayekihitaji? Usingizi na uchovu hauna simile. Vimkumbapo mtu, hana budi bali kujitupa kitandani. Hana budi kwa kuwa hii ni sheria ya maumbile. Vipi tena kusema kwamba ni wale tu ambao wamepakwa ‘‘Mafuta’’? Usingizi ni usingizi na si kwa mtu, mnyama au mdudu.’’ (kur. 8-9).

Mawazo haya ya Mtue kwa mujibu wa Nadharia Amali, yanaonyesha mzinduko kuhusu hali ya maisha ya jamii yake. Yanatuelekeza kumwona Mtue kama mtu anayetafuta usawa na haki kwa wote katika jamii. Hile ndilo lengo alilokusudia Mkangi la kuwazindua wanajamii ili kupigania haki na usawa katika jamii ya msomaji.

Kuja kwa mama Fofi mahakamani (uk. 19) kunamfanya Mtue achanganyikiwe zaidi. Taabu ya mama Fofi ni kwamba ‘mafuta’ yake ‘yashaoshwa’. Hili ni tatizo kwa Mtue: ‘Tangu lini maji kuosha Mafuta? Si ajifute na taulo mara moja’ (uk. 19). Na huo ndio upofu wa Mtue unaomfanya kuonekana mjinga. Hajui wala hatambui maana ya ‘Mafuta’ na ‘maji’ kuyaosha mpaka sasa. Baadaye anatambua kuwa ‘hii ni porojo tu ili watu wasitambue vikwazo vilivyoko ama hawangejitahidi kujitafutia’ (uk. 20). ‘mafuta’ ni porojo na uwongo wanaofanyiwa watawaliwa ili wasitambue unyanyasaji au upunjwaji wanaofanyiwa. Kwa kubaki katika wingu la kutojua basi watabaki wametulia huku wakinyonywa. Kutofahamu anakoonyesha Mtue kumetumiwa kiuamilifu ili kuonyesha upofu walio nao wanyonge. Imewachukua muda kutambua kuwa wanadanganywa kupitia kwa porojo za kisiasa. Ufahamu anaoupata Mtue una athari za kiuamilifu kwa wanyonge wengine na wasomaji. Ufahamu huu unakusudiwa kuleta athari ya mzinduko kwa wanyonge na wasomaji ili wapate kutambua ukweli wa hali zilizomo katika jamii zao.

Kutokana na maelezo ya wateule, Mtue alitambua kuwa mafuta ni aina moja na yalitiwa katika vyungu saba na kubandikwa majina tofauti. Jambo lililokuwa la kustaajabisha sana ni asili ya mafuta. Mafuta haya yalikuwa mikojo ya paka. Wateule waliojipaka mafuta haya walikuwa wataka kudumisha hadhi yao. Mikojo ya paka kumthilishwa na mafuta ni jambo la kuaibisha mno. Jazanda hii inaibua hisia za mnuso zinazoathiri moyo ili kuhisi uzito wa uongo wa viongozi.

Jazanda ya kitanda na mikojo ya paka ni kichocheo cha zinduko. Msomaji anafafanukiwa na uhalisi kwamba, mara nyingi viongozi walio mamlakani hutumia uongo ili kuwaweka mamlakani. Wengi wao hawana hekima. Wateule wamekula yamini ili wasifichue uongo huu (uk.87).

Kupitia kwa jazanda hii, Mkangi alilenga kuwazindua wasomaji kwamba, katika kitengo cha utawala kuna mambo yanayochukuliwa kama siri kali. Neno ‘‘siri – kali’’ linachukua matamshi ya kimzaha ya serikali (Vunyoli, 2004). Mkangi alitaka kupitisha wazo kuwa wadhalimu wako katika ngazi za utawala na pia kuna mambo katika serikali ambayo ni uongo lakini yamechukuliwa kuwa kweli ili kusitiri walio uongozini. Mwamko anaopata msomaji unaleta hisia za majuto anapofafanukiwa na ukweli kwamba viongozi wanaopaswa kuaminiwa ni wanafiki na washirikina. Mwamko huu hatimaye ni mapinduzi kama alivyodhamiria Mkangi.

### 3.2.2 Safari ya Ti

Safari ni tendo la kwenda masafa ya mbali na mahali mtu alipo (TUKI, 2010). Safari ya Ti baada ya Mtue kutiwa kizuizini imetumiwa kijazanda. Ti alipanga safari kwenda kutafuta jamii ya Mtue iliwajulishe msiba uliompata Mtue. Safari ya Ti ni ngumu mno na ina matatizo mengi. Kijazanda wingi wa matatizo haya inaashiria vikwazo vinavyomkumba mpiganiaji yeyote wa haki za wanajamii wenzake. Ti alikuwa mzawa wa tabaka la wateule, kwa hivyo kujinasibisha na wachochole ni kama ubatizo wa moto. Mwandishi anasema:

> Huku viatu mikononi, alisikia ‘‘tafya’’ pale wayo wake wa kushoto ulipovuka kizingiti njiani kuingia nyumbani. Baridi ya matope haikuwa ikimghasi tena kwa kuwa, juma nzima hakuwa akilala pengine isipokuwa ndani ya kidimbwi. Ungeambiwa kuwa huyu ndiye yule Ti, haungesadiki. Rinda lake lilikuwa limeshaanza kukukutaa kwa shauri ya kuishi matopeni. Ngozi yake ilikuwa imeshashirai kwa kukosa mafuta. Nywele zilikuwa timutimu na kwa jumla, hali yake ilikuwa imekaa kama mwenyeji yeyote yule wa sehemu ile ya mji (uk.61).

Maelezo haya ya mwandishi yanaibua jazanda ya uchovu na uchafu katika safari ya Ti. Hapa Mkangi alilenga kuwazindua wasomaji wake kuhusu mambo matatu: kwanza, umuhimu wa kujitolea kupigania mapinduzi yatakayoleta ujenzi wa jamii mpya. Pili, kuwazindua wasomaji kwamba, mtu akiwa na mtazamo wa kimaendeleo na kibinadamu anaweza kusababisha mapinduzi licha ya utajiri wake, kama alivyofanya Ti ambaye anatoka katika tabaka la

wateule. Pamoja na ugumu na muda mrefu ambao mpiganiaji haki huchukua ili haki ipatikane, Mkangi anawahimiza wanajamii wasife moyo kwani safari huleta mafanikio kama yale yaliyoletwa na safari ya Ti.

Tatu, Mkangi alilenga kuwazindua wasomaji kwamba safari hubadilisha mpiganiaji haki. Baada ya safari, Ti anazinduka na kubadilika. Ametoka katika tabaka la wateule katili wasiokuwa na utu lakini kupitia kwa safari ngumu anarejewa na utu wake. Ti anajiunga na wachochole kama akina Msati, Pakacha, Zaitu, Nyepi na wengine na kutiana nguvu na vuguvugu za mapinduzi yanayolenga ukombozi na ujenzi wa jamii mpya. Aidha, katika muungano wa wengi kuleta mapinduzi, lazima pawepo na kiongozi au viongozi shupavu wasiotetereka.

Safari ya Ti pia imetumiwa na Mkangi kijazanda kuwakilisha harakati za kutafuta au kuvumbua mambo kadhaa. Kwanza, Mkangi anatuwasilishia mhusika Ti akiwa katika harakati za kutafuta ukweli. Ingawa Ti anatoka katika tabaka tawala, hilo pekee linamkera hasa baada ya Mtue, rafikiye, kutiwa ndani. Hafurahii utabaka wake kamwe. Mateso aliyofanyiwa Matope pamoja na kutiwa mbaroni kwa Mtue vinampekecha moyo bila kumpa amani. Matukio haya mawili yanamfanya aanze kutafuta ukweli:

> ‘‘Ajabu ni kwamba nilizaliwa ujingani. Nimekulia ujingani. Nitafia ujingani. Nala, nanywa, nafa ujingani… yaonekana ujinga ni wepesi, ni raha, ni starehe na hausumbui. Ujinga si matatizo, bali ni starehe ya kujiona ni mimi mtu basi ’’ (kur. 51-52).

Huu mzinduko ndio unaomfanya Ti aamue kutafuta ukweli na kuwaunga mkono wanyonge katika kupigania haki yao na usawa. Anaenda matopeni wanakoishi wanyonge. Ni huko ndiko anakopata hali halisi ya maisha ya jamii yake. Kujitosa kwake kwenye safari ya uvumbuzi kunamfanya ajifunze mengi. Kuna watu wanaoishi kwenye vidimbwi vya matope, hawana chakula, makazi wala nguo. Hawa watu wamekukutaa kwa kukosa ‘mafuta’. Na hawa watu ni wengi. Haya yote yanamtia uchungu. Lakini hafi moyo. Ana dhamiri dhabiti ingawa maisha hayo mapya ni magumu kwake – kukosa ‘mafuta’, chakula, maji safi na mahali pa kulala (uk. 61, 65). Pili, safari ya Ti inawakilisha harakati za kutaka kuvumbua na kuleta uhusiano mpya. Mkahawani pa Jasho, Ti anaonyesha dhamiri yake mpya ya kutaka kuleta uhusiano na wanamatope wanaobaguliwa na kudharauliwa. Ti anaamua kuwanunulia chai na kuzua maongezi nao. Kwa kufanya hivyo Ti aliweza kuvunja ukuta unaowatenga wanyonge na mamwinyi (uk. 56-60). Azma yake ni kuishi nao na kuleta usawa katika jamii. Hivi ni vita

vya ukombozi dhidi ya ubaguzi na unyanyasaji uletwao na 'mafuta'. Hapa safari ya Ti imetumiwa kiuamilifu kuonyesha haja ya kuvunja kuta zinazowagawanya watu katika jamii. Safari inatuonyesha kuwa ili kuwepo na usawa sharti watu wajikomboe kifikra, kihali na kimali.

Aidha, Mkangi ametumia Ti mhusika mwanamke kijazanda ili kuwakilisha jamii mpya. Amemtumia Ti kwa kusudi la kuonyesha kuwa wanawake wana jukumu kuu la kujenga jamii mpya na yenye usawa na haki. Wanawake katika jamii yenye ubabe dume huwakilisha wanyonge katika jamii hiyo. Mkangi amemtumia Ti akiwa na lengo la kuwazindua wajamii wanaokandamizwa katika jamii kuwa wana jukumu la kuungana na kuleta mabadiliko katika jamii wanamoishi. Kupitia kwa taswira hii ya Ti, nafasi ya mwanamke inajitokeza wazi katika jamii. Mwanamke ni kiumbe muhimu sana katika jamii. Kwa kuangazia msingi wa Nadharia Amali unaohusu matumizi ya kitu ili kuona muhimu wake, unaafiki jazanda hii ya safari yaTi.

### 3.2.3 Vidimbwi vya Maji na Matope

Kidimbwi ni mahali ardhini palipochimbika na kukaa maji. Ni shimo la maji au bwawa dogo (TUKI, 2004). Kwa upande mwingine tope ni udongo wa majimaji unaonata (TUKI, 2004). Mkangi alitumia vidimbwi vya maji na matope kijazanda. Aidha, kulingana na Nadharia Amali, alizitumia jazanda hizi kiuamilifu ili kuwazindua wasomaji wake kuhusu matatizo wanayoyapata maskini. Matope kulingana na muktadha huu linaashiria uchafu na dhiki inayowakumba wanyonge katika jamii yenye utabaka. Matope ni raia anayeishi katika kidimbwi cha matope kama makazi yake. Aidha, kidimbwi cha maji katika muktadha huu kina maana ya matatizo na dhiki zinazowakumba wanyonge katika jamii kutokana na ukosefu wa mahitaji ya kimsingi. Kawaida, binadamu hulalia kitanda katika jengo fulani ambalo linamsetiri kutokana na baridi, mvua na jua. Matope ni jazanda iliyotumiwa na Mkangi kuonyesha udhalimu wa namna hii katika nchi nyingi za Kiafrika, Kenya ikiwemo. Wanyonge kama watoto wa mitaani kwa jina 'chokoraa' wanateseka pakubwa sana kwa kukosa mahitaji ya kimsingi kama vile malazi, chakula na mavazi. Mkangi analenga kuwazindua wasomaji kuhusu mfumo wa kitabaka usio na usawa na ambao hukandamiza maskini.

Jazanda ya kidimbwi cha maji ambapo wachochole kama Matope hulala inaoonyesha athari ya utabaka. Maskini katika jamii iliyo na matabaka huumia sana kutokana na ukosefu wa mahitaji ya kimsingi kama malazi. Mkangi anatuonyesha binadamu ambaye amelala katika kidimbwi hiki bila kuonyesha usumbufu wowote ule. Tunaambiwa:

> Mtue alizunguka hapa na pale, asijue pa kwenda. Alijikuta akisozana na kidimbwi cha matope. Bila kufikiri, alivuta makohozi na akawa yu tayari kuyatema humo kidimbwini. Badala yake – aliyameza. Hakuamini alichokiona. Mtu? Binadamu. Naye alikuwa fofofo usingizini… hakutaka kumruka – kwani si adabu njema. Kwa hivyo, alimzunguka huku akijiwazia ya kwamba ingekuwa ubora amwache ajilalie mbali – ya nini kumsumbua? Lakini wazo jingine lilimjia – akamregelea. Alimgusa kwa taratibu na huku moyo ukimwuma na kumwenda mbio… Nchi hii vipi? Mtu hawezi hata kulala matopeni bila kusumbuliwa? (uk.9).

Mtue anakutana mara ya kwanza na Matope akiwa amelala fofofo kwenye kidimbwi cha matope. Hilo pekee linatosha kutueleza kuhusu hali ya hawa wanyonge katika jamii. Katika uhalisia wa maisha mtu kulala usingizi wa pono matopeni, hakuna starehe zozote zile. Waama kwa msingi wa Nadharia Amali msomaji anapatwa na hisia za huruma na wasiwasi anapofafanukiwa na wazo kwamba kuna binadamu ambao wanateseka kwa kiasi kikubwa kama vile Matope. Uvumbuzi huu unalenga kumtia msomaji hamasa ya kupanga mapinduzi dhidi ya mfumo wa kisiasa usiowajali maskini kama Matope. Kwa mujibu wa Nadharia Nmali Mkangi alilenga kumzindua msomaji kuhusu chanzo cha matatizo kama vile ukosefu wa malazi katika jamii.

Kule kulalia matope yenye ubaridi na umajimaji bila usumbufu kumetumika kijazanda. Mkangi anatumia umajimaji au maji kumaanisha ukweli. Kulalia matope ya umajimaji ni kule kuishi kwa ukweli. Walioshikilia ukweli wanajipata kwenye matatizo mengi lakini matatizo haya hayatingishi msimamo wao thabiti. Wanaendelea kushikilia ukweli wakiwa na matumaini kuwa watapata ushindi siku moja.

### 3.2.4 Uchi wa Matope

Matope aliletwa mahakamani akiwa amevalia mabaki yaliyokuwa awali ni suruali fupi, yaliyositiriwa na ukambaa uliomwingia matakoni na kujitokeza mbele kinenani ambako kibambu cha nguo ndicho kilichoonekana kikimhifadhia heshima yake (uk.35). Kipande cha tambara alichokivaa kusitiri uchi wake kilitupiliwa mbali na watesaji wake na akabaki uchi wa mnyama, tukio ambalo liliwafurahisha sana hao watesaji wake. Mwandishi anatueleza kuwa:

> Ti alisinyaa alipouona ule ukambaa uliokuwa umemsitiri utu wake ukivutwa na kukatwa kwa hasira. Kufanyiwa hivi, vicheko vikalipuka – vicheko vya kiwehu (uk.41).

Kule kuvutwa kwa ukambaa uliomsitiri utu wake Matope alibaki uchi wa mnyama. Uchi wa Matope ni jazanda inayoashiria usafi wa roho aliokuwa nao Matope licha ya kwamba anateswa. Anararuliwa mararu yake na hakuna makosa ambayo tunaelezwa aliyafanya ili kufanyiwa kitendo hiki cha unyama. Anafikishwa humo mfungwa tayari kwa maana kuwa huko kuletwa mahakamani hakuna umuhimu kwake kwani hatapewa muda wa kujitetea na kusikizwa kwa haki. Kesi yake imekatwa kitambo hata kabla ya kufanyika. Kulipuka kwa vicheko kutoka kwa watesaji wake kunadhihirisha unyama wanaofanyiwa wanyonge. Mahakama yenyewe ni za ‘mwenye nguvu mpishe’. Jazanda hii ya uchi wa Matope inaonyesha tofauti za kitabaka zilizopo katika jamii. Waama kwa msingi wa Nadharia Amali unaohusu matumizi ili kufunza na kuzindua, anayofanyiwa Matope yamekusudiwa kuonyesha uovu wanaotendewa wanyonge. Mbali na hilo hayo matendo yamekusudiwa kutufanya tulione tabaka la juu kama lenye dhuluma nyingi kwa wanyonge. Hali hii inazua chuki kwa msomaji inayomfanya alione tabaka tawala kama nyanyasaji. Kwa hiyo jazanda ya uchi wa Matope imetumiwa kiuamilifu kuonyesha hali ya mateso ya wanyonge wanayofanyiwa na watawala.

Hivyo ndivyo wafanyiwavyo wanyonge ili kuwanyamazisha. Kusudi ni kuwa wanataka kuwafanya wao watulie huku wenye uwezo wakiendelea kuwanyima haki zao na kuwabagua. Dubwana mmoja wa watesaji wa Matope anamkagua kama vile mnunuzi wa kipande cha nguru anavyofanya. Mwandishi anatumia tashbihi kusawiri jinsi Dubwana alivyomwona Matope kama kiumbe asiyekuwa na thamani yoyote. Mwandishi anasema:

> Hapa, Dubwana alimgeukia Matope na akamkagua kama vile mnunuzi wa kipande cha nguru. Tena afadhali huyo basi: kwani ingawaje harufu na tafyatafya haipendilei, kinywani hana budi atakibugia. Lakini hii leo, Matope alijiona akikaguliwa ili aonekane na dosari ya kutoa kisababu cha yeye kukeukwa na baadaye, aangamizwe kabisa. Macho ya Dubwana yalimpekua ingawaje alikuwa yu uchi tuputupu. Yakiwa kama darubini na sindano mumo kwa mumo, yalimpekesheni na kumpekecha kwa undani sana kwa minajili ya kutafuta kijisababu. Mwisho, alimkodolea macho kana kwamba kiwiliwili cha Matope kilikuwa kimekaa kama cha zimwi…(uk.43).

Kitendo cha Dubwana cha kumkagua Matope aliyekuwa uchi ni jazanda inayoonyesha kwamba katika utawala wa kimabavu watawaliwa hupimwa kwa mizani moja na wanyama. Kawaida binadamu aliye na akili timamu huona haya anapomwangalia binadamu mwingine aliye uchi wa mnyama. Lakini ni kawaida kumtazama mnyama yeyote bila aibu ya kujiuliza yuko uchi au la. Kwa upande mwingine, mara nyingi binadamu aliye na akili timamu akitolewa nguo hadharani hujaribu kujisitiri kwa mikono sehemu zake za siri zisije zikaonekana. Lakini kwa Matope wakati huo wote wa kukaguliwa akiwa uchi wa mnyama mwandishi anasema kuwa hata kupesa hakupesa (uk.43). Hali hii ya Matope ya kutoshtuka kutokana na kitendo cha Dubwana cha kumkagua akiwa uchi na hata kutoshughulika kuficha uchi wake, ni jazanda inayomaanisha kuwa mfumo wenye utabaka usiowajali watawaliwa huwapelekea watawaliwa hao kukata tamaa maishani na kujiona kama kundi la watu wasiokuwa na thamani yoyote ile maishani. Jambo hili linadhihirika wazi wengine wanapomuuliza Matope kama yeye ni mtu kweli? (uk.42). Swali hili la balagha limetumiwa kiuamilifu ili kuwazindua wanyonge ili waone uhusiano wao na watawala hawa dhalimu.

Aidha, Mkangi alitumia uchi wa Matope kijazanda kumaanisha umaskini unaowakumba baadhi ya wanajamii na madhila wanayoyapitia maishani kwa sababu ya hali hiyo ya umaskini. Kuwa uchi machoni pa watu wengi kulimtia Matope uchungu ambao mwandishi anaumithilisha na ule wa kudungwa na sindano. Matope ni kiwakilishi cha wanajamii maskini kupindukia. Wamesawiriwa kama binadamu wanaokosa mahitaji yao ya kimsingi kama vile mavazi, makazi na chakula. Ushuhuda kuhusu ufukara wao na madhara yasababishwayo na huo ufukara ni sura yake matope. Ngozi imesinyaa na kukonga kabla ya siku zake. Akiwa na umri wa miaka ishirini na mitano tu, yuaonekana shaibu aliyebugia chumvi nyingi tofauti na Mtue mwenye umri wa miaka thelathini na mmoja lakini yuaonekana kijana tu. Sababu ya tofauti hii ni taabu zinazowasakama wanyonge. Taabu zote hizo zinaletwa na ubaguzi na kunyimwa ‘mafuta’ kama anavyosema msimulizi:

> ‘‘Bila ya kuficha, ilikuwa wazi kabisa kuwa yule bwana hakuwa na budi ila kulala matopeni kwa kuwa hakuwa na mafuta. Na kuingia kitandani sharti mtu awe nayo, ajipake. Ama hana lakini apakwe. Kwa hivyo, na kwa wale ambao hawakuwa nayo, tatizo kubwa lilikuwa jinsi ya kujipatia fursa hii mahsusi ili mradi mtu aweze kujikita kitandani’’ (uk. 10-11).

Si rahisi kwa wanamatope kufurahia maisha kwani wenye uwezo na mali wamewawekea vikwazo na kuwanyima kilicho chao wote. Mwandishi alitumia uchi huu wa mhusika Matope

kiuamilifu kulingana na Nadharia Amali akilenga kuibua hisia za uchungu kwa watawaliwa ili kupigania ukombozi wao.

Hali kadhalika, uchi wa Matope ni jazanda inayomaanisha kusema ukweli bila kuficha lolote hata ingawa ukweli huo unaweza kuzidisha mateso yake kutoka kwa watesaji wake. Hii ndiyo sababu inayomfanya Matope kuwapasulia ukweli pale mahakamani. Anawaambia wenye uwezo hivi:

> ‘‘Tumezaliwa matopeni, tumezaana matopeni, tumekufa matopeni na tutazikwa matopeni… Mmefanya uongo ukawa ukweli na ukweli ukawa uongo…Mmepindua hata sheria za maumbile kumamatia enzi yenu…Unyama wenu ndio utu na utu wetu ndio unyama. Mafuta ndio thawabu na maji ni mauti…Si maji ni uhai? Ni maisha na ni chanzo? Vipi leo yasemekana ni Mafuta? …Tutazuka basi na maji tuyakomboe… kwani maadam vidonda viko, nzi kufa si hasara…’’ (uk. 40-41).

Haya yalitosha kuelezea jazanda yote ya uchi wa matope. Huu ndio ujumbe wote wa wanyonge kwamba ukweli uzingatiwe na utawale bali si uongo. Hili lisipotekelezwa kwa amani basi hapana budi nguvu kutumiwa. Huu ndio msimamo wa wanyonge waliopata zinduko- kina Msati, Jasho, Gweni, Pakacha, Mbeyu, Nyepi na Zaitu. Usemi wa Matope hapo juu umetumiwa kiuamilifu ili kuwachoma wateule. Hawakuzoea kuambiwa ukweli kama huo aliowaambia Matope.

Uchi wa Matope pia umetumika kijazanda kumaanisha kuzinduka kwa mhusika Matope. Matope ni mhusika ambaye amezinduka kutoka kwa ujinga, uongo, woga na propaganda za watawala zilizowavumbika wengi na kuwafanya wasimtambue adui yao halisi. Kuzinduka huku kumemfanya aamue kupigania haki ya wanyonge kwa kuwaambia wateule ukweli wa yale wanayowafanyia. Wakitaka wajirekebishe ila wasipotaka basi nguvu zitumiwe. Kwa jinsi hii basi Matope amesawiriwa kama mwanamapinduzi anayepigania ukombozi wa wanyonge. Ukombozi utapatikana tu iwapo ukweli utazingatiwa. Matope si mwoga. Utulivu unaoonekana usoni pake unaonyesha uhakika alionao kuhusu lile analopigania. Hata baada ya kuteswa habadilishi msimamo wake. Hukumu yake ni ‘unyongwe ili uwe kielelezo kwa wengine’ (uk. 45). Hata hili halimshtui. Wala mawazo ya kimzaha ya Mtue hayakusibu:

> ‘‘Yaonekana kuta tuzijengazo ‘ndicho’ ili kuwazuia watu kama hawa kuja kutuharibia starehe zetu si imara

> ama ndefu vya kutosha vya wao kushindwa kuziparaga.
> Naona marisasi tu ndiyo dawa iliyobaki ''. (uk. 34).

Kwa Matope, hata hiyo risasi haingekuwa dawa mjarabu ya kumnyamazisha. Haki yake ataidai popote pale. Msimamo wake imara wa kupigania ukombozi kwa kuwaambia madhalimu ukweli unatufanya turidhike kwamba tumekutana na mwanamapinduzi shujaa asiyeteteteka katika nia yake. Na hii ni kwa mujibu wa Nadharia Amali.

**3.2.5 Mkunazi**

Mkunazi ni jazanda aliyotumia Mkangi katika muktadha wa riwaya ya mafuta kumaanisha njia kuu za kuzalisha mali au rasilmali za nchi. Njia hizi za kuzalisha mali au rasilmali za nchi ni mali ya kila mwananchi katika jamii yenye usawa na haki. Haya ni kinyume katika riwaya ya *Mafuta* ambapo Mkangi anatuonyesha wanaomiliki njia za uzalishaji wakiwa wachache mno tukilinganisha na wasiokuwa nacho. Si kwamba rasilmali yenyewe ni ndogo kiasi cha kutowatosha wote. La, hasha. Suala ni kwamba rasilmali iliyopo imemilikiwa na wachache na ugavi wa hiyo mali ni mbaya. Na hiki ndicho chanzo cha mivutano na kilio miongoni mwa jamii. Mkangi alitumia jazanda hii ya mkunazi akiwa na lengo la kuwazindua wasomaji wake ili wapiganie ukombozi na hata kuleta mabadiliko katika jamii yao. Haya ni kwa mujibu wa Nadharia Amali inayohusu umuhimu wa kitu katika kuangalia kazi au matokeo ya kitu hicho.

Kwa upande mwingine mwenye mkunazi ni jazanda inayomaanisha mmiliki wa rasilmali au nyenzo hizi kuu za kuzalisha mali. Aidha, mwenye mkunazi katika muktadha wa riwaya ya *Mafuta* anawakilisha wale wenye vyeo, viongozi na watawala na wanaomiliki njia za uzalishaji mali, wanaowanyonya walio wanyonge na kuwanyanyasa. Hali hii inajidhihirisha zaidi kwenye jamii ambazo zina matabaka. Matabaka yaliyomo katika jamii ya *Mafuta* yametokana na ugavi mbaya na umilikaji wa rasilmali. Kuna wachache ambao wanamiliki takribani njia zote za kuzalishia mali. Mwenye mkunazi anawakilisha tabaka hili.

Hebu tuangalie baadhi ya mbinu zinazotumiwa na watawala ili kuhalalisha ugwiji wao na nafasi zao katika jamii. Kwanza, wanawadanganya raia kwa kutumia kasumba maluwaza mbalimbali kama hii ya ' mafuta' (kur.8-9). Wao wametumia uwongo ili waonekane kuwa kweli, wao ndio wanaohitaji na kustahili kuwa na hiyo mali. Fikra za mwenye mkunazi pale Jali anapoandamwa kuwa ni mwizi zaonyesha haya yote:

> Hali mayowe ya ''mwizi huyo'' yalikuwa yangali yakimjia, yule mwenye mkunazi alisimama pale shinani na tabasamu usoni akijua kuwa vita vya wakosa

> kunazi havikuelekezwa kwake. Kwamba mafungu ya kunazi yalikuwa hayako tena baada ya umati kuondoka, havikumuudhi sana akijua kuwa hiyo ilikuwa gharama ndogo kulipa kuzuia malofa kufichua njama hii. Alicheka kindanindani upepo ulipovuma upande wake na kusikia mayowe ya ‘‘mwizi huyo…’’ bado yakimjia. ‘Mungu akunyime yote, lakini akunyimapo akili, basi hataki uwe tofauti na mnyama aliyekufa, akajisemea.’’ (kur. 5-6).

Kwa hili tukio, ni dhahiri shahiri kuwa wananchi wamechanganyikiwa, wamedanganywa na kuukubali uwongo wa wale wanaomiliki njia kuu za kuzalisha mali. Kadiri ‘kina yakhe’ watakavyoendelea kufunikwa na wingu hili la ujinga, ndivyo watakavyoendelea kunyonywa na kunyanyaswa.

Waama huu ndio msingi wa nguvu na uwezo wa tabaka la juu linalowakilishwa na jazanda ya mwenye mkunazi. Linajidumisha kwa kutumia uwongo. Mbinu kuu ya kueneza huu uwongo ni kwa kueneza fikra kuwa wale walio na ‘mafuta’ tu ndio wanaostahili kuwa wateule (kumiliki mali mzomzo).

Njia nyingine inayoliwezesha tabaka la juu (la wateule) kujidumisha ni kupitia kwa nguvu na vitisho. Mfano mzuri hapa ni pale Matope anapogundua ukweli wa mambo na kuamua kuupigania (kur. 33, 41, 80-89). Haichukui muda kwake kutiwa mbaroni na kufikishwa mahakamani. Pale mahakamani anasema ukweli kuhusu hali ya jamii yake. Anawaambia wenye uwezo jinsi wanavyotumia uwongo ili kuwanyonya na kuwanyanyasa wasio na uwezo (kur. 40-41). Huu ukweli unamchongea kwani anapigwa, anatukanwa na hata kutemewa makohozi (kur. 40-41). Mwishowe anatupwa korokoroni. Mtue naye hakuepuka hukumu kama hii pia. Yeye alijichongea kwa kujaribu kupigania ukweli hata ingawa alitokana na tabaka la wateule.

Hizi ndizo njia ambazo kwazo tabaka la wateule linafaulu kujilimbikizia mali maridhawa huku likiacha wanyonge katika uchochole usioelezeka. Wateule wanaogelea katika makasiri, magari na anasa nyinginezo zilizokithiri. Mwenye mkunazi na akina Dubwana, Dubwasha, Bwagu na Bwaguzi ni wachache mno ukiwalinganisha na wasiokuwa na mtaji wa kuwakimu.

Mkangi alitumia jazanda ya mkunazi na mwenye mkunazi akiwa na lengo la kuwazindua wajamii ili kuona kuwa ukombozi unahitajika na hivyo upiganiwe. Kulingana na Mkangi sababu za kupigania ukombozi huu ni nyingi. Kwanza, walio wengi wanataka ukweli utawale wala si uwongo. Pili, suala la matabaka sharti kutafutiwa ufumbuzi mwafaka ili kusiendelee

kuwako na unyonyaji. Mateso, unyonyaji, ubaguzi na kuonewa wanakofanyiwa adinasi wa tabaka la chini hakustahili kuendelea kuwako katika jamii. Haya ndiyo masuala yanayohitaji kutafutiwa jawabu ili kuwepo na utulivu na amani ya kweli.

Maandishi aliyoandika Jali kabla ya vurumai la pale mkunazini na ambayo ndiyo hadithi ya *Mafuta* inayosomwa na akina Zuka na Kazamoyo ni mfano mwingine mwafaka unaoyesha kuchoshwa kwake na hali ya jamii yake. Haya maandishi yanakuwa hazina kubwa inayowazindua wanajamii na kuwafanya wapiganie haki na usawa wao. Hata kama Jali aliuawa au angeuawa, bado angekuwa amewacha cheche za kufumbua macho ya waliolala usingizi wa mavune.

**3.3 Istiari**

Mkangi alitumia istiari pia ili kuipa lugha yake makali ya kuwasilisha aliyonayo. Istiari ni mbinu ya lugha ambapo tabia za watu au vitu viwili hulinganishwa kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Levinson (1988: 12) anasema hivi kuhusu uchaguzi bora wa lugha:

> ‘‘Nadharia Amali huchunguza uwezo wa watumizi wa lugha kuhusisha sentensi na miktadha ambamo zinafaa.’’

Wazo hili la kinadharia ni muhimu katika kutuongoza kuona anayosema Mkangi, anapoyasema na muktadha uliomzunguka. Ina maana kwamba mtumiaji wa lugha huchagua lugha inayofaa muktadha fulani na huko kunategemea iwapo hiyo lugha inafaulisha lengo lake.

Kwake Crystal (1987: 120) Nadharia Amali huchunguza sababu zinazotawala uchaguzi wetu wa lugha katika mitagusano ya kijamii na athari ya uchaguzi huo kwa wengine. Kwa kweli kwenye sehemu hii tumechunguza lugha ya istiari aliyotumia Mkangi na athari za matumizi ya lugha hiyo kwa hadhira ambayo ni wahusika na wasomaji. Waama lugha ni kifaa kinachotumiwa na wasanii kutekeleza yale wanayotaka yatekelezwe katika jamii. Lugha wanayotumia wasanii yaweza kutofautiana toka kwa msanii mmoja hadi kwa mwingine na hivyo kutofautisha msanii mmoja na mwingine.

**3.3.1 Mbuni**

Mkutano wake Mtue na Matope unamfunulia ukweli unaouma; hali mbaya ya wanyonge inamsikitisha. Matope kalala matopeni, ngozi yake imesinyaa na amekonga kama buda aliyekula chumvi nyingi. Kumbe sivyo: Matope ana umri wa miaka ishirini na mitano tu ilhali

yeye Mtue ana umri wa miaka thalathini na mmoja (kur. 9-10). Mzee ndiye anayeonekana kijana na kijana anaonekana mzee. Ukweli huu unamduwaza Mtue. Kisa na mkasa wa haya yote ni uteule wa ‘mafuta’, kunyonywa na kunyimwa haki, kubaguliwa na kudhulumiwa kwa wanyonge na tabaka tawala na wenye navyo. Ugunduzi huu unampa Mtue ghera na hamasa ya kupekua zaidi jamii yake.

Katika pitapita zake za kutaka kujua hali ya jamii yake, Mtue anakutana na Ti. Hili linakuwa kama jaribio kwake. Anaamua kufanya urafiki na Ti, akiwa na nia ya kupata msimamo wake Ti kuhusu hali ya jamii yao (uk. 13). Ili kufikia lengo lake, Mtue, alitaka kujua kutoka kwa Ti kuwa, mbona mtu kukilalia kitanda lazima awe amejipaka mafuta. Anaendelea kumwuliza kuwa ikiwa ni hivyo, ni kwa nini wachache tu ndio wanao uwezo wa kuyapata. Ti anaonyesha msimamo wake kwa kumjibu kuwa, ili kukilalia kitanda lazima mtu awe mteule. Anaendelea kumweleza kuwa mteule ni bahati na hivyo wasio wateule ni bahati yao mbaya. Anamalizia kwa kumtahadharisha kuwa, asijiingize kwa mambo ambayo hatayaweza kwani, hataweza kuondoa uteule katika jamii. Anaendelea kumhimiza kujistarehesha kwa sababu ana bahati hiyo ya kuwa mteule na asisumbukie ya wasiokuwa wateule.  Kwa kulipinga wazo la Ti kwamba mtu ajipumbaze tu kwa kujistarehesha bila kujali yamzungukayo, Mtue anatumia istiari kwa kumwambia Ti kuwa:

> ‘‘kweli nakubaliana nawe. Lakini wasaa mtu hapasi kujifanya mbuni. Kujistarehesha; napenda sana, ama nisingalikuwa nimekunyemelea. Ama sivyo? Huku akisema hivi, Mtue alijisongeza kwake na akamvuta taratibu.’’(uk. 13).

Istiari anayotumia Mtue kumjibu Ti katika dondoo hili ni: ‘wasaa mtu hapasi kujifanya mbuni.’ Mtue anatumia hii istiari ya ‘kutojifanya mbuni’ kupinga wazo lake Ti la kukaa tu kama mjinga bila kujali hali ya wengine katika jamii. Mtue anachukizwa na hali ya matabaka kuwepo katika jamii. Hapendi hali ambapo wachache wanamiliki na kuhodhi mali nyingi ambayo wengi wanaihitaji lakini hawapati; wananyimwa.  Istiari anayotumia Mtue hapo juu inaonyesha chuki aliyonayo pamoja na maneno yake yafuatayo:

> ‘‘Kiniudhicho ni ile kanuni yake tu basi… kweli inamlazimu mtu kuwa amepakwa mafuta kwanza kabla ya kukilalia kitanda? Na vipi wale ambao hawana? Kwani nao si watu? … mbona ubaguzi namna hii?’’ (uk.8).

Mtue haridhiki na hali ambapo baadhi ya watu katika jamii wananyimwa kilicho chao wote. Huko ni kunyimwa haki na ni dhuluma inayoleta ubaguzi unaoumiza. Kwake basi hali hii mbaya inayoikumba jamii yake sharti irekebishwe. Hapo ndipo wanapotofutiana na Ti. Mtue yeye haridhiki kwa hali iliyopo wala hayuko tayari kubaki akitazama kama atazamaye sinema tu (uk. 13). Anakana kwa kutumia istiari tuliyotaja hapa juu.

Kwa upande wake Ti, yeye amekubali hali ya jamii iliyopo (matabaka) na haoni haja ya kurekebisha wala hadhani hilo lawezekana. Hii ndio maana Mtue anapomwomba amsaidie kuondoa hali mbaya iliyopo anamjibu:

> ‘‘Utawezaje kuondoa uteule katika jamii? Wewe ukiwa u mteule, basi u mteule. Wasiokuwa na bahati, hiyo ni bahati yao mbaya. Ya nini kujitakia na mambo hutayaweza?’’ (uk. 13).

Huku ni kushitakia majaaliwa na kujiona kama mtu asiyeweza kujaribu kutatua tatizo lililopo. Ni kukubali hali iliyopo kama ndiyo hali ya maumbile; matakwa ya Mwenyezi Mungu, binadanu ana nini kujaribu kuyageuza. Hapa ndipo Mtue anatumia sitiari hii kiuamilifu akikusudia kumbadilisha Ti. Athari ya sitiari aliyotumia Mtue kwa Ti ni kuwa, Ti ukweli ulianza kumtanzukia kidogo kidogo na hata kumwezesha kuona hali halisi ya jamii yake. Istiari hii ilitumiwa na Mtue kwa nia ya kumwathiri Ti na kumfanya ageuze mtazamo wake kuhusu jamii yake. Hapa mwandishi kupitia kwa istiari hii anatuonyesha Ti kama kiwakilishi cha wateule wachache wanaotanabahi na kuzinduka na kuanza kusaliti maisha yao ya kiubinafsi na kiuanyanyasaji katika jamii. Hili ndilo lilikuwa lengo la Mkangi.

### 3.3.2 Njuzi

Mtue anatueleza hali ya watu wote waliohudhuria kikao cha mahakamani wakingojea hukumu ya Matope itolewe. Anatuambia kuwa wote waliohudhuria kikao cha mahakamani walionekana wakiwa na hofu kubwa yeye akiwa mmoja wao. Anasema:

> ‘‘Mwenzake Ti alikuwa kana kwamba ameketia mwiba. Si shushurushushuru hizo namna ya paka atakaye kuzaa. Ukweli ni kwamba, si Ti peke yake ndiye aliyedhihirisha utwetwe huu. Furukutu za hofu zilihisika zikienea jinsi ya wale waliokuwapo kujitahidi kuzificha. Njuzi alikuwa ameingia nyumba ya kuku. Si ajabu wengi walikuwa wakijijambia na kujikojolea ovyoovyo’’ (uk. 35)

Kutokana na dondoo hili, ni wazi kuwa Matope anapoingia mahakamani anasababisha shushurushushuru kwa kila mteule aliyekuwepo. Hapa ndipo mwandishi anatumia istiari kuwa ni kama 'njuzi alikuwa ameingia nyumba ya kuku.' Kuku wasingeacha kufurukuta kwani adui yao kawaingilia. Hapa mwandishi analinganisha Matope na njuzi. Wateule hawatulii kwani wanajua kuwa Matope atawaambia ukweli na hilo ndilo wanaloogopa. Hivyo yeye ni adui anayeweza 'kuwala' kama njuzi alavyo kuku kwa kutumia ukweli.

Istiari hii imetumika kiuamilifu ili kutuonyesha kuwa viongozi wa tabaka la juu, wana jukumu la kudumisha tabaka lao kwa kuendeleza uwongo kwa kutumia kila njia; iwe vitisho, mahakama au kasumba maluwaza za kisiasa na kiuongozi. Kwa upande mwingine hili linatupa tumaini la kuwa ushindi wa haki na ukweli dhidi ya dhuluma na uongo utapatikana ikiwa wanyonge wote wataungana na kuwaambia wateule ukweli wa yale wanayowafanyia.

Uamilifu wa istiari hii unadhihirika wakati ambapo Matope alipopatiwa fursa ya kujibu mashtaka. Anawatobolea ukweli kwa kuwaambia kuwa, wanyonge wamezaliwa matopeni, wamezaana matopeni, watakufa matopeni na watazikana matopeni. Anaendelea kuwaambia kuwa, wateule wamefanya uongo ukawa ukweli na ukweli ukawa uongo. Aidha, aliwamba kuwa wamepindua sheria za maumbile ili kumamatia enzi yao na kufanya unyama wao kuwa utu na utu wa wanyonge kuwa unyama wao. Alimaliza kwa kuwaambia kuwa, watajikomboa kwa kutumia maji (kur. 40- 41). Mwandishi anasema kuwa baada ya Matope kumaliza kuwaambia ukweli huu macho mekundu yaliwatoka na hasira kuwapanda. Povu ikawatoka vinywani na mishipa kuwasimama kwa kupiga mayowe ya kumlaani Matope (uk. 40). Wateule waliokuwa karibu naye, walianza kumsongelea na huku makucha tayari kumpapura. Kwa upande mwingine, Matope alionekana tuli kama shonde la mavi kung'ong'a kwa nzi hakukumshtua.

Kisa cha wateule kujifurukuta kama kuku njuzi anapoingia katika nyumba yao kinawazindua Ti na Mtue na kuwafanya wajichunguze upya. Wanaamua kujisaka ili wajielewe wao ni nani. Kutoka hapa anapanga safari ndefu iliyojaa ugunduzi mpya. Ti anazinduka na kutambua kuwa amekuwa akiishi maisha ya uwongo. Anakata uhusiano wake na maisha kama hayo na yu tayari kushirikiana na wengine ili kuyakomboa maji. Hili ndilo lililokusudiwa na Mkangi.

### 3.3.3 Ukame

Mwandishi anajaribu kuonyesha hali ya maisha ya wanyonge kukosa mahitaji ya kimsingi kwa kutumia istiari. Anamtumia Mama Fofi ili kueleza hali hii. Anasema:

> ‘‘Marehemu mume wangu alizaliwa katika mazingira ya ukame. Maisha – siyo yake tu – lakini hata kwa jamii yake yote, toka jadi yao, walikuwa watu hohahe. Ukame huu ulionekana ukienea jamii nzima na kurithika kama ufalme. Ikiwa kulikuwa yuko mmoja wao ambaye aliweza kunusurika kutokana na hali hii, basi mimi sijawahi kuambiwa. Hivi ni kusema kwamba mume wangu Sifa, ndiye aliyekuwa wa kwanza kujitoa kutoka hali hii ya kusikitisha’’ (uk. 26).

Katika maelezo haya, Mama Fofi anatumia istiari ‘Ukame huu ulionekana ukienea jamii nzima na kurithika kama ufalme.’ Ukame ni istiari inayoashiria ukosefu wa mahitaji ya kimsingi kwa wanajamii. Anaendelea kulinganisha ukosefu huu na ufalme. Si kwamba ukosefu umependwa kama ufalme upendwavyo bali umekuwa mwingi na usiokwisha kama vile ufalme ulivyo na uwezo mwingi na usivyokwisha kwa haraka. Kwa kushadidia ukweli wa istiari ili kuipa nguvu ya kiuamilifu Mama Fofi anaeleza maisha ya mumewe hivi:

> ‘‘Alizaliwa ngozini…, ya mbuzi ilikuwa nyumba ya nyasi isiyo na madirisha. Mlango huo huo mmoja ndio kila kitu kiliingia na kutoka. Si watu si mifugo. Si mbu si moshi. Si kuku si mainzi. Si uvundo si marashi. Si watoto si watu wazima…’’ (uk.27).

Mwandishi anatumia maelezo haya kiuamilifu ili kuonyesha hali ya unyonge alikozaliwa mumewe Mama Fofi. Mama Fofi anajaribu kuonyesha kuwa mumewe alizaliwa katika umaskini wa hali ya juu sana. Hii ndio sababu hata inambidi kutumia takriri ili kutilia nguvu uchochole huo. Istiari hii ya kufananisha ukosefu na ukame, kwa jumla imetumiwa kiuamilifu ili kuwazindua wanyonge waone taabu wanazopitia ili waanze kutafuta suluhisho kwa matatizo yao. Mkangi analenga kuwazindua wasomaji kuwa, suluhu la tatizo la umaskini ni kupanga mapinduzi ili kumwondoa yule anayewanyang’anya na kuwanyima haki zao.

Istiari hii iliwachochea wanyonge kushirikiana, kuungana na kuwa kitu kimoja. Huu umoja ndio unaoweza kuwasaidia kumudu maisha magumu yanayowakabili. Kwa vile wao ni kama chungu, wanaenda kuhemera pamoja. Ndiyo maana wanakula pamoja (uk. 65), wakipanga mambo yao pamoja na wakiwa na nia moja (uk. 63). Haya yote ni kwa mujibu wa msingi wa Nadharia Amali uanaohusu matokeo ya matumizi ya kitu fulani.

### 3.3.4 Nyoka Mkoko

Mtue akiwa katika hali ya kudadisi ili kujua kina majibaba yaliyokuwa katika jumba lile la wateule, alimgeukia mwenzake, Ti, na kumuuliza amweleze aliyemwona ni nani. Ti

alimwambia kuwa ana bahati sana. Alimkaripia kwa ufedhuli wake. Ti alimweleza Mtue kwa hasira kuwa huyu jibaba alikuwa ni mmojawapo wa watu wale wanne adimu mwote nchini (uk. 17). Baada ya Mtue kujulishwa kuhusu njemba huyu mmoja pale mahakamani, analifananisha na 'nyoka mkoko' (uk. 17). Mtue alitumia sitiari ya kufananisha jibaba hili na nyoka mkoko ili kuonyesha dharau alilonalo kwa wateule na heshima wanazopewa na wateule wenzao. Kitendo cha Mtue kumfananisha mteule yule nyoka mkoko, kilimfanya Ti apandwe na hasira zaidi. Alimwambia Mtue aache dharau zake kwani kazi za wale watwana ni kubwa sana. Kazi yao ni kuona kuwa kila mguu wa kitanda, unahudumiwa barabara. Ili kuonyesha jukumu kubwa la jibaba hili Mtue anaeleza:

> ''Si ukubwa tu, bali ana ubarakarala wa kupindukia. Kwani jukumu lake la kuona mguu wake wa kitanda uko imara na kitanda hakitingishiki au kupwaya au kuwa mregumregu, vimemfanya kuwa mtu wa hasira za haraka zisizohitaji kuchokozwa… Na kwa mtu yeyote kuonyesha ufedhuli wowote aghalabu hunyongwa …; shukuru sana malaika wako,'' Ti akamalizia (uk. 18).

Hata baada ya Mtue kutahadharishwa kutoonyesha madharau kwa mteule huyu kupitia kwa dondoo hili, anazidisha madharau yake kwake kwa kusema kuwa, 'kweli huyu ni nyoka mkoko kweli.' (uk. 18).

Mwandishi alitumia istiari hii kiuamilifu ili kuonyesha kuwa kuna mgogoro kati ya wanyonge na wenye uwezo. Wenye uwezo wanataka kudumisha vyeo na hali yao nzuri huku wanyonge wakipigania haki na usawa. Mvutano huu ndio unaosababisha vita kati ya makundi haya mawili, vita ambavyo vinatujengea kisa. Uhusiano kati ya wahusika wa makundi haya mawili ni wa chuki. Wanyonge wanawachukia wenye uwezo kwani wamewanyang'anya na kuwanyima kilicho chao wote. Wenye uwezo nao hawataki wanyonge wadai kilicho chao, wanataka waendelee kunyamaza na wasemapo ukweli basi huwa wamekosea hivyo wanawachukia. Huu mvutano, kuviziana na kuvurugana ndiko kunakosukuma msuko wa matukio ya riwaya hii mbele. Hali hii imetumika kiuamilifu kutekeleza wajibu wa kukisukuma kisa mbele. Kwa hivyo ingawa wahusika kutoka kila kundi hawashirikiani kwa wema, wanajengana kwani wanafanya kila mmoja kumamatia analopigania katika kundi lake. Ni kama wanaotiliana makali ili washindane waone nani atakayeibuka mshindi – hakuna anayekubali kuwa mshindi hadi kipenga cha mwisho. Mkangi kupitia kwa istiari hii analenga

kuzindua msomaji kuwa, kuna mgogoro baina ya tabaka la matajiri na tabaka la maskini na mgogoro huu unatokana ugavi na umilikaji wa nyenzo za uzalishaji mali.

### 3.4 Namna ufumbaji umeendeleza au kukwamiza usawiri wa wahusika katika *Mafuta*

Mbali na kisa cha hadithi ya riwaya, wahusika ni kiungo muhimu katika riwaya. Marshall (1962:14) anawaita hawa wahusika 'watu'. Kwake, hadithi ya riwaya huhusu watu, wanayoyafanya, wanayofanyiana na yanayotendeka kwao. Ni kweli kwamba aghalabu kutokana na matendo ya wahusika kisa cha riwaya hujisukuma mbele. Wahusika wa kazi ya fasihi hujenga jamii maalum ya hiyo kazi ya fasihi. Hiyo jamii ina mienendo yake, utamaduni wake, maendeleo yake na maisha maalum yanayoihusu. Hii ndiyo maana Marshall akawaita wahusika 'watu'.

Mazrui na Syambo (1992: 72) wanawaeleza wahusika kama binadamu wa hadithini. Hata hivyo wanatahadharisha kuwa binadamu hawa ni tofauti na wale wa ulimwenguni. Maana ya kuwaita wahusika 'binadamu' hapa ni kwamba wao ndio huihuisha hadithi, huifanya jamii ya riwayani kuwa jamii inayoishi kila mara tunapoisoma riwaya hiyo. Kwa kufanya hivi hiyo jamii ina uhai wake na inawasiliana nasi pale tusomapo kazi hiyo ya riwaya. Hii ndiyo maana Mlacha (1985: 33) akasema kwamba maana ya wazo na dhamiri ya msanii hujitokeza riwayani na kupata ukamilifu na uhalisi pale ambapo msanii anatumia vinywa, fikra na matendo ya wahusika. Forster (1993: 30), kama vile marshall, amewaita wahusika 'watu'. Anasema kuwa hawa ni watendaji. Hawa watendaji hutumiwa na mwandishi kuwasilisha aliyonayo.

Waama wataalam wengi (Marshall 1962, Mlacha 1985, Mazrui na Syambo 1992, Forster 1993) wanawatambua wahusika kama viumbe wa hadithini ambao hutumiwa na mwandishi au msanii kufikia malengo yake. Hawa wahusika huchaguliwa na msanii, wakaumbwa na kutumiwa naye kulingana na makusudi yake. Huku kuchaguliwa, kuumbwa na kutumiwa na msanii kulingana na makusudi yake ndio kumetuwezesha kuchunguza namna ufumbaji umeendeleza au kukwamiza usawiri wa wahusika wa riwaya ya *Mafuta.*

Mafumbo ambayo Mkangi ametumia yamemsadia kuumba wahusika kwa kuwapa majina ya majazi. Mbinu hii imewawezesha wasomaji kuwafahamu wahusika wa riwaya ya *Mafuta* kwa haraka na kuwakumbuka kwa muda mrefu. Mafumbo yamemwezesha kumpa mhusika sifa moja kubwa sana ili ajitokeze kwa haraka na hivyo kufahamika kwa urahisi. Forster (1993:47) anaiona hii kama njia rahisi ya kuwatambua wahusika wa fasihi. Ama mhusika

aweza kujitokeza kwa sura ambayo inamfanya akumbukwe kila wakati. Mkangi alizingatia mawazo ya Mazrui na Syombo (1992: 73) kuwa wahusika rahisi kufahamika ni wale wanaotiwa katika fungu la ubaya au uzuri bila ya taabu. Kupitia kwa mafumbo Mkangi ameweza kuwaweka wahusika wake katika makundi haya mawili. Mkangi ameweza kuwapa wahusika majina ambayo yana maana pana kulingana na mazingira anamowatumia na jinsi wanavyotenda. Kinadharia amali twaweza kusema mwandishi ameyachagua haya majina kutokana na dafina ya leksia ya lugha kwa makusudi ya kutuwasilishia ujumbe alionao (Crystal 1987: 120). Hebu tuangalie haya majina japo kwa ufupi.

Matope ni jina linalotufahamisha ujumbe mpana lakini kwa njia ya mkato na yenye nguvu nyingi. Ujumbe hufahamika kwa kumhusisha na mazingira anamopatikana. Kwa kawaida 'matope' huhusishwa na uchafu. Wale wafanyao kazi za sulubu na za shambani ndio huchafuliwa kwa matope. Mwandishi ametumia hali hii kuonyesha unyonge, ukosefu, kutojiweza na umaskini. Hizi hali ndizo anazoziwakilisha Matope kwa njia ya mafumbo. Mwili wake mzima ni matope. Hata nywele zake ni vichuguu vya matope tu.

Bwagu na Bwaguzi, wawa hawa ndio tena Dubwana na Dubwasha, ni majina ya jumla yanayowakilisha kundi la wenye uwezo katika riwaya hii. Yalivyotumika na mwandishi yanajitokeza kuwa na maana pana zaidi kuliko jina la mtu tu. Hebu tuyaangalie majina ya kwanza mawili - Bwagu na Bwaguzi. Tukiyaangalia kwa jicho la ndani zaidi tunaona kama mwandishi amechezea maneno 'pwagu' na 'pwaguzi' tu. Kupitia kwa majina haya mwandishi ameweza kutufahamisha kuwa, wenye uwezo ni waongo, wezi, wanyang'anyi, watu wenye hila na wanaopigania masilahi yao ya kibinafsi. Mafumbo aliyotumia yalimsaidia mwandishi kuwachora wahusika Dubwana na Dubwasha. Kulingana na ufafanuzi wa sura zao ni watu wenye nyuso zinazometameta kama majongoo, wenye matumbo ya kutondoroka na ya kufura kama walio na mimba nne, macho kama ya bundi na sauti za kukwaruzika kama wanaoshongolewa (kur. 16-17). Hizi sura ni za kutisha na kuchukiza. Kile kitendo cha mijiteule hii cha kubadilishana majina ni fumbo linalomaanisha hila nyingi za kibinafsi wanazotumia kujipatia maslahi yao kibinafsi.

Ingawa mwenye mkunazi hakupewa jina, haya maelezo ya kimafumbo yanatufanya tumjue yeye ni nani. Ni yeye tu ndiye aliye na mkunazi, anayeruhusu kunazi zitundwe, azipangaye mafungu, ayapaye bei (uk. 92). Mkunazi umesimamia rasilmali ya nchi. Iwapo ni mtu mmoja tu ndiye anayeimiliki basi inaonyesha wengi wamekosa haki zao. Wachache wamewanyang'anya walio wengi kilicho chao wote. Na wanafanya kila juhudi ili wale wengi

wasiokuwa na chochote wasigundue kwamba wananyimwa kilicho chao wote. Wanawaajiri kwa malipo duni, wanawaeleza uongo kuhusu mali ya nchi na kutumia nguvu na vitisho. Kutokana na fumbo hili tunatambua mwenye mkunazi kama wale wanaomiliki njia za uzalishaji mali.

Mwandishi alimweka mhusika Zuka mwanzoni kiuamilifu ili aweze kuzua suala litakalofuatiliwa. Hili ni fumbo kwani msomaji anahitajika kutafakari ili kutambua sababu za kuwekwa mwanzoni. Yeye ndiye anayezuka na wazo la kuyakusanya makaratasi aliyoacha Jali na yaliyokuwa yanapeperushwa na upepo (uk. 7). Huu uzushi unakuwa na faida kwa wahusika wote na kwa wasomaji kwani hayo makaratasi ndiyo dafina ya hadithi ya 'mafuta'. Baada ya kusoma hadithi hii, ni Zuka ndiye anayezua wazo la kumtafuta mwandishi, Jali (uk. 90). Kumpata kungewasidia kujua alichomaanisha na dhamiri yake. Na ni yeye Zuka ndiye anayekuja na wazo la kwenda kumuuliza mwenye mkunazi maswali kuhusu umilikaji wa mkunazi na mwizi halisi ni nani – naye aambiwe ukweli (uk. 92). Mwandishi amemchora Zuka kama mzushi na kimbelembele. Uzushi wake Zuka umetumiwa kiuamilifu ili kuwa ndiyo asili ya hadithi ya 'mafuta'.

Mwandishi amemsawiri mhusika Kazamoyo akiwa na maana nzito ambayo inaweza kutambulika tu kutokana na vitendo vyake. Alimtumia kiuamilifu ili kutupa ujumbe kwamba, kushinda magumu daima lazima kuwa na akili gunduzi na tumaini lisilovia. Hii ndio sababu anatuonyesha Kazamoyo ambaye hafi moyo katika ugumu wanaokumbana nao. Hafi moyo wanapocheza kamari na kufutwa chote walichokuja nacho (kur. 1-5). Anajitahidi akiwa na mwenzake, Zuka, kulipa madeni ili kuendeleza mchezo wao wa kitoto. Wanaposoma hadithi ya 'mafuta', hafi moyo ingawa ni ngumu kueleweka. Hata wanapoanza kumtafuta Jali, bado ana tumaini kuwa watampata (uk. 91). Hawampati haraka na hata kisa kinapomalizika bado hawajampata. Kwa jinsi hii, ametumiwa kimafumbo ili kuonyesha kuwa yeye ni mhusika aliye na matumaini.

Mwandishi amemtumia mhusika Jali kiuamilifu ili kuwasilisha ujumbe kuwa, inafaa kujali maslahi ya watu wote katika jamii kimafumbo. Jali anawajali wananchi wenzake wanaonyanyaswa na ndiposa akaandika hadithi ya 'mafuta' na kuwaachia wasome ili iwazindue wapiganie haki yao. Ni mhusika aliye na mwamko wa kisiasa na kijamii na anayeelewa jamii yake ilivyo. Anawafahamisha wengine kuhusu hali ya jamii yao kupitia kwa hadithi aliyoandika na kuwaachia. Yeye ana utu na anapenda kuleta mabadiliko mema katika jamii yake. Jali anawakilisha Mkangi ambaye aliandika riwaya ya *Mafuta* na kuwachia

wasomaji wake akiwa na lengo la kuwazindua kuhusu dhuluma za uwatala wa Kenya dhidi ya watawaliwa.

Lugha ya ufumbaji waliyopewa wahusika inawawezesha kushika nadhari ya wasikilizaji au wasomaji na hivyo kuwafanya waendelee kushiriki kwenye msuko wa matukio. Kwa kupewa lugha ya mafumbo, wahusika wa riwaya hii wanatufikia kama watu wanaomiliki utamaduni wa jamii yao hasa kuhusu kipengele cha fasihi simulizi. Hii lugha ya mafumbo inawawezesha kuwasilisha ujumbe wa mwandishi kwa njia ya mkato na iliyojaa hisia. Takribani kila mhusika anajua wajibu wake na lugha inayofaa wajibu huo. Hivyo Matope hahitaji kujieleza kwa mapana na marefu ila kujitokeza mbele ya wadhalimu wake, kuwaacha wamtazame na kisha kutamka maneno machache na hivyo anakamilisha kisa chake kirefu ambacho kingemchukua muda mrefu kukieleza. Inapolazimu wahusika wengine wametumia hata ngano na hata hadithi kutueleza waliyo nayo. Hii ni aina mojawapo ya mbinu ya kutumia mafumbo katika kusawiri wahusika wa riwaya. Mbeyu anatoa hadithi ya wazazi waliotajirika kutokana na kazi ya kuwanyanyasa wangine (kur. 66-70). Gweni anatoa ngano kuhusu mfalme mwenye ubinafsi uliokithiri (kur.70-75) unaomtumbukiza katika aibu isiyotajika. Naye Jasho anahadithia juu ya Chui na Nyani na vita (kur. 78-79). Hadithi hizo zote zinarejelea wazo la uongo unaotumiwa na watawala na wenye uwezo. Mbali na kutumia uongo kuwanyanyasa wanyonge, huo huo uongo uwapofusha macho na kuwafanya wajinga (watawala). Kupitia kwa mbinu hii ya mafumbo wahusika wamesawiriwa kama wanaomiliki dafina hii ya fasihi simulizi ambayo inatumiwa kuzindua wanajamii wengine waliolala.

Kwa jumla, lugha waliyopewa wahusika katika riwaya hii imejaa uzito wa yale waliyo nayo na kusema. Mara kadhaa wahusika wanatumia methali ili kutilia nguvu na mkazo yale wayasemayo. Mama Fofi anapoeleza alikotoka mumewe anasema: ‘‘utokako hakujui na uendapo pia’’ (uk.27). Amebadilisha methali isemayo ‘ mtu hajui atokako, hajui aendako’, lakini bado makali ya methali hii yanahisika. Sababu ya Mama Fofi kutumia mawazo ya methali hii ni kutilia mkazo wazo kwamba yeye pamoja na mumewe walikuwa wametoka mbali na wametia juhudi ili kuweza kuingia uteuleni. Naye Dubwana akielezea usaliti wa Ti anasema ‘‘kweli kikulacho’’ … (uk. 45). Ingawa haikamilishi methali, ametufahamisha ukweli wa ‘‘kikulacho ki nguoni mwako.’’ Ti alikuwa mmoja wao (mteule). Kwake kuwaunga mkono wanyonge kwa kuchekelea Dubwana ni usaliti usiofichika. Na hapo anakuwa kunguni anayeuma kutoka ndani si kutoka nje.

Baada ya kupoteza tumaini la kuingia uteuleni, Mama Fofi anapoteza tumaini la kuishi. Katika kujaribu kumtuliza mwenzie, Mama Shibe anamwambia, 'mwiba na mwiba haichomani' (uk. 46). Shibe ametumia hii methali kumweleza mwenzake kwamba maadam wanajuana na alikuwa amejitahidi hata akakaribia uteuleni, asiwe na shaka kwani sheria za uteuleni zaweza kupindwapindwa ili kumfaa yeye. Na ndiposa baada ya kuambiwa hivyo: ''sura ya mwenzake (Fofi) ilionekana ikianza kutanduka kwa imani ya furaha'' (uk. 46).

Ti anapokuwa kwa Msati, chakula kinacholetwa ni kidogo mno kuwatosha wote waliopo. Ni masikitiko tu. Ili kusisitiza uhaba huu msimuliaji anasema: '' lakini kifo cha wengi ni harusi'' (uk. 65). Kwa kweli haya ni mawazo yanayopita akilini mwa Ti kwani alipoona chakula kinaletwa alifurahi kwani alikuwa na njaa. Lakini chakula chenyewe ni kidogo mno. Methali hii basi imetumiwa kujipa moyo kuwa kuumia kwa wengi ni kama furaha.

Matumizi ya methali huchangia zaidi katika kuunda lugha ya mafumbo. Aghalabu methali zinapotumiwa katika maongezi huipa lugha uhai na mvuto wa kihisia. Hili ni kama pambo la lugha isiwe tu chombo cha kuwasilisha mawazo kwa njia kavu kavu bali kiwe chombo kilicho na urembo unaovutia na unaotamanika. Kwa njia hii huwa kama kitu kinachoishi. Hivyo mafumbo huongeza uhai wa wahusika wanaotumia lugha hiyo. Wahusika wa riwaya hii wanaonyesha ukwasi katika matumizi ya lugha jinsi hii kama vile utafiti huu umebainisha hapa.

Aidha, katika *Mafuta*, Mkangi ametumia wahusika wengi wanaotafakurisha msomaji kupitia kwa mafumbo. Mwandishi alijua kwamba hii kazi ya kisanaa ingehitaji kuwazindua watu waone upya mambo waliyoyazoea. Ili kulifika lengo hii, wahusika sharti wawe watu waliopevuka kimawazo na wanaouliza maswali yanayozindua. Ndivyo walivyo wahusika katika riwaya hii. Wahusika waliotumiwa ni watu wenye pumzi nyingi za uhai, wenye kujitawala kimawazo, walio na nia na wasiotetereka katika dhamira zao. Hivi vipawa vyote vinawafanya waulize maswali ya kutafakurisha na kumfanya msomaji aone mambo upya. Kwa kufanya hivi basi mwandishi hakufaulu kutunga kazi mwafaka ya kisanaa tu bali pia anagusa wasomaji wake na kuwafanya waiangalie jamii yao upya. Hivi ndivyo mwelekeo wa Nadharia Amali ulivyo. Huangalia matokeo ya matumizi ya kitu fulani. Kitu huangaliwa kuwa na umuhimu tu iwapo kinafaulu kutekeleza jambo fulani. Kwa vile katika *Mafuta* wamefaulu kufikisha ujumbe wa mwandishi basi twaweza pia kudai kwamba mwandishi amefaulu katika kuwasawiri kimafumbo.

### 3.5 Kiishilio

Sehemu hii imebainisha kwamba kuna viwango vitatu vya mafumbo katika riwaya ya *Mafuta*: Taswira, jazanda na istiari. Katika kuyahakiki mafumbo haya, utafiti huu umefafanua jinsi Mkangi anavyoyatumia mafumbo haya ili kuwamulikia wasomaji wake uhalisia wa mambo wakati alipokuwa akiandika riwaya hii. Pia, Mkangi ametumia mafumbo haya kiuamilifu kama kichocheo cha zinduko kwa wasomaji wa *Mafuta* ili wabainikiwe na hali halisi za maisha yao. Lengo la Mkangi la kuandika riwaya ya Mafuta ni kutaka msomaji atambue hali yake na kupata msukumo wa kuleta mapinduzi yatakayowaondoa wadhalimu mamlakani.

Tunapochunguza mafumbo katika riwaya ya *Mafuta*, uhalisia wa mateso ya wanyonge na wafungwa unabainika. Pia harakati zinazoleta mabadiliko na ujenzi wa jamii mpya unamulikwa na mwandishi. Vilevile mapinduzi yanayoletwa na wengi katika jamii yanaonekana yakiwa na nguvu na uwezo wa kuondoa viongozi wenye mfumo wa udhalimu. Aidha, athari za utabaka katika jamii zimefafanuliwa kiuamilifu ili kuwachochea wasomaji katika kupigania usawa katika jamii.

Kwa jumla, Mkangi alitumia mafumbo ambayo kuiamilifu yalilenga kuwamulikia wasomaji wake uhalisia katika maisha yao ili wapiganie mabadiliko yanayoleta haki na usawa katika jamii. Halikadhalika, Mkangi anaonyesha kuathirika na mazingira yake katika kuibusha mafumbo ya *Mafuta*.

Matumizi mazuri ya lugha ya mafumbo katika kuchochea uzindushi kwa wanajamii inalandana na mihimili ya Nadharia ya Amali ambayo huangalia athari ya kitu, matokeo au kazi ya kitu hicho. Kulingana na Leech (1967), fasihi haiwezi kuangaliwa kwa undani bila kuzingatia matumizi ya lugha.

Aidha, katika sehemu hii tumechunguza  namna ufumbaji umeendeleza au kukwamiza usawiri wa wahusika katika *Mafuta.* Tumebaini kuwa mafumbo aliyotumia Mkangi yalimsaidia kufaulu katika kuwasawiri wahusika wake. Kwanza, mafumbo yalimsaidia katika kuwapa wahusika wake majina. Majina aliyowapa wahusika yalikuwa na maana pana zaidi kuliko yalivyotamkika tu. Pili, lugha ya mafumbo aliyowapa imewawezesha kushika nadhari ya wasikilizaji au wasomaji na hivyo kuwafanya waendelee kushiriki kwenye msuko wa matukio. Pia, lugha hii ya mafumbo imewasaidia kuwasilisha ujumbe kwa njia ya mkato na iliyojaa hisia na hivyo kuwazindua wale waliolala.

Katika sura ya nne utafiti huu utachanganua na kubainisha vile mafumbo yalivyotumiwa katika riwaya ya *Walenisi* kama kichocheo cha zinduko.

# SURA YA NNE

# MATUMIZI YA MAFUMBO KAMA KICHOCHEO CHA ZINDUKO KATIKA RIWAYA YA *WALENISI*

## 4.0 Utangulizi

Riwaya ya *Walenisi* inashughulikia maswala nyeti yaliyokumba jamii ya mwandishi wakati wake. Katika kutekeleza jukumu la kumzindua msomaji, Mkangi ameuwasilisha ujumbe wake kwa njia ya kiuamilifu kutokana na jinsi anavyotumia mafumbo yanayotokana na mazingira yake.

## 4.1 Taswira

Taswira ni picha inayomjia msomaji akilini anaposoma kazi ya sanaa kwa kufananisha hali halisi ya maisha (Wamitila, 2004).

### 4.1.1 Mwanamke

Suala la nafasi ya mwanamke limechukua nafasi kubwa katika riwaya ya *Walenisi*. Suala hili haliwezi kuangaliwa vyema bila ya kuchunguza kuwako kwa jamii mbili tofauti. Kwanza, kuna jamii iliyotangulia ile ya Walenisi. Jamii ya Waleni au Wachuna. Kitabia jamii hii inafanana na jamii ya Dzombo. Kwa upande wa pili kuna jamii huru ya Walenisi. Hii ni jamii ambayo imekombolewa na mwanamke. Katika jamii hii mwanamke ni kiumbe huru ambaye anatoa mchango sawa na mwanaume.

Mkangi ametumia mbinu ya ukinzano kuibua taswira mbili kinzani za mwanamke wakati wa utawala wa Wachuna ambao ni sawa na jamii ya Dzombo na taswira za mwanamke huru wa Walenisi. Taswira mbili kinzani zinalenga kuwachochea wanawake kujikomboa na kujiweka mkabala mmoja na wanawake huru wa Walenisi.

Wanawake katika jamii ya Dzombo na wakati wa utawala wa kichuna wanasawiriwa kama viumbe duni, ambao wanatumiwa kama vyombo vya kuzindua ashiki za wanaume. Mwandishi anaeleza kwamba wanawake walikosa mamlaka ya maamuzi. Walinyimwa nafasi za kushiriki katika maendeleo ya nchi, hawakupewa nafasi za uongozi. Pia walilazimishwa kumeza dawa za kila aina za kupanga uzazi (uk. 123).

Taswira inayoibuliwa na maelezo haya ya mwandishi ni ya mwanamke ambaye ni kama sanamu. Hana uhuru wa kujiamulia lolote lile. Ni dhaifu na ambaye hana busara yoyote ya

uongozi. Mwandishi anaendelea kusema kwamba wakati wa Wachuna, mwanamke hakuchukuliwa kama binadamu bali kama chombo cha kumfariji mwanaume. Ikiwa aliambiwa azae basi alizaa kama mtambo. Alipoambiwa asizae basi ndipo hapo taabu za tembe, sindano na vijiti vilipogunduliwa. Wengi walifanywa tasa kwa mifereji yao ya mayai ya uzazi kukatwa na kutiwa vitanzi (uk.123).

Taswira ya mwanamke inayoibushwa kutokana na maelezo haya ni kiumbe ambaye anaamriwa kama mtambo mtu. Hana uhuru wa kupanga mambo yake. Ni taswira inayoashiria jukumu la mwanamke alilotengewa na jamii ambayo haizingatii usawa wa kijinsia. Lengo la Mkangi lilikuwa ni kuhamasisha jamii kuhusu jukumu la upangaji uzazi. Jukumu hili halipaswi kutengewa mwanamke pekee, bali ni wajibu wa wawili (mke na mume) kuamua namna ya kupanga uzazi.

Tofauti za kijinsia zinazidishwa na Dzombo anapowaeleza wenyeji wake kuwa huko kwao Duniani, wanawake waliowahi kupewa nafasi za uongozi walikuwa ni wale waliomiliki viwanda vyao wenyewe. Anasema:

> ‘‘huko kungekuwa ni wanaume tu peke yao. Kukiwa na mwanamke, basi huyo labda ndiye mwajiri – lakini hata huyu ni nadra sana. Kwa kawaida, mwanamke akiweko, huwa kama kielelezo tu wala hatazamiwi sana kutoa mawazo au mawaidha yoyote. Akiweko, lake ni kunakili yanayojadiliwa na baadaye kuwaandalia chai waume’’ (uk. 142).

Uchache wa wanawake katika uongozi ni fumbo linaloashiria binadamu asiye na usemi wowote katika jamii. Mwanamke anapaswa kunyamaza, kunakili yanayosemwa katika mkutano bila maswali na baadaye anasukumiwa jikoni ambapo anahitajika kuwaandalia wanaume chai. Hii ni taswira ya mwanamke ambaye ni kama kiumbe anayekosa busara na hekima.

Hali hii ya mgogoro wa kitabaka inayotokana na tofauti za kijinsia inawakilishwa vizuri kwa taswira zinazoibushwa kupitia mazungumzo ya kindoto kati ya Dzombo na mkewe Hani. Katika mazungumzo hayo, kuna urudiaji wa kauli kadha ambazo zinasisitiza mtazamo hasi wa jamii kumhusu mwanamke. Urudiaji huu unaifanya hali hiyo ijitokeze waziwazi na kwa njia inayoeleweka vizuri. Dzombo akiwa katika ndoto anamsikia mkewe Hani akimsuta:

> ‘‘… Nyinyi waume, tuna nini? Kwenu, mwanamke ni, embe lililoiva: ukishalila, huwa ni koko ya kutupiliwa mbali. Kwenu, mwanamke ni ndizi: ukishaila, huwa ni

> ganda la kutupiliwa jaani. Kwenu, mwanamke ni hindi: ukishalitafuna, huwa ni gunzi. Kwenu, wake ni maua: mkishaufyonza, huwa ni ganda la chungu. Kwenu nyinyi, mwanamke ni nanasi: shinani kutamu, nchani kakasi. Kwenu, mke ni dau: likishavusha ni gogo kwenu nyinyi, wanawake ni samaki, kuwala mwataka, harufu hamtaki. Kwenu mwanamke ni 'nywele', 'macho', 'uso', 'masikio', 'pua', 'midomo', 'matiti', 'kiuno', 'nyonga', 'mapaja', 'miguu' – lakini katu si mtu. Alimaliza kwa kufoka, wanaume, hamna hata chembe ya utu. '' (kur. 135-136).

Mwanamke analinganishwa na embe ambalo ni tamu kulika, lakini mwishowe linabaki koko la kutupiliwa mbali ule utamu ukiisha. Pia anafananishwa na ndizi ambayo ganda lake hutupiliwa mbali, halina utamu na hakuna anayelila. Mwanamke pia ni sawa na muwa ambao ukifyonzwa utamu wake, ganda lake hutupiwa chungu. Aidha, amefananishwa na nanasi ambalo ni tamu shinani lakini nchani kakasi hakuna anayetaka kula kipande cha nchani. Mwanamke pia analinganishwa na samaki ambaye ingawa ni mtamu, harufu yake huchukiwa. Dau ni chombo cha majini ambacho hutumiwa kuvushia watu majini. Mwanamke analinganishwa na dau ujanani lakini uzeeni ni gogo ambalo ni bovu. Mwandishi amejenga taswira ya mwanamke kiuamilifu kwa kumlinganisha na takataka na vifaa ambavyo havina umuhimu wowote maishani. Taswira hii inaashiria kutothaminiwa kwake mwanamke katika jamii ya kiubabedume. Tukizingatia msingi wa Nadharia Amali unaohusu matumizi ya kitu fulani ili kupata umuhimu wake, mwandishi alitumia taswira hii ili kuwachochea wanawake wazinduke na kuanza kupigania ukombozi wao. Taswira hii inamjia msomaji hasa mwanamke, ikiwa na athari kubwa mno kwake. Mkangi analenga kuwahamasisha wanawake kuhusu madhila wanayotendewa na wanaume.

Mwanamke amechorwa kama malaya. Katika kikao cha walevi kwa mzee Matingazi, mwanaume mlevi anamwita mwanamke malaya. Anasema:

> ''Mwanamke, hee, mimi siwezi kumnunulia mwanamke pombe. 'Kwa nini?' Mwenzake akamwuliza. Kabla ya kujibu, kwanza akateuka, na huku akiwatupia macho ya dharau wateja wenzake wa kike, akasema, 'wote ni Malaya tu.' Kisha akateuka 'gee', huku akiyumbayumba kutoka shingoni.'' (uk.92).

Malaya ni mwanamke ambaye hana heshima kwa mwili wake na anashiriki katika vitendo vya ngono na kila mwanaume. Hii ni taswira ya kuonyesha migogoro iliyopo kati ya jamii ambapo mwanamke ni kiumbe asiye na uhuru wa kutangamana na wanaume katika vyumba

vya starehe, kwani akifanya hivyo huonekana kama malaya. Lengo la mwandishi katika kuibusha taswira inayomlinganisha mwanamke na takataka, malaya na vifaa ambavyo havina umuhimu maishani ni kumzindua msomaji kwamba, chanzo cha matatizo baina na ya mwanamke na mume ni tofauti za kijinsia. Iwapo tofauti hizi zitatupiliwa mbali, watu wa jinsia zote watakuwa sawa. Aidha, Mkangi anadhamiria kumulika umuhimu wa utu katika jamii. Anaonyesha kuwa, ukosefu wa utu huibusha matatizo ya kutoelewana baina ya mwanamke na mume. Mbinu ya taswira imetumiwa katika muktadha huu kiuamilifu kumzindua msomaji kuhusu umuhimu wa utu na usawa katika jamii. Iwapo jamii itakosa utu, basi tofauti za kitabaka na kijinsia zitakuwepo na migogoro itaendelea kuwapo baina ya matabaka haya mawili.

Hali kadhalika, kulingana na Dzombo, mwanamke duniani anaolewa anapolipiwa mahari. Kulingana na Mkangi, mahari ni kielelezo tosha cha jinsi jamii za kibabedume zinavyomwangalia mwanamke kama chombo kinachoweza kumilikiwa na kuuzwa. Maoni haya yanaunga mkono kauli za Hani mkewe Dzombo. Mahari ni kama bei na huchangia katika dhuluma wanazotendewa wanawake na wanaume waliowalipia bei hizo. Bi. Uvetie akinukuliwa na Gibbe (1978) anaeleza kuwa, itikadi ya ubabedume ilipoanza kumkandamiza mwanamke iliamua kumkaba zaidi huyu mwanamke kwa kumlipia mahari. Taswira inayoibushwa na kitendo cha kumkaba mwanamke inaashiria binadamu anayenyimwa uhuru wa kutenda lolote lile. Bi. Uvetie asema mahari yalimtia mwanamke pingu. Taswira ya mwanamke aliye na pingu au silisili mikononi inaashiria kunyimwa uhuru kwake. Mkangi anatoa wito kwa mwanamke msomaji kutoa pingu hizo kupitia kwa kutupilia mbali itikadi ya ulipaji mahari.

Kwa upande wa pili, Mkangi anatusafirisha hadi Walenisi ambapo anatuchorea taswira ya mwanamke tofauti iliyokinyume na mwanamke Duniani kwa Dzombo. Tunaelezwa kuwa jamii ya Walenisi ilikuwa huru na mwanamke huko alikuwa huru. Mwanamke anatoa mchango sawa na mwanaume. Mama mtu - maanani anasema:

> ‘‘Wakati huu, mwanamke amekuwa sawa na mwanaume; ikiwa basi hakumzidi, kwa kuwa pamoja na maendeleo ya kisayansi, bado ni ndani ya mwanamke ambamo siri ya uhai hutungwa, kuota na kuzaliwa. Mwanamke amekuwa kitovu cha hekima na sisi Walenisi hatukomi kufurahia ukweli huu’’ (uk.123).

Walenisi walizingatia usawa baina ya mwanamke na mume. Dzombo anapokaribishwa katika katika kiwanda cha kutengeneza trimi, anashtuka kuona Mtu-Binti Fikirini ndiye mkurugenzi mkuu na ana watu wengi wake kwa waume wanaofanya kazi chini yake. Mtu-Binti Fikirini ni mwanamke anayeheshimiwa sana. Jina lake ni la kimajazi. Yeye ni mtu anayefikiria si kinyago. Mtu-Binti Fikirini amesawiriwa kuwa na busara na hekima kiasi kwamba anasimamia kiwanda cha usafiri wote katika nchi ya Walenisi. Hali hii inaonyesha kuwa Wawalenisi hawakubaguliwa kijinsia kinyume na hali ilivyokuwa wakati wa Wachuna. Aidha, Dzombo anapopelekwa Mapenzoni ambayo ni Thome kuu ya Walenisi, anapata halmashauri hiyo inaongozwa na mwanamke na zaidi ya hiyo, wanawake ni nusu ya idadi ya wanakamati wa halmashauri hiyo (uk. 198). Idadi hii inamshangaza Dzombo kwa vile huko kwao Duniani, alikuwa amezoea kuona madaraka makuu kama haya yakishikwa na wanaume. Isitoshe, Dzombo anapokwenda kushuhudia kufuzu kwa vijana, anashuhudia idadi sawa ya vijana wa kike na wa kiume kazini. Dzombo haoni ubaguzi. Anashtuka kuona wasichana wakiendesha matingatinga, kuburuta mapipa ya mbolea na wavulana wakiendelea kutengeneza mifereji ya kunyunyizia mimea maji. Kazi hizi za vijana wa kike zinaonyesha taswira ya jamii ambayo haimbagui mwanamke. Hakuna kazi zilizotengewa wanaume na wake Walenisi. Taswira hii ya mwanamke ambaye ni sawa na mwanaume imetumiwa na mwandishi kiuamilifu ili kuwachochea wasomaji wake wanawake katika jamii yenye dhuluma na ubaguzi kwa mwanamke kuzinduka na kupigania usawa na haki katika maisha yao. Anataka kuwahamasisha wanawake kuwa wana uwezo kama wanaume wenzao. Haya ni kulingana na msingi wa Nadharia Amali unaoangalia kazi yoyote ya sanaa. Kazi ya sanaa ina dhima ya kumwelimisha, kumhamasisha, kumburudisha au kumwonya msomaji.

Katika Walenisi kuzaa si tatizo la mwanamke peke yake. Tatizo hili la kuzaa linachukuliwa kama tatizo la wawili waliohusika (uk. 122). Taswira ya ushirikiano wa mke na mume wanapoamua kupata watoto ni kichocheo cha zinduko kwa msomaji. Msomaji anapata mshawasha wa kuazima itikadi ya kiutu ya Walenisi na kuihamisha kwake. Mwandishi anazidisha uzindushi kwa kusema kuwa, jukumu la Walenisi kupata watoto lilikuwa ni la kuwalea kiutu wala halikuwa ni la kuwazaa tu kwa sababu ya starehe zilizoongozwa na ubinafsi. Familia ya Walenisi ni taswira inayomzindua msomaji kuhusu jinsi ya kuwalea watoto kwa kutilia maanani uwajibikaji wa wazazi wote wawili.

Hali kadhalika, wanawake Walenisi wamekombolewa kuhusiana na ulipaji wa mahari. Walenisi walikuwa wametambua udhaifu wa mtazamo finyu unaosababishwa na ulipaji mahari, na ndiyo sababu Mtu-Binti fikirini anamjuza Dzombo kuwa:

> ‘‘Sisi hatuoani kwa mahari. Hatuuzani wala kununuliwa. Hapa Walenisi, sababu ya kwanza ya kuoana, ni kutaka kuendeleza utu, kushuhudia utu na kutekeleza mapenzi ya kiutu. Pili, kutaka kudumisha uhusiano ndani ya jamii kwa kutumia mbinu ya ndoa. Haya ndio masharti mawili muhimu sana, je, unayakubali?’’ (uk.134).

Taswira ya mwanamke huru Walenisi asiyenunuliwa wala kuuzwa kwa mahari inapingana na ya mwanamke anayelipiwa mahari. Hiki ni kichocheo cha zinduko. Mwito wa Mkangi kwa wanawake ni kwamba wanapaswa kutupilia mbali itikadi ya kulipiwa mahari inayowamithilisha na bidhaa. Zinduko la mwanamke linatiliwa nguvu na mwanamke wa Walenisi ambaye ni kiongozi katika Halmashauri ya Mapenzoni, mkurugenzi mkuu katika kiwanda cha trimi na ambaye ana uwezo wa kutoa mchango katika jamii yake. majukumu anayotekeleza yanaibusha taswira ya mwanamke jasiri na anayeheshimiwa katika jamii yake.

Wito wa Mkangi kupitia taswira za ukinzano za mwanamke katika jamii ya Dzombo na jamii ya Walenisi ni kwamba watu wanapaswa kuwa na utu, ili usawa uwepo katika jamii. Jamii ambayo ina misingi ya utabaka na tofauti za kijinsia haiishi migogoro. Lengo la Mkangi ni kuonyesha jinsi ambavyo maisha yangalikuwa mazuri ikiwa watu wote wangaliishi kama Walenisi. Mwandishi anatumia taswira mbili kinzani ambazo zanaibua athari kubwa ya zinduko kwa msomaji kwa kufafanukiwa na hali halisi ya maisha.

### 4.1.2 Vijana

Vijana Walenisi ni kichocheo cha zinduko kwa vijana na wasomaji wengine wa riwaya ya *Walenisi*. Jamii ya Walenisi imejigawa katika marika manne makubwa ambayo yanajulikana kama: rika Dunge (watoto), rika Hirimu (vijana chipukizi), rika Kambi (makamo) na rika vaya (wazee). Kila rika lilikuwa lina jukumu maalumu la kutekeleza kwa jamii nzima. Kila mmoja wa vijana hawa alipata elimu ya kutosha ili kumsaidia Muwalenisi kama anavyosema mwandishi:

> ‘‘Elimu ya huku ililingana na umri wa kila mtu – hasa ikiwa na lengo la kumfunza mkufunzi kuona na kukuza vipawa vyake, kujivumbua kiutu na kumwezesha kuzalisha mali. Kwa hivyo, vitu vitano vya muhimu vilisisitizwa sana katika kila kiwango cha masomo yao. Hivi vilikuwa ni juhudi, nadharia, utafiti, ujuzi na mawaidha… Elimu isiyo na lengo la kumpa mteja uwezo wa kuzalisha mali – hiyo haikuwa elimu, na hivi

> ndivyo wenyewe walivyokuwa wakisema.'' (kur. 109-110).

Aidha, Hirimu-pora lilianzisha utafiti wa hali ya juu katika mradi wowote ambao walikuwa wameamua ili kutumikia taifa. Mwandishi anatueleza kuwa vijana ndio waliochukua jukumu la kulisha jamii nzima kupitia kilimo cha kufa na kupona. Tunaambiwa huko Walenisi, vijana walifanya utafiti juu ya hali ya anga, udongo na magonjwa ya mimea. Matokeo ya utafiti huu yalitumika moja kwa moja na walinyunyuzia maji mimea yao na hawakutegemea mvua inayokuja kwa misimu isiyoaminika. Vijana walijitolea kufanya kazi bila usimamizi wa nyapara au mtu yeyote. Marika yao mbalimbali yalifanyia jamii kazi kulingana na uwezo wao na wakifukuza njaa katika nchi yao. Taswira ya vijana wa kike na wa kiume wenye bidii katika kilimo cha kufa na kupona na bila usimamizi imetumiwa na mwandishi kiuamilifu ili kuchochea zinduko kwa vijana wasomaji wa riwaya ya *Walenisi*. Vijana wasomaji wanahamasishwa kuwa wawe wawajibikaji maishani. Vijana Walenisi walijitolea kutafiti na kutia bidii zao katika kilimo bila kushinikizwa. Kutokana na bidii na kuwajibika kwao kazini matokeo mazuri yanaonekana yanayofaa kufuatwa. Akieleza kuhusu hali kama hii Holman (1936:411), anasema kuwa maana nzima ya wazo huonekana katika matokeo halisi, matokeo ambayo hujitokeza ama kama tabia nzuri za kufuatwa au tajriba inayotarajiwa iwapo hilo wazo ni sahihi. Tunaelezwa:

> ''Mbele yake kulisimama bahari ya shamba. Mawimbi ya masuke na masuke ya wimbi, mtama, mpunga mawele na ngano yalikuwa yakishangilia kwa kutikisa vichwa vyao hewani. Mahindi nayo yalijiandaa kama askari wanaongojea kukaguliwa.'' (uk.113).

Taswira ya mimea inayonawiri vizuri kutokana na bidii na uwajibikaji wa vijana hawa inawakilisha ujumbe wa mwandishi wa mafanikio makubwa. Ukubwa wa mashamba la mimea hii ya asili umelinganishwa na bahari. Ukubwa wa shamba hilo unaashiria bidii na kujitolea kwa vijana Walenisi kutokomeza njaa kabisa. Mwandishi alitumia tashihisi kuchora taswira hii ili kushadidia ujumbe wake.

Isitoshe, mwandishi anatuchorea taswira ya vijana Walenisi waliofurahia sana kazi yao. Walifanya kazi huku wakiimba nyimbo na mashairi yaliyokashifu Uchuna na udhalimu wao. Dzombo alisikia kwa mbali sauti ya vijana wakiimba kazini alipokuwa anazuru miradi yao ya maendeleo. Alisikia sauti ya kike ikihimiza:

> ‘‘Hirimu, bega kwa bega shime; jasho letu ni ngao na shibe.Ujira ni wetu: moyo tusife. Wachuna tuwafunike: shibe tupanue.Vijana tu rasilimali; atukataaye alaaniwe. Vijana tusiwe makapi; kwa Wachuna wanyonyaji. Vjana yu viongozi: si wa kesho – ni wa leo’’ (kur. 112-113).

Wimbo huu unawasawiri vijana hawa kama wazalendo wa nchi yao. Wimbo huu ni kichocheo kikubwa cha uzindushi. Mkangi alilenga kuonyesha kwamba, uzalendo huwasukuma vijana kujihusisha na maendeleo ya nchi kutokana na mapenzi makubwa kwa nchi yao. Aidha, wimbo huu unaonyesha kuwajibika kwa vijana hawa kazini. Nyimbo za vijana Walenisi wakiwa kazini ni za kimapinduzi. Zinaibua hisia za kimapinduzi za vijana ambao wamekataa kuwa makupe na makapi katika jamii. Vijana wamekombolewa kimawazo na wamejitahadharisha kutokana na mifumo inayoendeleza utabaka katika kuzalisha mali.

Kwa upande mwingine mwandishi anatuchorea taswira ya vijana katika jamii ya Dzombo ambao hawana kazi; ni majangili, malofa, malaya na ambao hata wakiwa kazini hawana nidhamu yoyote. Hali hii inaelezwa na kijana Mtu-Wazo anaposema:

> ‘‘Wakati wa enzi ya Wachuna, hakukuwa na uongozi mwema na vijana hawakuwa na faida kubwa kwa jamii isipokuwa kuchukuliwa kama wazushi wa bughudha na kiuchumi, kama vilemea. Wanaume wao nguvu zao ziliishia katika uasherati hali wasichana wao, nguvu zao zikaishia katika umalaya. Hawakupewa fursa ya kuzalisha mali, kwa hivyo basi, wengi wao, walipevuka kuwa majangili, wakora na kumalizikia magerezani na kufia huko.’’ (uk. 107).

Taswira ya vijana inayoibuliwa na dondoo hili ni kinyume kabisa na vijana Walenisi. Inaonyesha mazingira makali waliokulia vijana wakati wa utawala wa Wachuna. Vijana wakati wa Wachuna wanalinganishwa na nzige na makapi kuonyesha kwamba watawala hawakuona faida yoyote inayoweza kuletwa na vijana ndiposa wengi wakaishia magerezani. Hii ni taswira inayomsikitisha msomaji sana. Wakati wa utawala wa Wachuna, vijana waliishia kuuawa kwa kupigwa risasi. Hali hii ndiyo Mkangi anayoiita ‘ moto wa marisau’ (uk. 108).

Taswira ya vijana katika jamii ya Dzombo inafumbatwa vizuri na taswira ya familia ya Dzombo aliyoiacha Duniani kupitia ‘‘kifo’’ chake. Mwandishi anatueleza kwamba akili yake Dzombo siku moja iliruka hadi kwao Duniani, kwa mke wake Hani na watoto wao watano.

Alijua kuwa bila msaada wowote, familia yake ilikuwa ikiteseka pakubwa sana. Mwandishi anasema:

> ‘‘Alijua kuwa bila msaada wowote, basi familia yake pengine ilikuwa ishafukuzwa na bwana mwenye kibanda, kwa kukosa kulipa kodi. Pia, na hicho kijishamba kitapigwa mnada, ili kulipa ule mkopo aliopewa. Aliona mkewe na watoto wakifukuzwa shuleni na kuanguliwa kwenye jua kali. Aliona binti zake Chizi na Umazi wakijitafutia riziki kwa kulazimishwa kupiga umalaya huku wakitokwa na machozi na huzuni zisizoisha mwao rohoni. Alimwona mkewe, Hani akitapatapa kwa kuuza chang’aa na kutembea na walevi wasio na makao. Aliwaona wavulana wake Tsuma, Munga na Chai wakipevuka kuwa wevi, watumishwa, majangili, magaidi, magawadi na wazururaji malofa. Watu ambao miili yao itakuja kuwa chakula cha marisasi ya wenye mali…’’ (uk. 127).

Familia ya Dzombo inazua athari kubwa ya kihisia za huruma kwa msomaji. Kutokana na ukosefu wa kazi na kutoshirikishwa kwa vijana katika maendeleo ya nchi, wengi wa vijana hawa wanaishia kujitumbukisha katika wizi, umalaya, ulofa na matumizi ya dawa za kulevya. Na wengine kutokana na maovu haya, hupatwa na magonjwa ya zinaa kama ukimwi. Chanzo cha ukosefu wa kazi kwa vijana katika jamii ya Dzombo kulitokana na itikadi potovu kwamba, vijana ni viongozi wa kesho sio leo. Kwa hivyo, wangonje kesho yao ifike wapate kazi. Mkangi alitumia taswira hii kiuamilifu akidhamiria kuwazindua wasomaji wake wafahamu kwamba vijana ni kundi muhimu sana katika jamii na lazima wapewe nafasi kutoa mchango wao nchini. Aidha, mwandishi alilenga kupitisha wazo kuwa, baadhi ya maovu na magonjwa yanayowakumba vijana chanzo chake ni ukosefu wa kazi.

Taswira ya vijana Walenisi inalinganishwa na taswira ya vijana kutoka Duniani ambao wengi hawana kazi, na wanangoja tu kuajiriwa katika maofisi na viwanda kumefanywa kiuamilifu ili kuchochea zinduko kwa vijana wasomaji wa riwaya ya *Walenisi*. Msimamo wa Mkangi kupitia taswira nzima ya maendeleo ya vijana kwa njia ya kilimo huko Walenisi ni kwamba, kilimo ni shina la maendeleo katika nchi nyingi barani Afrika, Kenya ikiwemo, ingawa kinadharauliwa na wengi. Mwandishi analenga kuitwaza hadhi ya kilimo ili yeyote aifanyaye kazi hii asijione duni. Kutokana na taswira ya vijana Walenisi, Mkangi anawashauri vijana wajihusishe na kilimo na wakome kulowea mijini wakitafuta kazi ambayo haipatikani.

Vijana Walenisi wamesawiriwa kama wanamapinduzi. Vijana Walenisi walikataa dhuluma na mateso waliyosukumiwa Wachuna kupitia kwa zinduko lao. Hali hii inaelezwa hivi:

> ‘‘Vijana wenyewe hawakugundua kutumiwa kwao vibaya kwa makame. Lakini siku walipozinduka, babee, mbona Wachuna walitafuta pa kujificha na wasipaone… vijana – chipukizi walizinduka kwa kukubali kutorudi nyuma ili wawe magugu ya wengine wachache wenye nguvu.’’ (uk. 108).

Dondoo hili linaonyesha mapinduzi makali yanayoongozwa na vijana Walenisi kutokana na mfumo mbaya wa kisiasa wa Wachuna. Vijana walikataa kuwa makapi na makupe. Taswira hii ya mapenduzi yanayoletwa na vijana Walenisi imetumiwa kiuamilifu ili kuwa kichocheo cha uzindushi kwa vijana wasomaji wa riwaya ya *Walenisi*. Wito wa Mkangi kwa vijana wasomaji ni kwamba wana uwezo wa kubadilisha mfumo wa kisiasa usiowajali na unaowafanya kuamini kuwa wao ni viongozi wa kesho, si wa leo, na hivyo kuwasukuma pembeni kungojea kesho isiyofika. Pia mwandishi anamzindua msomaji kuhusu njia inayopaswa kufuatwa ili kuleta mabadiliko katika maisha yake na jamii kwa jumla.

### 4.1.3 Mapenzoni

Mapenzoni ilikuwa Thome au Baraza kuu kabisa ya Walenisi. Thome yenyewe ilikuwa ni ya watu kumi. Wake watano na wanaume watano kati yao waliwakilisha akina mama na akina baba, vijana wa kike na wa kiume, wakulima na wafanyakazi wa viwandani, miji na mashambani, wataalamu na warasimu. Thome hii ilikutana mara mbili kwa mwaka na kila baada ya miaka mitatu kulichaguliwa wajumbe wapya. Desturi hii haikuwazuia Wawalenisi wenyewe kumwondoa mjumbe yeyote au kuiondoa Thome yote kwa pamoja hata kabla ya kumalizika kwa muda wao (uk. 198).

Maelezo haya ya mwandishi yanaibua taswira ya halmashauri yenye usawa, iliyochaguliwa na watu huru, waliowachagua kiasi kwamba, walikuwa radhi kuiondoa Thome yote mara moja hata kabla ya muda. Taswira hii ya desturi za Mapenzoni ni kichocheo cha zinduko kwa msomaji. Kwanza, Mkangi alitumia taswira hii kiuamilifu ili kumzindua msomaji kuwa haki na usawa ndio nguzo muhimu katika utawala wa nchi. Aidha, alilenga kumzindua msomaji kwamba, sio lazima mjumbe akichaguliwa akae mamlakani pasipo kutekeleza wajibu wake kama kiongozi. Anawazindua wanajamii kwamba, wana uwezo mkubwa wa kumwondoa mjumbe yeyote waliyemchagua wakati wowote bila kungonja amalize kipindi fulani mamlakani ikiwa hatekelezi jukumu lake. Dzombo anajulikana na mzee Mtu-Mwenzio kuwa

mapenzoni ni tofauti kabisa na fyanduzi (serikali) ya enzi ya wachuna. Ukweli huu unaashiriwa na jina lenyewe (mapenzi). Mapenzoni ni chombo ambacho kinazingatia usawa, mapenzi na utu. Aidha, chombo hiki kina majukumu ya kusambaza mapenzi yaliyoko kwenye misingi ya uchumi, utu na ubinadamu, kupongezana na kutiana shime na kuhakikisha kuwa udhalimu haupo (uk. 203). Maelezo haya yanalenga kummulikia msomaji hali ya siasa katika nchi yake ili aone uhalisia uliopo.

Aidha, Mkangi anaibua taswira ya Mapenzoni ambayo inamvutia Msomaji sana. Kupitia maelezo ya mwandishi, Mapenzoni ni jengo kubwa la kiajabu na lenye adhama kubwa. Neno 'Mapenzoni' lilikuwa limeandikwa kwa herufi kubwa za dhahabu. Ndani kulikuwa na ukumbi mpana uliokuwa umetandikwa zulia zito lililokuwa na rangi za kisiki. Mwandishi anasema rangi zote saba na michanganyiko yao mara saba ilifanya ukumbi ule kumetameta. Kwa sababu ya rangi hizi na miale yao, Dzombo aliona sura na mavazi ya mzee Mtu-Mwenzio yaking'ara kwa utukufu wa kipekee na akionekana kama aliyekuwa akielekea hewani badala ya kuvyoga chini. Uzuri wa jengo hili unashadidiwa na kuta za dhahabu, dari la mawingu ya lulu iliyokuwa na nyota za kila rangi zilizokuwa zikikimbizana kwa kasi. Pia, kuta zenyewe zilikuwa na vitundu vidogo ambavyo vilikuwa vikipisha upepo mwororo wa kuburudisha. Kwa sababu hii, chumba chote kikasikika kama kimejaa sauti nyororo za muziki wa kuongoa (uk. 205). Kufikia hapa taswira ya Mapenzoni ya sauti nyororo za kuong'oa inamfanya msomaji kuamini kabisa hapa ni peponi sawa na anavyofikiria Dzombo.

Imani ya dini ya kikristo inatwambia kuwa, mbinguni kutakuwa na sauti nyororo za Malaika wanaoimba wakimsifu Mungu kila wakati. Mwandishi anazidisha taharuki ya jengo hili la ajabu kwa kutuchorea taswira ya Buku kubwa mno. Mwandishi anasema:

> ''Hofu hii ilizidi baada ya kiambaza kimoja mbele yake kilipojifungua kwa urahisi ungedhani ni pazia. Na ni nini alichokiona? Buku. Tena kubwa mno. Tena la dhahabu; lililokuwa limeandikwa kwa wino mwekundu'' (uk.206).

Taswira ya Buku hii inamtia msomaji hisia za wasiwasi na hofu kubwa. Kulingana na mafunzo ya dini matendo yote ya binadamu, mema na mabaya, huandikwa katika Buku la matendo. Matendo hayo, yatasomwa siku ya hukumu. Hisia za msomaji anapoona Buku hili ni kwamba, Dzombo yuko peponi na matendo yake mabaya aliyoyatenda akiwa kwao Jehanamu yako karibu kusomwa. Pia, msomaji anamwona Dzombo kama mwenye dhambi. Buku hili lilikuwa na amri kumi. Zinaposomwa amri hizo, Dzombo hakuamini masikio yake.

Amri hizo zilikuwa kama muziki kwenye masikio yake wakati ambapo alikuwa amekata tamaa. Hakuamini aliposikia sauti za kike na za kiume zikikariri kwa zamu:

> ‘‘Si dhambi: kuwa ulimi wa - mabubu wa uoga. Si dhambi: kuwa macho ya – vipofu wa ufahamu. Si dhambi: kuwa masikio ya – viwizi wa ukweli. Si dhambi: kuwatetea – wanaonyanyaswa. Si dhambi: kulia na – wanyonge. Si dhambi: kuwakinga waliotiwa - mapingu na minyororo. Si dhambi: kujitambulisha na – maskini hohehahe. Si dhambi: kukomesha vilio – vya wateswao magerezani na makorokoroni. Si dhambi: kupigania haki na usawa wa kila binadamu. Nderemo na vigelegele vya kupasua moyo vikajaza jumba.’’ (kur. 208-209).

Amri hizi zimetumiwa kiuamilifu ili kuonyesha kilele cha zinduko kwa Dzombo. Anafahamu kuwa aliyoyatenda ili apate hukumu ya kifo Duniani sio dhambi katu. Alikuwa akipigania usawa na haki kwa kuwazindua wanyonge. Dondoo hili ni kichocheo cha zinduko kwa wasomaji. Mkangi analenga kuwatia wasomaji hisia za ujasiri kwamba, sio dhambi kamwe kutenda vitendo ambavyo vimekaririwa. Lengo hili limelandana na mihimili ya nadharia amali inayohakiki kazi ya sanaa kama kitu kilichoundwa ili kuwa na athari fulani kwa hadhira (athari kama vile kuburudisha, kufunza au kuibua mihemko) na huelekea kupima umuhimu wa kazi kulingana na kufaulu katika kufikia lengo hili. Kilele cha furaha ya Dzombo ni anaposoma maandishi juu ya jalada la buku hilo. Maandishi yalikuwa yakionekana kama vile damu ilivyo inapochuruzika. Aliweza kuyasoma yalipomfikia karibu. Nayo yalikuwa yakisema: ‘‘Lakini haya yote ni madhambi, kwa Wachuna wala watu.’’ (uk. 209).

Maandishi haya na amri kumi kutoka kwa Buku hilo ni kichocheo cha zinduko kwa msomaji kwamba, vitendo vya kuzindua umma mnyonge ni dhambi tu kwa viongozi dhalimu, ambao wanataka wanyonge wazidi kudidimia. Katika kutojua huku, wao wanazidi kuwalaghai na kuwanyonga.

Lengo kuu la Mkangi kuchora taswira ya kuvutia ya mapenzoni ni kupinga itikadi tatu kuu hasa katika jamii nyingi barani Afrika, Kenya ikiwepo. Kwanza, jamii za kiafrika zinaamini kuwa, Mwafrika hana uwezo wa kujenga mijengo ya kuvutia kama Mapenzoni. Pili, maendeleo makubwa aliyoyaona Dzombo Mapenzoni yanapatikana tu mbinguni kwa Mungu. Aidha, wamanaamini kuwa, mzungu peke yake ndiye aliye na akili na weledi wa kujenga mijengo ya ajabu na kufanya maendeleo makubwa lakini sio mwafrika. Hali hii inafumbatwa vizuri na Dzombo anapowaeleza wenyeji wake kwamba:

> ‘‘Nitokako, tunatiwa kasumba ya kuamini kuwa ni watu wachache sana na tena ngozi nyeupe tu peke yake, ndio walio na akili, ilhali sisi wengine, ni kuamriwa tu kama wanyama. Kwa hivyo, hawa ndio viongozi na wataalamu wa kila jambo. Utaona basi wao na vibaraka vyao, wanajipa malipo yaliyo zaidi ya maradufu ya wengi wa wafanyakazi katika kila kiwanda au mradi… Yasemekana kuwa bila wao, basi hakuna lolote ambalo linaweza kutendeka’’ (kur. 143-144).

Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa jamii ya mwandishi imeaminishwa kuwa wao hawana uwezo, akili na busara ya kufanya maendeleo makubwa kama wazungu. Mkangi anatumia taswira ya mbinguni kiuamilifu kama wigo-bezo na kuicheka jamii inayodhani mambo mazuri yote yako Mbinguni badala ya kujitahidi kuyaleta wenyewe. Wito wa Mkangi ni kuwa, binadamu asijikalie kitako na kuota kwamba siku moja akifa ataenda mahali pema peponi kama vile imani ya dini inavyomwongoza. Binadamu anaweza kujijengea peponi hapa duniani kama vile sala ya Bwana inavyokariri:

> ‘‘Baba Yetu Uliye Mbinguni, Jina Lako Litukuzwe. Ufalme Wako Nauje. Mapenzi Yako Yatendeke Hapa Duniani kama Yatendekavyo Huko Mbinguni…’’ (uk. 147).

Vilevile, kilele cha Mkangi kuibua yaliyoandikwa katika Buku lile ni kumtia msomaji ari na mshawasha wa kufahamu kuwa, hata kwa Mungu si dhambi kujinasibisha na wanyonge na wanaonyanyaswa. Aidha, si dhambi kupigania usawa na haki. Ni viongozi dhalimu ambao wanatumia uongo kupitia dini kwamba, matendo ya kupigania haki na usawa na kupinga walio mamlakani ni dhambi. Maskini nao kupitia uongo huu wa viongozi dhalimu wanaaminishwa kuwa zamu yao ya kufurahi itafika wakifa. Mkangi alilenga kufichua unafiki huu wa viongozi wadhalimu.

Kwa muhtasari, taswira za Mapenzoni alizoibua Mkangi, zilikusudiwa kumzindua msomaji na kumpa mwamko mpya juu ya hali halisi ya maisha yake, chanzo na suluhu la kuyatatua matatizo yanayomkabili. Mwamko alioulenga Mkangi unalandana na mihimili ya Nadharia Amali.

### 4.1.4 Mapacha

Taswira ya mapacha inahusu wasichana wawili Medza na Chihenyo. Walipozaliwa walikuwa wamekumbatiana mithili ya wapenzi, ndiposa wakaitwa mapacha. Taswira hii inaashiria mapenzi makubwa na kutobanduka kwao walipokuwa tumboni. Walitenganishwa

walipokuwa nje baada ya kuzaliwa. Asasi ya ndoa ndiyo iliyokata kitovu kilichokuwa kimewaunganisha, kwani Medza aliolewa na mwanaume maskini ilhali Chihenyo aliolewa na mwanaume tajiri. Wasichana hawa wawili waliolewa siku moja na wakajifungua watoto siku moja. Medza alimzaa Tabu na Chihenyo alimzaa Furaha. Majina yao ni ya kimajazi na yametumiwa kiuamilifu ili kiashiria hali zao halisi za maisha. Siku moja watoto wa mapacha hawa Tabu na furaha walipatwa na msiba. Tabu alishikwa na ugonjwa ghafla na kuanza kutapika na kujikojolea. Wakati ule mamake Tabu alikuwa akijaribu kumfumia kirinda kutokana na mabaki ya matambara ya mavazi yake ya harusi ili kusitiri mwanawe uchi na baridi. Maelezo haya ya mwandishi yanaashiria umaskini mkubwa wa Medza. Nayo taswira ya Tabu kutapika, kuhara, kupapatika na kujikojolea, inaonyesha maumivu makubwa aliyokuwa nayo na uzito wa ugonjwa uliompata. Medza pasipo na lingine alimzoa mtoto wake na kumkimbiza katika zahanati kwa miguu. Hakuwa na uwezo wa kupata gari ili wafike zahanati haraka. Alifika akiwa amechoka na amejaa matapishi na kinyesi cha Tabu.

Taswira ya Tabu na mamake ambaye alikuwa amejaa matapishi na kinyesi cha mwanawe inazua athari za kihisia za huruma kwa msomaji. Ni taswira ambayo inauhangaisha moyo wa msomaji sana na hivi ndivyo anavyolenga Mkangi. Walipofika mahali pa huduma ya kwanza, waliungana na wengine. Mwandishi anasema:

> ‘‘Hapa palikuwa ni pa huduma ya kwanza. Hakuwa wa kwanza hapo. Alikuta na kuungwa na wengine wengi wa aina yake kitabaka. Mgonjwa alihitajika kungojea hapo kwa huduma na uchunguzi. Baada ya hivyo, ndipo ilipojulikana ikiwa angelazwa ama la. Wakisubiri, Metabu, aliona sakafu imejaa wagonjwa waliotapatapa kwa uchungu. Migumio yao ya maumivu ilisikika na kupajaza hapo pote. Wagonjwa wengine walionekana wamelala tu tuli pale sakafuni na macho yasiyo na tamaa kutumbuka. Msitari wenye ulijikokota kwa mwendo wa kinyonga.’’ (uk. 182).

Dondoo hili linatupa taswira ya kundi la akina yakhe, Tabu akiwa mmojawapo ambao wanaonyesha kukata tamaa na ambao wana maumivu makubwa sana. Migumio ya maskini hawa inaashiria uchungu waliokuwa nao kutokana na ndwele tofautitofauti. Kundi hili la ‘‘wasio nacho’’ linazua hisia za huzuni dhidi ya mfumo wa siasa za kitabaka. Athari ya mfumo wa siasa wenye matabaka ni kuwa maskini hutengwa na kusukumwa pembeni na matajiri. Maskini hunyimwa haki na mahitaji ya kimsingi kama vile huduma ya matibabu. Aidha, hakuna anayemjali maskini. Athari hii ya jamii yenye matabaka ndiyo inayompata Medza na mwanawe. Wakati huo wote Medza alikuwa anampakata mwanawe. Tabu roho

ilikuwa ikimwenda mbio na kutapika mara kwa mara. Sasa matapishi yalikuwa yamemwisha. Kilichokuwa kikimwandama kikawa ni fufutiko la kigegezi ambalo lilifanya mbavu zake changa kubenuka kwa uchungu mwingi uliozidishwa na kutokwa kwa nyute zikiwa na nyongo. Machozi yalikuwa yakimtoka mwana, huku macho ya huzuni yakimwangalia mamake yakisihi usaidizi (uk. 183).

Kutokana na taswira ya hali ya Tabu, msomaji anapata hisia za kupuuzwa kwa maskini na mfumo wa kitabaka. Mkangi ameibua hisia hizi kiuamilifu ili ziwe kama kichocheo cha zinduko kwa msomaji kwamba, jamii yake ina matabaka na yanapaswa kuondolewa ili kuleta usawa na haki kwa wote. Aidha, msomaji analengwalengwa na machozi anapoona mtoto ambaye anatapika, matapishi yanakwisha, anashikwa na fufutiko la kigegezi ambalo linampelekea kutoa sauti tu ya kutapika kwa sababu tumboni hamna kitu. Taswira ya kubenuka kwa mbavu zake changa kwa uchungu na nyute kumtoka Tabu inamfanya msomaji kuhisi uchungu na maumivu aliyokuwa nayo mtoto huyu. Macho ya huzuni ya Tabu ambayo yanamwangalia mamake yakisihi usaidizi, yanazidisha hisia za huruma kwa msomaji na chuki kwa madaktari ambao hawakuwajibika kumsaidia mtoto huyu angalau kuokoa uhai wake. Hali ya Tabu ilikuwa mbaya mno kwa sababu ya kutohudumiwa haraka. Mwandishi anaeleza:

> ‘‘Ilikuwa sasa ni jioni, zamu ya kumwona daktari ilipofika. Tabu akalazwa kitandani kwa uchunguzi. Wakati huu, ngozi yake ilikuwa imebadilika na kuonekana kama kizee.’’ (uk.184).

Taswira ya Tabu ya kubadilisha ngozi na kuwa kama ya kizee inazidisha hofu na wasiwasi kwa msomaji. Mtoto huyu alikuwa amepoteza maji mengi mwilini. Si ajabu ngozi yake haikuwa na wororo wowote ule. Daktari anatambua kuwa Tabu hakuwa na kitu tumboni. Aliugua ugonjwa wa utapia mlo na marasimi. Huu ni ugonjwa wa kukosa lishe bora unaowapata watoto wa maskini. Tabu alikula tunguja-mwitu wakati njaa ilipomzidi. Tunguja-mwitu ni matunda yenye sumu. Taswira ya Tabu kula tunda la mwitu lenye sumu baada ya kukosa chakula ni fumbo linalomaanisha mengi. Kwanza, linamaanisha kuwa jamii yenye matabaka, maskini hukosa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi na hata huduma bora ya matibabu. Pili, linamaanisha kuwa, maskini katika jamii hii ya kimatabaka, huwa wamekata tamaa maishani ndio sababu hutumia chochote kama chakula hata ikiwa ni sumu. Aidha, maskini katika jamii kama hii huwa na hadhi sawa na mnyama. Mwandishi alitumia taswira hii kiuamilifu kuwazindua wasomaji kwa kuwamlikia matatizo wanayopitia ili kupigania ukombozi katika maisha yao.

Kilele cha kupuuzwa na kubaguliwa kwa maskini kinafikia wakati tunaelezwa kuwa mtoto huyu hakuweza kulazwa kutokana na ukosefu wa vitanda na ‘drip’.  Mamake Tabu hana pesa za kununua ‘drip’ hiyo katika maduka ya kuuza dawa. Aidha, hakuna dawa yoyote ile daktari aliyompa Tabu ya kumsaidia kutibu ndwele yake. Daktari bila kigegezi anamshauri Medza ajaribu tena keshoye huenda akababahatika. Medza alipokuwa njiani peke yake usiku akirudi nyumbani, mwandishi anasema:

> ‘‘… Akiwa njiani usiku huo akirudi nyumbani peke yake, alimsikia Tabu akikata roho mgongoni kwake.’’ (uk. 185).

Haya yalipotendeka, mumewe alikuwa ameajiriwa mbali na kwao kazi ya kulinda familia ya Mchuna mmoja ili aweze kulala kwa usalama. Alikoajiriwa mumewe kulikuwa mbali na mawasiliano yalikuwa ni njia ya mdomo tu, kwa hivyo mumewe alikuja kuyajua baadaye. Kifo cha Tabu akiwa mgongoni mwa mamaye, kimetumiwa namwandishi ili kuwa kichocheo cha zinduko kwa wasomaji. Kifo cha Tabu kimesababishwa na mambo kadha. Kwanza, umaskini wao kiasi kwamba Tabu hapati chakula. Analazimika kula matunda yenye sumu njaa inapomzidi. Pia, Tabu alikuwa na utapia mlo na marasimi kutokana na ukosefu wa lishe bora. Aidha, ukosefu wa utu wa daktari aliyemnyima Tabu huduma. Kutokana na maelezo haya, mwandishi anamzindua msomaji kuhusu namna utabaka unavyoathiri afya ya jamii. Hili ni jambo lenye uhalisi katika jamii nyingi barani Afrika ambazo zina matabaka. Magonjwa kama utapia mlo na marasimi ni sugu mno kwa watoto wa tabaka la chini. Kwa jumla mwandishi alitumia taswira hii ya Tabu kiuamilifu ili kuwamulikia wasomaji matatizo yanayowakumba maskini katika jamii yenye matabaka. Amewamulikia matatizo hayo akidhamiria kuwachochea ili wazinduke na kupigania mapinduzi yatakayoleta usawa na haki kwa wote.

Ili kuzidisha athari zinazoletwa na matabaka katika jamii, Mkangi anatusafirisha katika jamii ya pili ambayo ni ya kitajiri. Katika kisa hiki, mtoto wake Chehenyo (Furaha) aliungua siku ile ile Tabu alipougua. Alingua alipovutiwa na sufuria iliyokuwa mekoni na akaiburuta. Aliungua vibaya sana. Chihenyo alipomwona mwanawe Furaha ameungua hakupoteza muda. Mara moja alimpigia simu daktari wao wa kibinafsi ambaye alimwelekeza la kufanya kuhusu huduma ya kwanza. Vifaa vya huduma ya kwanza vilikuwamo humo nyumbani. Alimtia Furaha garini na kumpeleka Nokolani. Mlangoni alimkuta daktari wao akimngonjea na kumchukua mtoto mara moja. Chihenyo alipewa kinywaji ambacho daktari wake alikuwa ameagiza apewe. Alipomaliza akajisikia mwili ukilainika na usingizi kumnyemelea.

Kufikia hapa, kitendo cha kupiga simu kwa daktari wao wa kibinafsi, huduma ya kwanza, kumpeleka mtoto Nokolani kwa gari, kuchukuliwa kwa furaha mara moja na madaktari na mamake kupewa kinywaji cha kumlaza asimfikirie mtoto wake kinaashiria ukinzano baina ya Tabu na mamake kwa upande mmoja, na Furaha na mamake kwa upande mwingine. Hizi ni taswira tofauti ambazo zinalenga kuchochea zinduko kwa msomaji kuhusu athari mbaya inayoletwa na tofauti za mifumo ya kiuchumi katika jamii. Hisia za msomaji kwa msiba wa Furaha ni tofauti na hisia za Tabu. Msomaji anapatwa na hisia za kuudhika kwa kulinganisha vitendo vya kiutu anavyotendewa Furaha ilhali Tabu anapuuzwa kutokana na umaskini wa familia yake. Hakuna hisia zozote zile za huruma kutokana na kuungua kwa Furaha. Hisia hizi zinamhamasisha msomaji kuhusu dhiki za maskini ambao chanzo chake ni utabaka.

Hisia za huzuni zinazidishwa na mwandishi anapotueleza kwamba wakati huo mmoja Medza alipokuwa akisikia mwanawe akikata roho na mwili kuanza kuwa baridi hivi ndivyo vile Chehenyo aliposikia akiguswa mkononi kwa upole. Alipoyafungua macho yake kwa uchovu aliona msichana muuguzi akitabasamu. Alipoyaangaza macho zaidi alijikuta yuko katikati ya mumewe na daktari wao. Naye huyo daktari akawa akisema:

> ‘‘Ni nguo zake ndizo zilizomsaidia na kumkinga ama angekuwa amepata majeraha mabaya zaidi. Ni malengelenge ya kiasi ya hapo kipajini na mapajani, ama kuungua kwake ni asili mia tano kwa mia. Mshtuko ndio uliompumbaza kwa hivyo, nimempa dawa ya kumaliza. Kitu cha kuchunga ni kuona kuwa nguo zake hazimgandami pale alipochomeka… Nitawatembeleeni kesho asubuhi nione amelalaje; lakini ikiwa kutatokea mabadiliko yoyote, msikawie kunipigia simu,’’ (uk. 186).

Kutokana na dondoo hili, Mkangi alilenga kumzindua msomaji kuhusu mambo kadha. Kwanza, baadhi ya vifo vya maskini husabishwa na ukosefu wa msaada kutoka kwa matajiri ambao hawana utu na imani kwa wasiobahatika katika jamii. Pili, mwandishi alidhamiria kuonyesha athari mbaya za utabaka hata kwa ndugu. Maneno ya daktari huyu yanaonyesha kwamba madaktari wa kibinafsi wanapatikana katika tabaka moja la matajiri. Ni marafiki wao, na wanalipwa vizuri na matajiri hao. Tatu, dondoo hili linatuonyesha umuhimu wa mavazi mazuri ambayo yalimkinga Furaha kutokana na majeraha ya maji moto. Aidha, umuhimu wa simu kwa familia unatiliwa mkazo. Mwandishi anazidi kuchokora hisia za uchungu kwa msomaji anaposema kuwa, Fauraha aliweza kusoma na kuhitimu akawa daktari ilhali hata kaburi la Tabu likawa halijulikani tena ni wapi lilipokuwa (uk.186).

Taswira ya mapacha inaonyesha hali ya utabaka kupitia ndoa. Kwa mujibu wa taswira hii huduma za matibabu zilikuwa tofauti. Picha ya Nokolani inaibuliwa kuwa tofauti na zahanati za wanyonge. Taswira ya Nokolani ikilinganishwa na ya zahanati za wanyonge ni kichocheo cha uzindushi. Taswira hizi ni tofauti kabisa ambazo zinaashiria bonde kubwa lililopo baina ya matajiri na maskini. Tofauti hii ya kitabaka ndiyo Mkangi anazungumzia ili awazindue wanajamii kupigania usawa. Aidha, Mkangi alitaka kupitisha wazo kuwa mikasa ya vifo katika zahanati za wanyonge inasababishwa na madaktari na wafanyakazi wasiowajibika kama asemavyo mwandishi:

> ‘‘Hali hii ilizidishwa na wauguzi, madaktari na wafanya kazi wote, kwa jumla, kujiona, kukosa nidhamu na moyo wa kiutu. Kwa upande wao, wagonjwa hawa hawakuhalisi kuendewa mbio. Kwa hivyo, wakati wa chai ulipofika, wote walipatoweka bila kigegezi rohoni. Hiki kilikuwa ni kitendo chao cha kawaida kama vile kwenda choo.’’ (kur.183-184).

Kupitia taswira ya mapacha, tabia ya baadhi ya madaktari, wauguzi na wafanyakazi wa umma ambao hawafanyi kazi yao kwa dhati, inafichuliwa. Mkangi alitumia taswira hii kiuamilifu akidhamiria kutoa mwito kwa madaktari ili waone wajibu wao kwa umma mnyonge na wautekeleze ipasavyo. Pia, anatoa wito kwa msomaji wa riwaya hii kuandaa mapinduzi kwa wale wafanyakazi wa umma ambao hawatekelezi wajibu wao ili kuleta haki na usawa katika jamii.

Kuelewa taswira hizi kama kichocheo cha zinduko kunategemea kuelewa lugha kwa kuzingatia maana zinazoibuliwa na lugha hiyo. Mwandishi ametumia lugha yenye hisia nzito kwa namna inayosawiri ufahamu wa msomaji. Mwandishi kupitia kwa taswira hii anatayarisha umma kwa minajili ya kujikomboa na kuanzisha ujenzi wa jamii mpya isiyo na matabaka. Aidha, Mkangi alilenga kuwazindua wasomaji kuwa migawanyiko ya kitabaka katika jamii inategemea uwezo wa kumiliki na kudhibiti nyenzo za kuzalisha mali hali ambayo inalifanya kundi moja kupata na lingine kukosa.

Taswira za mapacha zimetumiwa kiuamilifu ili kuweka wazi mambo kuwa huduma za matibabu huwa duni kwa sababu ya umaskini, ufisadi na ubaguzi baina ya watawala na watawaliwa. Kisa hiki ni mwongoni mwa shida nyingi zinazokabili nchi nyingi barani Afrika, Kenya ikiwemo. Kisa hiki kinalandana na mihimili ya Nadharia Amali hasa ule unaohusu matumizi ya kitu ili kuona matokeo yake. Matokeo ya matumizi ya kisa hiki ni kuwa kiliwazindua Walenisi. Tunambiwa:

> ‘‘Yaonekana kisa hiki kilikuja kikawa kisa kimojawapo muhimu kilichowazindua Wawalenisi. Kiliwafanya kutambua kuwa uadilifu si kwa kuzaliwa ama kwa bahati mbaya, bali ilikuwa ni kwa sababu wa kijamii uliodumishwa na sheria za utawala wa kichuna. Bila shaka kilikuwa kisa kimojawapo kilichoanzisha harakati ambazo mwishowe zilifanikiwa kwa kuwatimua Wachuna na Uchuna wao.’’ (uk. 187).

Maelezo haya ya mwandishi yanaibua taswira ya mapinduzi yaliyotokana na kuzinduka kwa Walenisi. Zinduko lao lilileta mwamko mpya wa ujenzi wa jamii mpya. Lengo la Mkangi kutuchorea taswira ya mapinduzi ya Walenisi ni kuchochea mapinduzi kwa wasomaji ili nao waubadili mfumo mbaya wa kisiasa usiowajali maskini. Mkangi alilenga kuwamulikia wasomaji kuwa njia ya kipekee ya kuondoa ubaguzi, dhuluma, ubepari, umwinyi na mali ya umma kumilikiwa na watu wachache ilhali wengi wanaumia kwa ujamaa. Mfumo ambao kwa mujibu wa Mkangi anaupendelea kwa sababu hauna ubaguzi na dhuluma kwa wanajamii.

Hali kadhalika Mkangi alitumia taswira za mapacha kiuamilifu ili kuibua hisia mbalimbali zinazoweza kuathiri moyo kwa kuhisi uchungu, kutokana na dhuluma zinazotendewa maskini na matajiri. Kutokana na hisia hizi, msomaji anatiwa hima ya kutaka kuleta mapinduzi katika jamii yake ili haki na usawa viwepo kwa kila binadamu.

### 4.1.5 Dzombo

Mkangi anatuchorea taswira ya Dzombo akiwa mahakamani akingojea hukumu yake. Dzombo hakutazamia huruma yoyote kutoka kwa hakimu. Hakimu alipoingia na watu kuamriwa kuketi, yule hakimu aliegemeza miwani yake nusu glasi puani kwake na akamtazama Dzombo kwa ile sehemu iliyo wazi na kumwamrisha kusimama. Baada ya kuinuka, ingawa Dzombo hakutarajia huruma yoyote alipigwa na butwaa la bumbwazi kwa hukumu aliyopewa ya ‘kifo’. Mwandishi anasema:

> ‘‘…zama hizo, mahakama hazikuwa zikifuata sheria kwa mujibu wa kulinda, au kutetea, wala kudumisha haki za binadamu. Kazi yake kubwa ilikuwa ni kumtia hatiani yeyote yule alikuwa amepatwa na kisirani cha kushtakiwa. Kwa hivyo, baada ya kuinuka, hakimu naye bila hata kusita, akatamka: ‘kifo’ baada ya kuhukumu, akazoazoa majoho yake na kuelekea ofisini kwake.’’ (uk.1)

Kutokana na dondoo hili tunachorewa Dzombo kama mhusika mnyonge ambayo hapatiwi nafasi ya kujitetea kabla ya kupewa hukumu. Yeye ni kiwakilishi cha wanyonge

wanaonyimwa haki ya kujitetea mbele ya mahakama wanaposhtakiwa kuwa wamefanya makosa. Kulingana na mahakama hii na uamuzi wa hakimu huyu, Dzombo anasawiriwa kama mtu ambaye alifanya kosa kubwa ambalo halifai kusamehewa bali lafaa hukumu ya kifo. Mwandishi anatumia taswira hii kiuamilifu ili kuonyesha kuwa kuna matabaka katika jamii ya Dzombo. Matajiri wametunga sheria na kujenga mahakama ili kulinda maslahi yao lakini kwa upande mwingine zikidhulumu maskini. Hakimu na matajiri hupatikana katika tabaka moja na hivyo wameungana ili kumwangamiza maskini katika jamii. Hukumu ya kifo imetumiwa kiuamilifu kumaanisha kuangamizwa kabisa kwa wale wanaopinga watawala. Mwandishi ametumia taswira hii ya Dzombo akiwa mahakamani na hukumu anaopewa ili kuwachochea wasomaji wanyonge kuandaa mapinduzi katika jamii yao yenye dhuluma kwa watawaliwa. Anatarajia wasomaji kuzinduka na kuleta mabadiliko katika mfumo wa utawala ili uzingatie haki na usawa.

Baada ya hakimu kutoa hukumu ya kifo kwa Dzombo na kuzoazoa majoho yake na kuelekea ofisini kwake, mwandishi anatuchorea taswira ya Dzombo akiwa amesombwa juujuu na kuangushwa ndani ya gari la mahabusu. Huku nyuma Dzombo aliwaacha wapenzi wake wakiomboleza kwa huzuni. Waliokuwako walijua mara moja gari hili lilikokuwa likielekea. Nao, ili waweze kushuhudia kutekelezwa kwa hukumu hii, na pia kumpa kwaheri ya mwisho, walitoka nje na kufululiza huko huko. Mwandishi alitumia taswira hii kiuamilifu ili kuonyesha dhuluma na mateso wanayopata watawaliwa kutoka kwa watawala wao. Dzombo hakupewa nafasi hata ya kuwaaga wapenzi wake. Mwandishi anataka kuwachochea wasomaji ili waandae mapinduzi na kuleta mabadiliko katika mfumo wa utawala unaowadhulumu wanyonge katika jamii.

Kuna taswira ya jamaa zake Dzombo karibu na sayari ili angalau waweze kumpa kwaheri ya mwisho. Walitokwa machozi na kuvuta kamasi, baa lao hili likawa halisemeki. Machoni kulisimama chombo cha mauti. Dzombo aliletwa akiwa amevalishwa tayari ili kutazamana na mauti yake. Kabla ya siku hii yeye alikuwa amesikia tu juu ya hukumu ya kifo kwa sayari lakini hii leo, kafara hakuwa mwingine isipokuwa yeye. Mwandishi alitumia taswira hii ya Dzombo akiwa tayari amevalishwa na ya jamaa wake wakitokwa na machozi kiuamilifu ili kuibua hisia za huzuni kwa wasomaji. Lengo la Mkangi kuibua hisia hizi za huzuni kwa msomaji ni kutaka kuchochea zinduko ili apiganie haki katika jamii yao. Maneno ya Dzombo kuwa, 'kabla ya siku hii yeye alikuwa amesikia tu juu ya hukumu ya kifo kwa sayari…', (uk.2) yametumiwa kiuamilifu. Mwandishi amelenga kumfahamisha msomaji kuwa, vitendo hivi vya unyama vimekuwa vikitekelezwa na watawala kwa watawaliwa kwa muda mrefu na

hii si mara ya kwanza. Alitaka msomaji afafanukiwe kuwa watawala hawana utu wowote katika maisha yao kwa watawaliwa. Mwandishi anataka msomaji kuutazama mfumo huu wa utawala kwa jicho pevu na ikiwezekana apange mapinduzi dhidi ya mfumo huu.

Mwandishi anatuchorea taswira ya Dzombo akiwa ndani ya sayari akikaribishwa na sauti ya mtambo-mtu. Sauti hii ya mtambo-mtu iliyomkaribisha ilimwarifu kuwa, ana dakika tano tu na aangalie maelezo ya kuendesha hapo mbele. Ndani ya sayari Dzombo alikwishaamua kuwa dakika tano ni nyingi sana kwa mtu kufufuka, sembuse ya mtu kufa? Kwa hivyo, alionelea kuendelea kupambana hata ikiwa ni dakika tano tu ndizo zilizokuwa zimebaki. Mwandishi anatuonyesha mhusika Dzombo ambaye ni mwenye msimamo thabiti kuwa panapo uhai, mauti aghalabu hujikunja. Kule ndani ya sayari tunamwona Dzombo asiyekuwa na hamaki hata ingawa alikuwa kaburini. Mwandishi anatueleza:

> ‘‘Ili aweze kuishi, alifahamu kuwa hamaki ndizo zilizokuwa adui wake mkubwa kwa wakati ule. La muhimu lilikuwa ni kuamua ni lipi la muhimu zaidi lililiokuwa likimpasa alijue, alifahamu na kisha atende ili limwezeshe kumfikia kiwango kilichofuata’’ (uk. 7).

Kutokana na taswira hii tunamwona Dzombo asiye na hamaki hata ingawa anatazamana na mauti ambayo hakuyatarajia wala kujitayarisha kwayo. Mwandishi ameitumia taswira hii ya Dzombo asiyekuwa na hamaki anapotazamana na mauti yake kiuamilifu ili iwe kama kichocheo cha zinduko kwa wasomaji wa riwaya hii. Analenga kuwafahamisha wasomaji kuwa, tusihamaki kwa unyama tunaofanyiwa na watawala dhalimu bali tutumie unyama huo tunaotendewa ili kuleta haki na usawa katika jamii yetu. Kwa kutojihusisha na hamaki, tunaonyeshwa picha ya Dzombo akichunguza usukani. Aliushika na akauvuta na akajua kwa uhakika kwamba utazisikiliza amri zake. Hapa Dzombo anaonekana mwenye matumaini.

Baada ya sayari kujing’oa, pumzi zilimwangama kwa ghafla. Alisikia akili ikiwa nyepesi na mwenye furaha ya ajabu. Alikuwa karibu kufunga macho alale lakini alijibumburusha haraka kutoka kwa ulaghai huo. Mwandishi anatuonyesha taswira ya Dzombo akiwa karibu kulala lakini akagutuka ili kumfahamisha msomaji kuwa, wanapoanza harakati za kupigania ukombozi wawe macho hadi mwisho. Wasidanganyike kwa hatua chache ambazo watakuwa wamepiga bali wajitahadhari katika kila hatua ili waweze kupata ushindi wao. Haya yanaafikiana na Nadharia Amali inayozingatia umuhimu na maana kupitia kwa kutazama na kujaribu matokeo au mwisho wa kitu fulani ili kutathimini umuhimu wa kitu hicho. Hii ndiyo sababu Dzombo alijitahidi kuishi kwa kupaa angani kwa sayari. Alizidi kusoma jinsi ya

kuiendesha akiendelea kutazama huku na huku sio kwa sababu ya woga bali kwa sababu ya kujiandaa (uk. 10).

Kuna taswira ya Dzombo ambaye amesakamwa na kiu na njaa akiwa ndani ya sayari ambayo ilikusudiwa kusababisha kifo chake. Kiu na njaa inayomkaba Dzombo akiwa sayarini imetumiwa kimafumbo kumaanisha changamoto ambazo wanamapinduzi hukumbana nazo wakiwa katika harakati za kupigania ukombozi. Lakini tunaambiwa kuwa hakukaa tu ili njaa na kiu vimuangamize bali alitalii sayarini na kutafuta wapi vyakula na vinywaji vilivyopachikwa. Kitendo hiki cha Dzombo cha kutafuta chakula ndani ya chombo ambacho kilichukuliwa kama kaburi lake, kinamsawiri Dzombo kama mwanaharakati mwenye imani na matumaini maishani hata katika hali ya mauti. Haya yanatarajiwa kuzindua wasomaji kuwa mwenye shida lazima ashughulike kwa kutatua hizo shida zake na kwa matumaini atafaulu. Mwandishi anasema kuwa, alibofya vizibo viwili ama vitatu hivi, na kwa ghafla mijeledi ikafyatuka. Alikula ugali na sukuma na kunywa maji ya zamzamu na madini pia. Sasa Dzombo kufa kwake kukawa amekusahau na akawa anatazamia mbele ambako atapata fursa ya kujieleza kwa Mungu mwenyewe (uk.11).

Mwandishi anatuchorea Dzombo akikumbana na majabali mbalimbali katika safari yake kwa sayari. Majabali haya yalikusudiwa kusababisha kifo chake kwa namna mbili. Kwanza, watawala walitarajia sayari kugonga mojawapo ya majabali haya na kulipuka kisha kudondoka kama gurudumu la moto ili kusababisha kifo chake. Pili, waliamini kuwa katika harakati za kukwepa majabali haya, sayari ingeisha mafuta. Kumalizika kwa mafuta kuna maana moja: kushuka kwa sayari kama jiwe na huku ndiko kungekuwa kufa kwake. Majabali haya yalikuwa ya kutisha sana. Mwandishi anasema:

> ‘‘Kutupa macho juu ya kidirisha cha kioo cha mtambo-mtu, akaona picha iliyomshtusha na kumtisha ajabu. Mikojo ilianza kumjia, lakini nayo pia ikakwama. Ule uvimbe wa kutisha ulizidi kujikuza na kujijaza pale kiooni jinsi vile sayari ilivyozidi kwenda kasi…jabali la magonjwa lilionekana likifura kila nukta. Kwa vile halikupendeza kamwe, aliweza hata kuhisi kunuka na kuvunda kwake kwa kule kuliangalia lile umbo lake tu pale kiooni. Hata yale maumivu yaliyokuwa ndani ya jabali hili, yaliweza kutanabahika kwa namna ya vile lilivyoumbika. Kutisha kwake hakuelezeki’’(uk.11, 23).

Mwandishi anatuchorea Dzombo akipambana na majabali yaliyokusudiwa kusababisha kifo chake na hata kuyashinda. Hata ingawa majabali haya yalikuwa ya kutisha, Dzombo

alipambana nayo kwa ukakamavu hadi akaibuka mshindi na shujaa. Mwandishi alitumia taswira hii ya Dzombo akikabiliana na majabali kiuamilifu ili iwe kichocheo cha zinduko kwa wasomaji wa riwaya hii. Mkangi alidhamiria kuwafahamisha wasomaji kuwa katika harakati za kupigania ukombozi wa jamii lazima mpiganiaji apitie matatizo au vikwazo mbalimbali hasa vya kutisha. Pia, alitaka wafahamu kuwa, yule atakayeibuka mshindi ni yule atakayekuwa mkakamavu na mwenye matumaini maishani. Lazima wanaharakati wajitayarishe kwa mapambano makali na tena mazito ambayo yangali yanawasubiri.

Baada ya kufaulu kupambana na majabali matatu: jabali la ujinga, magonjwa na udhalimu, Dzombo aliweza kutua katika nchi ngeni na ya kufurahisha jinsi mwandishi anavyosema (kur.33-34). Dzombo alipofika ulimwengu huu mgeni, aliyatembeza macho yake na kwa bahati nzuri akaona pembeni, vitu vyeupe vilivyokaa kama mitumbwi, vikija na kutoweka. Mwandishi anatwambia kuwa Dzombo aliviangalia na kuvikagua kwa muda mrefu kutoka mbali. Mwisho aliamua kuvikaribia lakini kwa tahadhari nyingi. Alivyozidi kuvikaribia ndivyo kimiujiza vyombo hivyo vigeni vilivyozidi kujidhihirisha. Mwandishi anasema kuwa, kweli vilikuwa vitumbwi, ajabu yake ni kuwa hakukuwa na maji. Badala yake aliviona vikielea hewani (uk.35). Baada ya kustaajabia Dzombo hakuwa na shaka kuwa alikuwa ametua mbinguni. Alijitupa ndani ya chombo kilichokuja na kukaa nyuma kabisa ya hicho kitumbwi huku uso wake wote ukiwa tabasamu tubu. Sauti nyororo zilikuwa zikiimba kwa utaratibu na muziki wa kutumbuiza. Alianza kufikiria vile mbavu zake zingekuwa. Mawazo yake yalipasuliwa kwa ghafla na kelele za nderemo na vifijo alipojikuta katikati ya sherehe kubwa kila mtu akimwangalia yeye tu. Wenyeji wake wawili – mke na mume, walijitokeza kuja kumlaki na kumsaidia kutoka mle chomboni.

Taswira ya Dzombo akiwa amefikia katia nchi ngeni imetumika kimafumbo ili kuashiria jamii mpya ambayo hujengwa kupitia kwa mapinduzi. Jamii hii ni ya kufurahisha na kupendeza. Ni jamii ambayo hakuna matabaka na inazingatia haki na usawa. Katika jamii hii mali ya umma hayajamilikiwi na watu wachache bali na watu wote. Hii ndiyo sababu vyombo hivi vya kusafiria alivyoviona Dzombo na kutumia kimojawapo vilikuwepo kwa manufaa ya watu wote na ndiposa akakitumia kusafiria bila kutafuta idhini hiyo kutoka kwa yeyote. Taswira hii imetumika kiuamilifu ili kuwachochea wasomaji kuandaa mapinduzi katika mfumo wa utawala wenye matabaka ili kuyaondoa matabaka haya na kuunda jamii yenye usawa na haki kama ile Dzombo alitua. Aidha, mwandishi anataka kuwazindua wasomaji kuwa ili kuleta mabadiliko katika jamii sio rahisi bali lazima wanamapinduzi kupitia katika

shida na matatizo mengi na ya kutisha kama yale aliyopitia Dzombo kabla ya kutua katika nchi ngeni.

Aidha, Mkangi anatuchorea taswira ya mhusika Dzombo akiwa mkulima. Mwandishi anasema kuwa, Dzombo alikata kauli ya kujiajiri mwenyewe kwa kuwa mkulima. Alikata vichaka na kufyeka msitu. Miiba ilimdunga na jua kumchoma bila huruma. Mvua ilimmalizikia mgongoni na umande kumpa nyungunyungu. Alipanda mahindi na yalipoanza kutoa punga na akiwa na imani katika uwezo wake wa kuzalisha mali, jioni moja, matingatinga yaliingia shambani na kuyafyeka mahindi yote. Keshoye asubuhi Dzombo alikuwa nje ya afisi za wakubwa wa ukulima akiwa amechachawa. Alipokwisha kutoa lawama na uchungu wote aliousikia kwa mrasimu fulani, mrasimu huyo alimwuliza jina lake. Alimfahamisha kuwa alivunja sheria za ukulima. Dzombo alipojaribu kudadisi ili kujua ni sheria gani alivunja alijibiwa kuwa:

> ‘‘Sikiliza, we bwana Dzombo; usidhani hatujakusikia. Mimi nimeshakueleza kwa nini mahindi yako ilibidi tuyafyeke. Na tulifanya hivyo kwa sababu ni Benki ya Dunia yenyewe ndiyo iliyotushauri kuwa sehemu hii inapaswa kupandwa mazao ya kuleta Fedha za kigeni- sasa wewe u nani wa kupinga ushairi huu wa kiutaalamu?’’ (uk. 18).

Taswira hii ya Dzombo akiwa mkulima inaibua hisia za huruma na uchungu kwa msomaji. Mkangi alitumia taswira hii kiuamilifu kwa kuibua hisia hizi za huruma na uchungu kwa wasomaji ili kuchochea uzindushi wa kupigania ukombozi wa wanyonge katika jamii yenye matabaka. Dzombo ametumiwa kimafumbo katika taswira hii kuwakilisha kundi la wanyonge watawaliwa wanaotendewa unyama na watawala. Mwandishi anajaribu kuonyesha wasomaji kuwa, maskini wanajibidiisha katika kufanya kazi ngumu ili kuyakimu mahitaji yao lakini hawafaidiki kutokana na jasho lao bali wananyonywa. Matajiri wanaunda sheria za kuhakikisha kuwa maskini wanaendelea kuwa maskini wahitaji na yule atakayeonekana kujaribu kukata minyororo ya umaskini waliowekewa na matajiri watawala, aadhibiwe. Haya ndiyo anayofanyiwa Dzombo. Aidha, Mkangi anataka kuwazindua wasomaji kuwa, ukulima ndio uti wa mgongo wa uchumi wa nchi. Anahimiza wasomaji watie bidii katika ukulima kwa kuwa ni kupitia kwa ukulima ndipo tunapata chakula na mahitaji mengine muhimu maishani.

Kwa jumla, Dzombo amesawiriwa kama mhusika mwenye bidii, mkakamavu na mwenye matumani maishani. Kwa hivyo, mwandishi alimchora mhusika huyu hivi ili kumzindua msomaji wa riwaya ya *Walenisi* kumuiga ili waweze kufaulu maishani. Kwa upande

mwingine, Dzombo amesawiriwa akikumbana na matatizo mbalimbali katika maisha yake. Tatizo kubwa alilokumbana nalo ni hukumu ya kifo kupitia kwa sayari. Yaliyosababisha Dzombo kupewa hukumu ya kifo ni kupinga watawala kutokana na vitendo vyao vya unyanyasaji kwa watawaliwa. Kwa hivyo, anajitokeza kama mzalendo na mwanaharakati katika jamii. Mwandishi anachochea msomaji kumuiga mhusika huyu ili haki itekelezwe kwa wanajamii wanyonge. Maelezo haya yanaafikiana na Nadharia Amali kwa mujibu wa James (1879), ambaye aliona kuwa maana nzima ya wazo huonekana katika matokeo halisi, matokeo ambayo hujitokeza ama kama tabia nzuri za kufuatwa au tajriba inayotarajiwa iwapo hilo wazo ni sahihi.

## 4.2. Jazanda

### 4.2.1 Majabali

Jabali ni mwamba mkubwa au ni jiwe kubwa (TUKI, 2004). Baada ya Dzombo kuhukumiwa kifo kupitia kwa sayari alikumbana na majabali matatu njiani. Majabali haya yalikusudiwa kusababisha kifo chake ama kwa kugongana na sayari au katika harakati za kuyahepa majabali hayo na kusababisha mafuta ya sayari kuisha na kuanguka kama jiwe. Jabali katika muktadha huu wa riwaya ya *Walenisi* ni jazanda inayomaanisha vikwazo au visiki ambavyo hukumba mwanamapinduzi anapojaribu kupigania jamii ili kuleta mabadiliko katika jamii hiyo. Majabali haya ndiyo yaliyotenganisha ulimwengu wa Dzombo, ambao ulijaa dhuluma na ulimwengu wa Walenisi, ulimwengu mpya usiokuwa na karaha.

Jabali la kwanza alilokumbana nalo Dzombo ni jabali la ujinga. Jabali la ujinga ni jazanda inayowakilisha itikadi za jamii. Itikadi hizi ni zile zilizopitwa na wakati ambazo huwafanya wanajamii wanaozishikilia bila mtazamo mpevu kuendelea kuishi katika hali ya ujinga. Itikadi hizi huwapofusha wengi katika jamii na kufanya mjinga kuonekana mwerevu na mwerevu kuonekana mjinga; mwehu kuonekana timamu; muuaji kuonekana mlinda usalama; msema ukweli kuwa mwenda wazimu; na busara hutoka kwa wasaliti. Kuna aina mbili za itikadi: itikadi asilia na itikadi jamii. Itikadi asilia ni zile ambazo hutokana na familia mtu anamozaliwa ilhali itikadi jamii ni itikadi ambazo hutokana imani za jamii pana. Itikadi hizi asilia ndizo zilizosababisha hukumu ya kifo kwa Dzombo. Mwandishi anasema kuwa siku moja, Dzombo alikuwa amemwambia nduguye kuwa hali ya ufukara wao ilitokana na kunyanyaswa na tajiri wao. Kwa kuwa ndugu huyo hakuwa akijua maana ya kunyanyaswa, basi yeye keshoye alimwendea tajiri wao na kumwambia, ‘‘Hebu nami nikunyonye.’’ (uk.14). Kwa sababu ya ujinga, yeye aliamini kuwa tajiri wake akikubali amnyonye naye atakuwa

tajiri. Usemi huu ulisababisha tajiri kuona Dzombo kama mchochezi na hivyo kupewa hukumu ya kifo kama mbinu ya kukomesha uchochezi unaokusudiwa kuzindua wanyonge kuona adui wao. Pia, itikadi asilia inajitokeza wakati jamaa na marafiki walikusanyika kumpa kwaheri ya mwisho katika kituo cha sayari. Mwandishi anasema:

> ‘‘kulikuwako na wale waliofurahishwa na kitendo hicho. Hawa walisikika wakisema ‘hii ndiyo dawa ya maneno mengi. Sasa wacha ajiropokee pekee humo ndani. Hakuna haja ya kuwaonea huruma watu kama hawa wasio na bahati kama sisi. Maneno yao mengi ni mbio za sakafuni na hazina budi kuishia sayarini’.’’ (uk. 6).

Kutokana na dondoo ni wazi kuwa, wengine wanaamini kuwa hukumu ya kifo aliyopewa mhusika huyu ni ya haki na inamfaa. Wao wanaamini kuwa adabu kama hii haitawapata kwani huwapata watu wasio na bahati. Mwandishi anatumia jazanda hii kiuamilifu ili kuwazindua kutokana na itikadi ambazo huwafumba na kushindwa kuona hali halisi ya maisha yao. Aidha, itikadi ya kijamii inajitokeza pale ambapo watu wanaamini kuwa, maskini nao pia watakuwa sawa na kuishi maisha bora watakapofika juu mbinguni. Kwa hivyo, wanafaa kuwa na subira na kutowaonea wivu wenzao na kufanya hivyo ni dhambi (uk. 145). Mwandishi kwa jumla alitumia jabali la ujinga ili kuwazindua wasomaji kuwa kunazo itikadi kadha ambazo zimepitwa na wakati na hivyo zinafaa kuangaliwa kwa jicho pevu ili mabadiliko yaweze kupatikana katika jamii.

Dzombo alipambana na jabali la pili ambalo ni jabali la ugonjwa. Jabali la ugonjwa ni jazanda inayomaanisha kasumba au propaganda. Hizi ni habari za uwongo zilizotiliwa chumvi ili kuwashawishi watu kuamini au kukubali jambo fulani. Propaganda hizi hutokea katika jamii yenye matabaka. Kwa hivyo, propaganda hizi huenezwa na tabaka tawala kwa tabaka tawaliwa ili wasiwapinge bali waendelee kuwaunga mkono katika uongozi wao. Katika jamii ya Wachuna, watawala walitumia ujanja tofautitofauti ili waweze kujidumisha uongozini. Mwandishi anasema kuwa walitumia ulaghai ule uliosema kuwa ati hawakuwa watu wa kawaida na asili zao basi si za kibinadamu. Wengine walijitia kusema ati hata damu zao hazikuwa nyekundu bali buluu na waliapa kuwa kuzaliwa kwao hakukuwa kwa kawaida. Walijitia umashuhuri kwa kusema haijulikani walikotokezea, ingawaje hawakuwa na budi ila kuwatawala waja wao. Waliotawaliwa walitazamiwa washukuru sana bahati yao njema (uk.167). Wachuna watawala wakiendelea kueneza kasumba za kuwatofautisha mwandishi anasema kuwa:

> ‘‘Wachuna wakasisitiza kuwa, kuishi kwao vyema kwa kweli haikuwa ni kwa kupenda kwao lakini, ni kwa sababu ya kuzaliwa na akili nyingi za kuwazidi wenzao. ‘Haki ya Mungu,’ waliapa, ‘si kwa kupenda kwetu, bali ni kwa kudra zake Mungu Mwenyewe - na makusudi yake hayabainiki’. Tuko tofauti kama vidole. Bila shaka, haya ndiyo mapendekezo ya Mola mwenyewe, sisi tu akina nani kuyapinga?’’ (uk. 169).

Maneno haya ya watawala yalikusudiwa kuwafanya watawaliwa kutojijua wala kujifahamu. Kasumba kama hii ilipooza bongo za watawaliwa hali nyoyo zao zi bado zinapiga. Hali hii ya kutojitambua iligeuzwa na ikawa ndiyo ya kawaida wakati wa Wachuna. Ishara ya kutojifahamu ni kuiga. Hali hii izukapo, huwa mtu hajithamini yeye mwenyewe tu, bali hata ukoo wake wote. Mwishowe mtu huwa hana adui mkubwa isipokuwa yeye mwenyewe. Lakini, ole wake ajitoleaye kumzindua huyu ataitwa mzushi, mchawi, asiyetosheka na majina kadha wa kadha.

Mwandishi alitumia jazanda hii ya ugonjwa kiuamilifu kuwachochea wasomaji kuzinduka na kupanga mapinduzi kwa watawala hawa dhalimu wanaotumia ujanja na propaganda katika kupumbaza watawaliwa ili wasiwapinge na kuendelea kuwanyonya. Mkangi alidhamiria kuwafahamisha wasomaji kuwa, Mungu ni mapenzi na kwa kuwa hivyo basi, katu hawezi kuwabagua wanawe: huyu amlishe na amvishe akiwa angali hai, na huyu amtaabishe katika uhai wake na amlishe na kumvisha baada ya kufa kwake. Huyu amfanye mtumwa, na huyu bwana wake. Haiwezekani kwa kuwa Mungu sivyo alivyo. Haya ndiyo yaliyoichochea jamii ya Walenisi kuungana na kuleta mapinduzi na kuwaangamiza Wachuna kisha kuunda jamii mpya yenye usawa na haki kwa wote. Haya yanalandana na mihimili ya Nadharia Amali.

Jabali la tatu ambalo lilitumika kijazanda ni jabali la udhalimu. Jabali la udhalimu ni jazanda inayoashiria vita au migogoro baina ya wanajamii wenyewe kwa wenyewe. Migogoro hii husababishwa na propaganda za watawala au tofauti za imani za dini. Inasemekama kuwa watawala Wachuna walikuwa wameeneza kasumba kuwa bila wao basi hakuna lolote ambalo linaweza kutendeka na watawaliwa waliamini hivyo. Watawaliwa waliendelea kudhulumiwa bila huruma na watawala hawa. Wachache waliozinduka walipojaribu kuwazindua wenzao, walishutumiwa na kuchukuliwa kuwa walikuwa maadui wakubwa wa umma. Haikuwa rahisi kuung’oa upuzi huu kutoka mawazoni na fikra za watu duni. Kutokana na haya mwandishi anasema:

> ‘‘Umma ulijigawa na kupigana wenyewe kwa wenyewe. Walipokuwa wakifanya hivyo, Wachuna walizidisha uchochezi, huku wakiendelea kuchovya uhondo wa asali kibuyuni kwa furaha za vicheko mpaka magegoni.’’ (uk. 149).

Mwandishi alitumia jazanda hii ya jabali la udhalimu akidhamiria kuwamulikia wasomaji athari ya propaganda za watawala na imani za watawaliwa. Kupitia athari hizi basi, anawatolea suluhu la migogoro baina ya wanajamii kuwa ni ushirikiano na umoja wao. Mkangi aliweka jabali hili la udhalimu kutokea mwisho baada ya majabali mengine kimakusudi. Ameliweka hivyo kijazanda kuashiria kuwa baada ya wanamapinduzi kuweza kukabiliana na vikwazo mbalimbali, mzozo wa kupingana wao kwa wao hujitokeza ili kukwamiza juhudi zao za kuleta mabadiliko.

Aidha, Dzombo kuhepa majabali kwa ujasiri yaliyokusudiwa kumwangamiza na kutua nchi huru ni kitendo kilichotumiwa na mwandishi kijazanda. Anamaanisha kuwa harakati za mapinduzi si rahisi. Njia ya kuleta mapinduzi ni kama njia ya kwenda mbinguni. Atakayefaulu katika kuleta mapinduzi katika jamii yake ni yule ambaye ni jasiri na mwenye msimamo thabiti. Kile kitendo cha Dzombo kutua katika ulimwengu wa kuvutia ni jazanda ya ujenzi wa jamii mpya yenye usawa na haki. Majabali kutenganisha ulimwengu wa Dzombo na ulimwengu huru alioutua Dzombo ni jazanda inayoonyesha kuwa kuna vikwazo kadhaa ambavyo huzuia ujenzi wa jamii mpya yenye usawa na haki.

Kwa jumla Mkangi ametumia jazanda ya majabali kiuamilifu ili kuwazindua wasomaji kwa kuonyesha umuhimu wa mapinduzi katika ujenzi wa jamii mpya. Mkangi anaonyesha kuwa, hata ingawa majabali yalikuwa ya kutisha mno Dzombo aliweza kujitokeza mshindi na shujaa kwa sababu ya ujasiri wake kwa kuyashinda majabali haya na kutua katika ulimwengu huru wa kuvutia na kupendeza.

### 4.2.2 Trimi, Sayari na Kreshi

Hivi ni vifaa vilivyotumiwa na mwandishi kijazanda ili kuonyesha maendeleo ya kiteknolojia katika sekta ya mawasiliano na ulezi. Trimi, sayari na kreshi ni vyombo vya zao la utafiti. Vyombo hivi viliundwa baada ya utafiti mkali wenye lengo la kusukuma ujinga nyuma. Trimi ni chombo cha kusafiria katika jamii mpya yenye uhuru, haki na usawa ya Walenisi. Chombo hiki hakina makelele, hakichafui mazingira na hakimsababishii kero msafiri. Trimi ni chombo ambacho hakihitaji mwendeshaji wala hakielekezwi mahali pa kuenda bali kina uwezo wa kusoma akili ya msafiri na kutambua mahali anataka kwenda. Kwa kukikalia tu hufyatuka

kwa kasi ya umeme wa radi. Trimi huenda mwendo wa kasi zaidi ya upepo wa kimbunga. Safari ya miaka kumi kwa sayari huchukua siku kumi kwa trimi. Pamoja na mwendo huo wa kasi, uzuri wa trimi ni kwamba huwa imara na shwari vilivyo. Hakuna kutingisika si mbele wala nyuma; kupepesuka huku na huko; ama kurushwarushwa juu na chini. Kinachosikika wakati wa mwendo wake ni mlio wa shwaa tu. Trimi ni mali ya umma ambazo hutumiwa na Mlenisi yeyote anayetaka kusafiri. Dzombo na wenyeji wake walitumia vyombo hivi katika safari yao ya utu.

Kwa upande mwingine, sayari ni chombo kilichovumbuliwa katika jamii ya Dzombo baada ya utafiti mkali kwa kugundua siri za maumbile. Maumbile, lake ni kuficha; binadamu, lake ni kufichua. Sayari hii, ilikuwa ni kielelezo cha migongano hii. Pia yamkini maumbile hufurahikiwa sana kugunduliwa siri zake, ingawaje hayatoi kauli vipi matunda haya ya migongano hii isiyokuwa na mwisho yapasavyo kutumika. Uhuru huu uliachiwa binadamu mwenyewe. Chombo hiki kilivumbuliwa kikidhamiriwa kuwa chombo cha shangwe kwa kupalia angani ili mtu ajisikie yuko huru. Uhuru usiokuwa na kikomo. Kilikusudiwa kuwachukua vijana kwenda kutalii anga za juu ili waweze kushuhudia upeo usio na mwisho, mfano wa vile mishipa ya ujana wao iwapumavyo nyoyoni mwao. Pia, chombo hiki kilikusudiwa kuwachukua wazalendo ili kwenda kujionea upeo wa maisha yao katika hali ya machweo yao hapa. Aidha, kingewapaisha wanaharusi ili kwenda kushuhudia kikweli utamu-chungu wa fungate.

Sayari ilikuwa ni chombo tu. Kazi iliyotunukiwa nayo iliambatana na hali ya maslahi ya binadamu. Kwa sababu ya matabaka katika jamii ya Dzombo, leo hii sayari ilikuwa imepewa kazi ya unyama wa binadamu. Kwa kawaida maslahi ni kwamba hupumbaza binadamu, hasa yakiwa ni ya kitabaka. Nayo sayari hii ilitunukiwa kazi hii ya kutoa uhai yaani; chombo cha mauti (uk. 3). Kwa sababu kilikuwa ni chombo tu, nacho kilikuwa hakina budi kwenda kokote kule kitakakoegeshwa. Kilichohitajika ni kuamriwa tu, basi.

Mwandishi anatumia jazanda hii ya trimi na sayari kiuamilifu ili kumzindua msomaji afahamu kuwa, nchi hii ni yetu na uchumi hauna budi kuwa wetu. Kati yetu, hatufai kuwa na umwinyi, kabaila wala bepari. Sote tuko sawa. Kwa hivyo, tupandacho ni chetu; tuvunacho ni chetu; tuvumbuacho ni chetu; tuzalishacho ni chetu. Utajiri na mali yote ni yetu sisi umma. Na umma ni wewe usomaye haya. Ukipuuza mali ya umma, wa kwanza unayempuuza na kumzorotesha, si mwingine bali ni wewe mwenyewe binafsi. Jukumu la viwanda vya uvumbuzi ni kurahisisha maisha katika Nyanja za mawasiliano. Ili kulitekeleza, utafiti ni

lazima. Aidha, anadhamiria kumzindua msomaji kuwa, mwongozo wa utafiti unafaa uzingatie kuwa, sheria za maumbile zigunduliwe, zitatuliwe na zitumiwe kwa manufaa na starehe za kila mmoja wetu. Vitu na vyombo vya utaalamu wetu katu visitugeuze tuwe watumwa wao bali viwe vya kurahisisha maisha ya umma na kila mmoja wetu kuvitumia na kuvitawala tuviumbavyo na tuvibunivyo ndilo shina la maendeleo na ustaarabu wetu.

Mwandishi anatumia sayari kijazanda ili kuonyesha kuwa katika mfumo wa utawala wenye matabaka, utafiti huzaa mauti badala ya uhai. Anaonyesha kuwa, katika hali hii uvumbuzi wa sayansi na teknolojia, kweli ni kurahisisha maisha-lakini si kwa wote, bali ni kwa wateule wachache. Pia, waviundavyo, wavivumbuavyo na wavibunivyo, vimekuwa ndivyo mabwana wao. Watu wanaishi ili wavitumikie bali si wavitumikishe. Wamevipa roho zao na kujipunguzia hadhi ya ubinadamu kwa kitendo hiki. Kwa upande mwingine mwandishi ametumia trimi kijazanda kuonyesha kuwa, katika jamii yenye usawa na haki, uvumbuzi huu wa sayansi na teknolojia una lengo la kurahisisha maisha kwa wote bila ubaguzi wa aina yoyote ile. Kwa hivyo, mwandishi anawapa suluhu kwa mfumo wa utawala wenye matabaka kuwa ni kuandaa mapinduzi. Matokeo ya mapinduzi ni uundaji wa jamii mpya isiyo na karaha kama ile ya Walenisi aliyotua Dzombo. Haya maelezo yanaafikiana na msingi wa Nadharia Amali unaohusu matokeo ya kitu yanayoonekana katika masuala ya kijamii.

Isitoshe, Dzombo akiwa katika kiwanda cha trimi, alionyeshwa kreshi na kuelezwa kuwa ni chumba ambapo wazazi huleta watoto wao na kuwaacha chini ya uangalizi wa walezi ambao wamefuzu katika kazi ya kutunza watoto wa kila umri. Wanawake nao kwa kujua watoto wao wako karibu na chini ya uangalizi ufaao, huwa huru na wanaweza kushughulikia majukumu mengine ya kitaifa (uk.150). Kreshi ni jazanda inayoashiria maendeleo ya kiteknolojia katika njia za kuwalea watoto kama wanavyofanya Walenisi. Jazanda hii ya kreshi inalenga kuwazindua wanawake wa jamii ya msomaji ambao hulazimika kuwaacha watoto wao wadogo nyumbani. Watoto hawa huachwa chini ya ulinzi wa mayaya ambao wengi wao hawana ujuzi wa kuwatunza watoto. Mama anaenda kufanya kazi mbali kiasi kwamba hawezi kumnyonyesha mtoto wake kama wanawake wa Walenisi. Jazanda ya kreshi inadhamiria kuwatia wanawake wasomaji ilhamu ya kutafuta mabadiliko katika njia za kuwalea watoto kama wanavyofanya Walenisi.

### 4.2.3 Kidundu

Kidundu ni mdudu mdogo mweusi mfano wa mbung’o. Maajabu ya kidundu ni kwamba pamoja na udogo wake wote huo, yeye huweza kukokota matonge ya mavi ya mbuzi, ama ya

kondoo, ama hata ya ng'ombe, ambayo huwa yamemzidi mara tatu kwa ukubwa. Sio hivyo tu, yeye pia huyabingirisha kinyumenyume ili kuyakuza. Na kadiri tonge lizidivyo kukua, ndivyo azidivyo kutia jitihada zaidi ya kubiringisha nyuma aendako na ambako hakuoni. Kidundu ni jazanda inayowakilisha wachuna watawaliwa wajinga. Kwa sababu ya ujinga wao, hawakuweza kutambua ubinafsi na ulafi wa watawala wao. Watawala hawa waliendelea kuwanyonya ili kujistarehesha kwa maendeleo ilhali maskini wakiendelea kuhangaika katika hali ya uchochole. Mwandishi anasema:

> ''Kwa hivyo, huku wakistarehe kwa maendeleo yaliyoletwa na sayansi, ufundi, uhandisi, teknolojia na kadhalika, hakukoma kuwazidishia waliowatawala elimu ya hekima ya kidundu'' (uk.191).

Katika dondoo hili usemi, 'elimu ya kidundu' ni jazanda inayomaanisha kuwa watawala waliwapitishia watawaliwa ujinga wa kufumba macho ili wasitambue ukweli wa maisha. Watawala walikuwa wakieneza elimu yenye ukweli wa kimazigazi kwa watawaliwa. Kwa sababu ya ujinga, watawala walizidi kujiendeleza huku watawaliwa wanyonge wakizidi kusongonyoka. Udundu uliwarudisha nyuma na kukosa hata kuona wapi walikokuwa wakienda. Hali hii ilidumu kwa karne nyingi kwa sababu walikuwa wamekitwa upumbavu kwa kuvikwa ujinga na watawala werevu. Katika ujinga, watu walikataa kuwa watu na utu wao kuwahama na kuwafanya kutojua kwamba la juzi limezaa la jana, na jana, la leo; na la leo, litazaa bila shaka la kesho. Hawakutaka kujua hivyo, ama hawakupewa nafasi ili wajue hivyo. Waliambiwa kikubwa maishani ni leo, leo tu - si mlaji ni hula leo? Kwa hivyo, si vinginevyo vyote ni kwa bahati nasibu? Waja wakafundishwa kuamini hivyo. Ili kuikuza imani hii yao, watawala wakatawanya michezo ya bahati nasibu chungu nzima. Watawaliwa walipumbazwa na kupumbazika na akili zikaganda, na ndivyo watawala walivyoendelea kuipalilia hali hii na kuendelea kuvuna maridhawa.

Mwandishi ametumia jazanda hii ya kidundu kumfahamisha msomaji na jamii yake kuwa matitizo wanayopitia katika jamii yanatokana na ujinga wao unaoenezwa na watawala. Anawafafanulia kuwa ujinga huu umewafanya waendelee kuumia ilhali watawala wao wakiendelea kujistarehesha. Mwandishi kwa kutumia jazanda hii anadhamiria kuwazindua watawaliwa kutokana na ujinga wao ambao unaendelea kuwafumba macho na kuwafanya vipofu wasiojua watokako wala waendako kama mdudu huyu. Ili kuwazindua zaidi watawala wapigane na ujinga unaondelea kuwapumbaza, mwandishi anaendelea kuwafafanulia zaidi athari ya ujinga wao. Anaeleza kuwa, kwa sababu ya ujinga wa watawaliwa, watawala

wachache waliweza kujirundikia mali na kuwa mamilionea hali wengi wakiishi bila chakula, nguo, nyumba, matibabu, elimu na kadhalika. Hawa mamilionea ndio waliokuwa watu waheshimiwa waliopaswa kuigwa kwa kuwa ati walikuwa kielelezo kizuri cha ustaarabu wa kuwa na chungu nzima huku wakilazimisha binadamu wengi kuishi kama wanyama.

Aidha, ujinga uliwadididimiza watawaliwa ndani ya ulafi. Mori ya ulafi wao ilikuwa ikizidi kutiwa chokochoko na watawala ambao walikuwa wakiwatupia vijipande vya nyama kati yao. Kwa uhaba wa  walivyotupiwa, wanyonge ikawabidi kupapurana, kukatana meno na kutiana makucha wakipigania hayo makombo. Kwa upande mwingine, watawala waliwacheka na kujitia kutoelewa chanzo cha tabia ya ushenzi wa wanyonge. Lakini walitambua kuwa walitawalika kwa urahisi baada ya kufuzu kwao katika ushenzi huo. Jazanda anayotumia Mkangi inalenga kumzindua msomaji dhidi ya mfumo wa utawala ambao unamdhalillisha mnyonge kama mnyama kwa kuwatupia makombo ya chakula, na mfumo ambao hautambui maslahi ya watawaliwa kwa sababu ya ujinga wanaowasababishia. Msomaji wa *Walenisi* anafafanukiwa na hali halisi ya shida zinazowakumba wanajamii wanyonge kupitia kwa jazanda hii ili kumpa mwandishi ilhamu ya kupanga mapinduzi kwa mfumo huu wa utawala usiowajali.

Isitoshe, mwandishi anaonyesha kuwa watawala Wachuna walitumia dini ili kuwadididimiza watawaliwa ndani ya figa la ujinga. Watawala waliwapa watawaliwa dini bure na kuwafanya waamini kuwa, ingawaje Mungu ametuumba sawa, usawa huu utapatikana tu baada ya kufa. Watawaliwa kwa kuamini kuwa nao pia watakuwa sawa na kuishi maisha bora watakapofika juu mbinguni, kwa hivyo, wanafundishwa kuwa na subira na kutowaonea wivu wenzao. Kupitia kwa dini wanyonge waliendelea kulaghaiwa kwa sababu walikuwa wakiishi katika hali ya ulemavu wa kimawazo. Watawala wakawa sasa wanalala raha mstarehe, hali wanyonge wakawa wakikesha usiku kucha wakiomba Mungu (uk.191). Kupitia kwa maelezo haya Mkangi alidhamiria kuwazindua wasomaji na jamii yake kuwa, Mungu ni mapenzi. Na mapenzi ni usawa; na usawa ni zao la ushirikiano; na ushirikina, ni mbinu zisizoisha za kuupisha ubinadamu wetu kwa kutumia kwa pamoja, vipawa vyetu tofauti. Pia, anawazindua wasomaji kuwa, unaweza kuwapumbaza watu kila siku, lakini si kila mtu kila siku.

### 4.2.4 Safari ya Utu

Neno safari limetumiwa kijazanda kumaanisha harakati za kumfunza mhusika Dzombo utu. Safari hii ilidhamiria kumfahamisha Dzombo maana ya utu.  Dzombo ni mhusika aliyetokomezwa kutoka duniani na tawala za dhuluma zilizojitia utukufu, ukweli, haki na

usawa. Duniani alikotoka Dzombo jamii yake ilikuwa imejigawa katika matabaka mawili: tabaka la matajiri (watawala) na tabaka la maskini (watawaliwa). Watawala waliwanyanyasa watawaliwa kwa kueneza propaganda yao iliyokuwa ikitoa porojo zilizokuwa zikisema kuwa kula, na kushiba si jambo muhimu. Kwa hivyo, wako wale waliobahatika kushiba - hapa wakimaanisha wao wenyewe; na kwa wale wengi waliokonda kwa njaa, waliambiwa ni kwa sababu hawakubahatika. Kuombaomba ndiko kulikuwa maisha yao na mwisho kifo kikawa mkombozi wao na hivyo hii ni ishara ya jamii ambayo imekosa utu. Kwa sababu Dzombo alikuwa mzaliwa wa jamii hii yenye matabaka aliathirika na imani hii na hivyo kupoteza utu wake. Alipotua katika jamii ngeni yenye kuvutia na kupendeza alijitupa ndani ya chombo ambacho alifikiria kuwa hutumwa kuja kuwapokea wageni wateule ili kuwafikisha mwisho wa safari zao. Akiwa katika chombo hiki anadhihirisha athari ya utabaka. Mwandishi anasema:

> ‘‘ Ungemwona, ungedhani umeona bepari la mabepari, jinsi vile alivyokuwa amejitenga pembeni-nyuma kabisa ya hicho kitumbwi, huku uso wake wote ukiwa tabasamu tupu. Alichokosa ilikuwa kofia ya kinyungu, mtemba na mwavuli’’ (uk. 36)

Katika maelezo haya mwandishi anajaribu kutudhihirishia kuwa mhusika Dzombo alikuwa amepoteza utu wake ndio sababu anakaa kama bepari chomboni. Mwandishi ametumia safari hii ya utu kijazanda ili kuwamlikia wasomaji athari ya ukosefu wa utu kwa wengine. Katika safari hii ya utu mwandishi anasema kuwa, walisafiri kwa Trimi chombo ambacho ni zao la utafiti unaozingatia utu. Katika safari hii Dzombo aliona mandhari ya kupendeza. Anasema:

> ‘‘Machoni mwake, aliona ulimwengu wa kupendeza na kujidhihirisha kwa kujitandaza na kuinuka kwa kila sehemu. Vijiji, miji, mashamba, viwanda mbuga, misitu, mabonde, vijito; bahari na pwani vilijitandaza hapa. Kulikuwepo na mabustani yaliyokuwa na kila aina ya matunda. Mbuga zilijieneza huku, hapa na pale zikivunjwa na vilima vidogo vidogo vilivyokaa kama nondo za mwari chipukizi. Katikati yao, kulitiririka vijito vya maji safi meupe.’’ (uk.57)

Dondoo hili linaonyesha mandhari ya kuvutia ya kijani kibichi, misitu, vijito, mabustani ya matunda ya kila aina na zaidi ya hayo, vijito vyo maji safi meupe yanayotiririka milimani na misitu mikubwa ya asilia. Mkangi anatuonyesha mandhari haya ya kuvutia ambayo ni zao la utu wa wanajamii ambayo ni tofauti sana na mandhari katika jamii ya Dzombo yenye ubinafsi na ulafi kutoka kwa watawala. Dzombo anamweleza Mtu-Bint Fikirini msiba uliopitia misitu

na mapori yao kuwa, wale wenye uwezo, badala ya kueneza stima kwa kila mwananchi, moto huo ukawa nadra kwa wengi - hasa akina yakhe, haidhuru ni wa mashambani ama wa mijini. Bei zilipanda kila siku na kuwabagua wengi kwa kuwanyima uwezo wa kugharamia moto na mahitaji muhimu. Pia, hawa wachache wakaingilia biashara ya makaa na kuni wakiuzia hawa wengi duni. Matokeo ya haya ni kuwa misitu na mapori yalifyekwa na majangwa kupanuka (uk.106).

Kutokana na maelezo ya Dzombo tunaonyeshwa majangwa ambayo yanatokana na kufyekwa kwa misitu asilia. Kwa sababu ya utu wa Walenisi, wanatia bidii katika kuhifadhi mazingira yao ili yawafaidi wote ilhali kwa sababu ya ubinafsi wa watawala Wachuna, wao wanakata misitu kwa manufaa yao ya kibinafsi. Kutokana na maelezo haya Mkangi analenga kuwazindua wasomaji waone umuhimu wa misitu ambayo ndiyo chanzo cha maji safi ya kutumiwa na binadamu wote na huo ndio utu. Mazingira ya kijani kibichi nayo yanavutia sana na huleta hewa safi inayohitajika na binadamu. Haya ndiyo mabadiliko aliyolenga Mkangi katika nchi yake ambapo misitu ya asili imekatwa na matajiri wakichoma makaa ya kuwauzia maskini wasiomudu bei ya stima. Pia misitu imenyakuliwa na mabwenyenye wasio na utu na kuifanya mali yao ya kibinafsi. Mkangi analenga kuwazindua wasomaji dhidi ya uharibifu wa mazingira ili nao wapapatike katika juhudi za kupigania upanuzi wa misitu, hifadhi yake na iliyonyakuliwa irudishwe na huu ndio utu.

Dzombo na wenzake wanapokuwa safarini, wanakumbana na matatizo kadha. Kwanza, kubadilika kwa hali ya hewa na kupigwa na hewa ya moto. Joto lenyewe lilizidishwa na mwendo wa kasi wa trimi kiasi kwamba kupumua kulikuwa kwa taabu. Hali hii inasababisha kiu ajabu, kukauka kwa midomo, damu kutokota na ulimi kugandama kaakaani (uk. 54). Dzombo na wenzake wanaumizwa pakubwa na joto hili. Mara kituo cha kwanza wanatupiwa maji na watoto lakini badala ya Dzombo kuwagawia wenzake, anayanywa na kujimwagia yaliyosalia. Hii ni jazanda ya mtu ambaye ni mchoyo na amejawa na ubinafsi. Mambo yalikuwa vilevile katika kituo cha mikate na mablanketi. Wenzake wanaumizwa na njaa ilhali yeye anateuka kwa shibe. Anapopewa mablanketi matatu ya kujisetiri na baridi kali, anajifunika yote kutoka kichwani hadi unyayoni bila kuwajali wenzake. Kutokana na kitendo hiki cha Dzombo cha ubinafsi, uchoyo na ukosefu wa utu, wenzake wanaathirika pakubwa sana mwishoni wa safari ilhali yeye anarudi ametuna kama beberu. Dzombo alichukulia kuwa, misaada yote aliyopata alipokumbana na shida zote safarini ilikuwa ni kwa sababu alikuwa na bahati. Alijua kuwa wenzake hawakupata msaada katika shida walizokumbana

nazo safarini kwa sababu hawakuwa na bahati maishani na hivyo hakuona sababu ya kuwagawia zao la bahati yake.

Baada ya safari ya utu Dzombo alijiangalia kiooni na kupata kuwa alikuwa na sura ya kupendeza na ya kuvutia na mwenye kiwiliwili kilichojengeka ingawa safari yenyewe ilikuwa ya matatizo mengi na ya kumchosha sana. Kwa upande mwingine, wenzake walikuwa wamedhoofika sana. Dzombo anaeleza hali mbaya ya Mtu-Bint Fikirini. Anasema:

> ‘‘Lakini siye huyo aliyemuona mwisho wa safari cyao. Aliyemwona alikuwa kinyanya kikongwe. Aliona Mtu-Bint Fikirini ambaye nywele zake zilikuwa zimetimka tifutifu, na macho ya kufifia yaliyojishindilia bupuruni.. uso haukuwa uso tena bali bupuru tupu. Masikio yakiwa yamekuwa ya kipopo na ngozi ikawa imeshirai na kukwajuka. Maskini Mtu-Bint Fikirini, safari ilikuwa imemmaliza’’ (uk. 62).

Sura ya mhusika huyu mwishoni mwa safari ilimtia simanzi Dzombo na mawazo yake yakamwelekeza kufikiria juu ya safari hii. Safari ilimzindua Dzombo na akaanza kujiuliza maswali yafuatayo: Nini maana ya safari hii? Kuna maana gani kuhusu visa vya watoto majukwaani? Kwa nini huduma zilionekana zikimtokea katika nukta ya mwisho ya kukata tamaa? Bahati mbaya za wenzake na kudhoofika kwao? Na maswali mengine mengi. Alianza kuingiwa na utu kwa kujilaumu kwa kuikuta kutoa jawabu la kidunia alipokuwa akibahatika pekee na wengine kukosa. Alianza kuhisi kuwa kama isingekuwa yeye safari hiyo haingekuwa imetungwa. Kwa sababu hii, bahati hii mbaya ya Mtu-Bint Fikiri, kiini chake ni yeye. Alizidi kujilaumu kwa kumpotezea mtoto wa watu maisha yake. Mguno wa huzuni ulimtoka bila yeye kujua.

Ni wazi kuwa sura mbaya ya Mtu-Bint Fikirini mwishoni mwa  safari inasababishwa na ukosefu wa utu na ubinafsi wa Dzombo. Mkangi alilenga kuonyesha kuwa binadamu anyimwapo utu na wengine huathirika sana. Mkangi alionyesha Dzombo athari hii ili kumfunza umuhimu wa utu. Mtu Dzombo aliweza kutambua athari hii ya ukosefu wa utu kwa sababu alikuwa amezinduka na kurejelewa na utu wake. Haya ni kwa mujibu wa Nadharia Amali.

Kwa muhtasari, ingawa safari ya utu ilikuwa na mateso mengi, inamfahamisha Dzombo ushirikiano, umuhimu wa utu na matumizi bora ya ardhi kwa manufaa ya wote. Pia, inamfahamisha njia za usafiri miongoni mwa mengine. Safari ya utu inamfunza Dzombo

mengi ambayo yangemzaidia kurejelewa na utu wake na kuleta maendeleo huko kwao jehanamu.

Jazanda ya safari ya utu, ni kichocheo cha zinduko kwa wasomaji. Maendeleo makubwa aliyokumbana nayo Dzombo katika safari hii ambayo ni zao la utu ni mambo ya kuigwa na jamii ya msomaji. Mkangi anashadidia kuwa ili maendeleo yafikiwe na jamii, ni lazima wawe na utu, mapenzi na usawa kati yao. Aidha, anawafahamisha kuwa ubinafsi ni adui katika maendeleo ya nchi. Haya maendeleo yatafikiwa kupitia mfumo wa ujamaa aliouenzi sana Mkangi.

**4.2.5 Uchawi, Moto na Mabavu**

Maneno uchawi, moto na mabavu yametumiwa na Mkangi kijazanda ili kusimamia koo tatu kuu za Wachuna. Hizi koo ndizo zilizoshika hatamu za uongozi katika enzi za Wachuna. Aidha, hizi koo za kichuna ziliweza kuzuka kutokana na ujanja tofautitofauti. Baada ya kuchipuka kwa koo za kichuna, kitu muhimu cha kwanza walichokisisitiza ili waweze kudumisha uchuna wao, kilikuwa ni kutumia ule ulaghai uliosema kuwa ati hawakuwa watu wa kawaida. Wengi walisema asili zao si za kibinadamu. Wengine wakajitia kusema ati hata damu zao hazikuwa nyekundu bali bluu. Waliapa kuwa kuzaliwa kwao hakukuwa kwa kawaida, kwa hivyo, hawakuwa na mama na baba sembuse babu na nyanya? (uk. 167).

Kila ukoo ulikuwa ukiwakilisha dhana mbalimbali. Kwanza, uchawi ni jazanda iliyowakilisha uganga, dini na sayansi. Kisa kilichozua Wachuna wa ukoo wa uganga, kilitokana na mtu mmoja aliyejulikana kwa jina la mchawi. Siku moja akiwa kichakani amechutama kwa haja kubwa, aliona bafe na chatu wakipindana. Baada ya chatu kuumizwa na bafe, chatu alijikokota hadi chini ya mti mmoja na kuanza kuchimbua, kuvunja mizizi ya mti huo na kuimeza. Pia akaona chatu akibambua maganda na majani ya mti huo kuyakata, na tena vyote hivi kuvimeza. Kufumba na kufumbua, chatu akawa haonekani. Baada ya chatu kutoweka haraka mchawi alifyatuka hadi shinani pa mti ule ili kuchimbua mizizi, kubambua maganda na kuchuma majani yake kisha kuelekea kwake. Hazikupita siku nyingi kabla ya jirani wa mchawi kuumwa na bafe. Kama ilivyokuwa desturi, watu walianza kumchimbia kaburi kwa sababu hakukuwa na dawa ya kutibu mtu aliyeumwa na nyoka. Mchawi alijitokeza na kumtibu kwa kutumia yale matawi, maganda na mizizi ya mti ule aliyotumia bafe kujitibu. Baada ya matibabu, mgonjwa mahututi aliweza kupona kabisa. Kutokana na kisa hiki sifa za uganga zikaenea kwa urefu na mapana (uk. 161).

Baada ya sifa za mchawi kuenea kwa mapana na marefu alianza kutishia kuwa, hangeweza kuendelea kutoa huduma za matibabu kwa kuwa ilimbidi naye pia aende kwake makondeni. Kwa sababu watu walikuwa wanamhitaji zaidi walimhakikishia kuwa watamlisha. Kutokana na ujanja huu mchawi aliweza kujilimbikizia mali nyingi. Mwandishi anasema:

> ‘‘Basi, ziada zikarundikana kwake na punde si punde, utajiri huo ukamtia hisia za kifalme, utukufu na mjua yote. Kama moto, akarithisha watoto wake wa kiume tu siri hii. Aliwalisha kiapo ili wasiitoe kwa mtu ama kwa ukoo, mwingine aslani’’ (uk.162).

Kutokana na maelezo haya ya mchawi, mwandishi anaonyesha ubinafsi wa hali ya juu. Mkangi alitumia jazanda hii ya mchawi akidhamaria kuwazindua wasomaji na jamii yake dhidi ya ubinafsi wa waganga, viongozi wa dini na wanasayansi. Mkangi analenga kuwafahamisha kuwa waganga, viongozi wa dini na wanasayansi hutumia ujanja na hila ili kujinufaisha wenyewe kutoka kwa wanyonge na kila wakati hujaribu kuficha siri hiyo isijulikane na watu wengine ila tu jamii yake. Pia Mkangi ametumia jazanda hii kiuamilifu ili kuwafahamisha hawa viongozi wa dini, wanasayansi na waganga kuwa ujanja wao unajulikana na kwa sababu tunawahitaji anatoa wito kwao waache kutumia ujanja huu kuwalaghai wanajamii wenzao kwa kujilimbikizia mali huku wanyonge wakiendelea kusononeka.

Pili, moto ni jazanda inayowakilisha ufundi, uhandisi na teknolojia. Ukoo huu wa moto ulianzishwa na mtegaji mmoja wa kulungu aliyejulikana kama moto. Siku moja akisubiri kulungu aliowatega wanaswe, alionelea atumie wakati huo kumtegenezea utandu mpenzi wake. Wakati huo jiwe na mti ndivyo vilikuwa malighafi. Moto alikata vijiti viwili na kuanza kupekecha kimoja juu ya kingine akidhamiria kutoboa matundu mengi, halafu ayakate na kuyaunga na uzi wa maua ili apate huo ushanga. Akizidi kupekecha kwa nguvu, cheche zilianguka juu ya majani makavu yaliyokuwa katikati ya mapaja yake na kwa ghafla majani yalichomeka na kuona moshi ukitoka. Alishtuka na kuruka kwa woga kwa sababu hakuwa ameshawahi kuona kioja kama hiki maishani. Cheche zilisambaa kwa haraka na kuwasha majani, nyasi na miti. Aliweza kuwashtua wengi na wakataka kujua alipata uwezo huu wapi. Hakuwaambia ukweli badala yake, aliwaambia ati ni malaika ndiye aliyemtunukia uwezo huo. Watu walizoea moto lakini aliwapa masharti kuwa moto uzimwe mara moja baada ya matumizi na hapo kwake tu ndipo moto mpya ungeweza kupatikana. Aliwatahadhaharisha kuwa moto hauibiki wala haufichiki na yule ambaye angefanya ujasiri wa kuibua ama kuficha, basi asije kulia baadaye.

Masharti haya yalifuatwa, akawa mgawaji wa moto pekee. Uwezo huu ulimtia hisia za ukubwa na punde si punde utukufu pia. Wakamtegemea yeye kwa sababu bila yeye hakukuliwa kitu. Ili kulinda moto huo kila mtu alikubali kumpa theluthi ya chakula chake na Moto akapata uwezo wa kurundika ziada. Siku si nyingi, mkewe na watoto wake wakawa hawana haja ya kufanya kazi (kur. 154-158).

Hivi ndivyo ukoo wa moto ulivyozuka na kujipatia utukufu, uwezo na hekima kwa kutumia hila zilizoweza kuwapa utawala juu ya wenzao na kuwala jasho lao. Mkangi ametumia jazanda hii kiuamilifu ili iwe kama kichocheo cha zinduko kwa msomaji na jamii yake kwa kuwamulikia jinsi ambavyo watawala hutumia ufundi, uhandisi na teknolojia kuwanyonya watawaliwa. Mkangi analenga kuwaambia watawaliwa kuwa, watawala hutumia ujanja na hila za kiufundi, kiuhandisi na kiteknolojia ili kuwafanya wawe wahitaji kila wakati na hivyo kufaidika kutokana na jasho la watawaliwa.

Tatu, mabavu ni jazanda aliyotumia Mkangi kuwakilisha uwezo, nguvu, vyeo na madaraka. Mwanzilishi wa ukoo huu wa mabavu alikuwa mwindaji mwenye sifa nzuri za ushujaa. Ingawa mabavu alikuwa jasiri na mwenye sifa nzuri hakupendwa na msichana mrembo aliyemtamani. Kupitia kwa ujanja Mabavu aliweza kumuoa msichana huyu mrembo. Alizidi kutumia ujanja huo huo na akajipatia wasichana warembo wote. Kwa hofu, watu hawakukosa kumjia wakitafuta ulinzi kwa kumpatia binti zao. Kwa kuongeza ujanja wake ilifikia wakati ambao haulizi wasichana tena ili awaoe, bali kujipa jukumu la kuwabikiri tu ili wazazi wao waweze kupata ulinzi wa simba. Punde si punde, ikambidi kulazimisha apewe chakula kama fidia ya ulinzi ili aweze kulisha jamaa na wafuasi wake. Sheria akatunga na watu wakalazimishwa kuitikia, huku wakilala kifudifudi mavumbini na macho kuyabwaga (kur. 162-166).

Mkangi alitumia jazanda hii ya mabavu akiwa na lengo la kuwafahamisha wasomaji wa riwaya hii jinsi viongozi hutumia ujanja kuwalaghai wanajamii ili kupata vyeo, madaraka, nguvu na uwezo. Mkangi anadhamiria kumzindua msomaji na jamii yake kuwa na ujasiri ili kuwapinga viongozi hawa laghai na kuleta mabadiliko katika uongozi wa jamii yao.

Kwa jumla Mkangi ametumia jazanda ya mchawi, moto na mabavu akilenga kuwazindua wasomaji na wanajamii kuwa, viongozi katika jamii yake wametumia ujanja na hila ili kumiliki uchumi wa ulimwengu huu huku wakitumia siasa zilizolingana ili kudumisha utawala wao. Kwa ujanja wao mwingi, wanajamii wengi wamepoozwa kimwili na kiakili. Si mke wala mume, thamani yao imekuwa ni kusubiri ili wawahi kufanyishwa kazi na viongozi.

Kwa wengi subira zao zimekuwa sawa na mvuke wa ndotoni. Miaka nenda miaka rudi, hao wamezaliwa na kufa wakiwa katika mazigazi haya ya subira. Nao viongozi kwa kusisitiza kuwa kazi ni bahati ya wachache, wamefaulu kumvua binadamu utu wake na kumpiga bei kama ndazi. Aidha, Mkangi analenga kuwafahamisha wasomaji na wanajamii wengine kuwa, viongozi wameweza kuzika mizizi ya utawala wao kwa kuotesha mambo matatu nyoyoni na akilini mwa watawaliwa. Nayo yamekuwa: ulafi, ujinga na uoga. Nayo kama mafiga yamejishikanisha na kusaidiana ili kwamba haijakuwa rahisi kuyatenganisha ili mtu kutambua lipi ni lipi. Kwa kuwafahamisha haya yote mwandishi anawachochea wasomaji na jamii yake kupanga mapinduzi katika uongozi huu dhalimu na kuleta mabadiliko katika jamii yake. Anatarajia ujenzi wa jamii mpya yenye usawa na haki kwa kila mwanajamii na haya yatapatikana kupitia kwa mapinduzi.

## 4.3 Istiari

### 4.3.1 Vijana Kulinganishwa na Nzige na Makapi

Nzige kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifuni* (2013) ni mdudu aina ya panzi lakini mkubwa na anayesafiri masafa marefu kwa makundi na huharibu mimea. Wadudu hawa wana uwezo mkubwa wa kuharibu mimea kutokana na wingi wao. Mwandishi anatumia istiari hii ya kulinganisha vijana na nzige kimafumbo akikusudia kuwasilisha maana pana zaidi ya ile inayobebwa na neno lenyewe. Kwanza, Mkangi analinganisha vijana na nzige ili kuonyesha kuwa idadi yao ni kubwa. Jinsi ambavyo nzige huwa na idadi kubwa, kiuhalisia pia idadi ya vijana ni kubwa duniani ikilinganishwa na wazee. Tukiangazia jamii ya Walenisi idadi hii kubwa ya vijana ndiyo inayosababisha kupewa jukumu la pekee katika jamii yao. Pili, Mkangi anadhamiria kuonyesha kuwa vijana wana uwezo mkubwa kwa kila jambo kuliko wazee. Tunapoangalia katika jamii ya Walenisi tunaona kuwa vijana ndio wanaofanya kazi na kwa sababu wa uwezo wao mkubwa wamefaulu kuzalisha chakula kinachotosha jamii yote. Ili kudhihirisha uwezo wa vijana Mtu-Binti Hekima, anamwambia Dzombo:

> ‘‘Sasa njoo ushuhudie mwenyewe uwezo wa vijana-chipukizi waliozinduka kwa kukubali kutorudi nyuma ili wawe magugu ya wengine wachache wenye nguvu’’ (uk. 108).

Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa vijana wana uwezo mkubwa. Mwandishi ametumia jazanda hii ili kuwazindua wasomaji vijana kuwa wana uwezo mkubwa na hivyo, wanahitajika kushiriki kikamilifu katika kuleta mabadiliko kwenye utawala dhalimu. Aidha,

Mkangi anawafahamisha vijana kuwa viongozi hudhamiria kuwatumia vibaya ili kujinufaisha wenyewe. Kwa hivyo, anawazindua vijana kuwa, wasikubali kutumiwa na viongozi dhalimu ili kujinufaisha kwa sababu ya uwezo wao mkubwa lakini anawahimiza kutumia uwezo ili kunufaisha jamii yote. Haya yanadhihirika pale ambapo Bint Nena anamwambia Dzombo kuwa, kutokana na juhudi za vijana, hakuna Muwalenisi hata mmoja alalaye na njaa (uk. 114). Tatu, Mkangi ametumia istiari ya kulinganisha vijana na nzige ili kumaanisha kuwa, aghalabu katika jamii yenye mfumo mbaya wa utawala vijana huharibu kwa wingi mahali ambapo hawajafanya kazi. Mwandishi analenga kumzindua kijana msomaji kuwa badala ya kutumia uwezo wake mkubwa kujaribu kuharibu vya wengine, anafaa kujiingiza katika utafiti kwa sababu utafiti ndio njia pekee iliyoko imwezeshayo binadamu kuyahama maumbile kwa manufaa yake. Kwa sababu ya wingi wao Mkangi anawahimiza vijana kujimiliki wenyewe kupitia kwa kujadiliana na kupanga kazi zao ili kila kijana atekeleze jukumu lake bila kuwa na nyapara.

Aidha, katika enzi za utawala wa Wachuna vijana wanalinganishwa na makapi. Vijana kulinganishwa na makapi ni istiari ya kuonyesha kwamba, viongozi hawakuona faida yoyote inayoweza kuletwa na vijana ndiposa wengi wakaishia magerezani. Wakati huo vijana hawakuwa na faida kubwa kwa jamii isipokuwa kuchukuliwa kama wazushi wa bughudha za kiuchumi. Vijana wanaume wao nguvu zao ziliishia katika uasherati hali wasichana wao, nguvu zao zikaisha katika umalaya. Aidha, vijana hawakupewa fursa ya kuzalisha mali, kwa hivyo basi, wengi wao, walipevuka kuwa majangili, wakora na kumalizikia magerezani na kufia huko. Mwandishi anasema:

> ‘‘Na kama makapi, waliteketezwa kwa moto wa marisau, ulevi, na magonjwa ya zinaa kama ukimwi na madawa ya kulevya… Vijana wenyewe hawakugundua kutumiwa kwao vibaya kwa makame. Lakini siku walipozinduka babee. Mbona Wachuna walitafuta pakujificha na wasipaone’’ (uk. 108).

Hii ni jazanda inayomsikitisha msomaji sana kuhusu vijana ambao wanafaa kuwa rasilmali muhimu katika jamii. Kwa sababu ya itikadi potovu kwamba vijana ni viongozi wa kesho sio wa leo, vijana hawakuweza kushirikishwa katika maendeleo ya nchi. Wengi wao waliishia kujitumbukiza katika wizi, umalaya, ulofa na matumizi ya dawa za kulevya. Mkangi alidhamiria kuwazindua wasomaji wake wafahamu kwamba vijana ni kundi muhimu sana katika jamii na wasipuuzwe bali wapewe nafasi kutoa mchango wao katika maendeleo ya nchi. Aidha, mwandishi anawachochea vijana kuandaa mapinduzi kwa mfumo wa utawala

unaowadharau vijana na kujenga jamii mpya ambayo itathamini vijana kama viongozi wa leo wala si wa kesho. Kwa kushadidia lengo hii lake-umuhimu wa kupanga mapinduzi, Mkangi anaonyesha vijana Walenisi jinsi ambavyo walianza kushirikiana kazini baada ya mapinduzi. Dzombo anasema:

> ''Kwa hivyo, alikuwa ameona wasichana na wavulana bega kwa bega wakipalilia, kunyunyuzia maji, samadi na dawa. Kila aliyemwona hakuwa goigoi, bali alikuwa akitokwa na jasho la kikweli, huku akisherehekea kazi yake. kwa vijana hawa, kazi ilichukuliwa kama sherehe sio kama girimiti-kazi ya kulazimishwa'' (uk. 117).

Kutokana na maelezo haya Mkangi anajaribu kuonyesha umuhimu wa mapinduzi katika mfumo wa utawala usiowathamini vijana katika jamii. Anajaribu kuonyesha kuwa jamii ambayo huthamini vijana, hawa vijana hujitolea katika kufanya kazi na matokeo yake ni kuzalisha chakula ambacho kinawatosha wanajamii wote kwa sababu vijana wana uwezo mkubwa. Mkangi analenga kuwahimiza vijana kushirikiana na kuwajibika kazini.

### 4.3.2 Madaktari Kulinganishwa na Hirizi za Viunoni

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004), hirizi ni kitu cha kuvaa mwilini kama vile karatasi iliyo na maandishi maalumu, kipande cha mti au uganga uliofungwa kwenye nguo au ngozi. Wakati wa Wachuna, Mkangi anajaribu kuonyesha kuwa, kulikuwa na matabaka mawili makuu: matajiri na maskini. Ili kuonyesha uhusiano uliokuwa kati ya madaktari na tabaka la matajiri hata baina ya maskini na madaktari, Mkangi ametumia istiari ya kulinganisha daktari na hirizi za viunoni. Anasema kuwa:

> ''Kila Mchuna hakukosa kuwa na daktari wake wa kibinafsi. Huyu, alimtibu kwake nyumbani na hata akiwa Nokolani. Kwa Wachuna, madaktari wa kibinafsi walikuwa kama ndio hirizi zao za viunoni'' (uk. 178).

Mwandishi katika kulinganisha madaktari wa kibinafsi na hirizi za viunoni ni istiari inayoashiria kule kutobanduka kwao na wateja wao ambao ni wa tabaka moja. Ili kudhihirisha haya mwandishi anasema kuwa, mama Muchuna alikuwa na mkunga wa kibinafsi. Huyu ndiye aliyemshauri na kumwandama tokea mwezi wa kwanza wa uja uzito mpaka mtoto kuzaliwa. Ilikuwa pia, baada ya kuzaa tu yule mzazi mumo humo Nokolani, kuna chumba cha kumrembesha kabla ya bwanake kumjia. Kwa akina mama wa Kichuna, kupata na kumpendeza mume kulizidi kuzaa na kumlea mtoto.

Mkangi ametumia istiari ili kuwazindua wasomaji kuhusu kuwajibika kwa madaktari wa kibinafsi. Analenga kuwachochea wasomaji na jamii yake kwa jumla kuwa, ikiwezekana kuwa na daktari wa kibinafsi anaweza kukusaidia kuliko madaktari wa umma. Pia, alitumia istiari hii akilenga kuwazindua madaktari wa umma kuwajibikia kazi zao kama vile madaktari wa kibinafsi wanawajibikia kazi yao.

Kupitia kwa kisa cha mapacha na watoto wao wasomaji wanafahamishwa kuwa, ukweli wa istiari hii hutokana na matabaka yaliyokuwepo wakati wa utawala wa Wachuna. Tabaka la matajiri, kwa sababu ya uwezo wao wa kuweza kumudu kuwa na madaktari wa kibinafisi, waliweza kuhudumiwa vizuri ilhali tabaka la maskini ambao hawakuweza kugharamia matibabu ya kibinafsi wengi walikufa kwa sababu ya kukosa kuhudumiwa. Mwandishi anadhihirisha haya anapotwambia kuwa baada ya daktari wao kumhudumia Furaha vizuri anawaaga kwa kusema kuwa ‘‘Nitawatembeleeni kesho asubuhi nione amelalaje; lakini ikiwa kutatokea mabadiliko yoyote, msikawie kunipigia simu’’ (uk. 186). Kwa upande mwingine mwandishi anatuambia kuwa kwa sababu ya umaskini Tabu hakupatiwa matibabu hata ingawa alikuwa hali mahututi bali aliambiwa na muuguzi kuwa, ‘‘ Hawezi kulazwa bali mama alihimizwa amrudishe nyumbani na ajaribu tena keshoye’’ (uk. 185).

Kupitia kwa kisa hiki cha mapacha na madaktari, msomaji anapatwa na hisia za huruma kwa wagonjwa maskini ambao hawapati huduma kwa sababu ya umaskini wao. Mkangi anatumia istiari hii akishadidia ukweli wake na kisa cha mapacha akilenga kuwachochea wasomaji na jamii yake wazinduke na kupigania usawa. Aidha, Mkangi analenga kufichua tabia ya baadhi ya madaktari, wauguzi na wafanyakazi wa umma ambao hawafanyi kazi zao kwa dhati na kutoa wito kwao ili wawajibike kazini.

Aidha, kwa kutumia istiari hii ya kuonyesha kuwa madaktari wa kibinafsi hawakubandukana na wateja wao, Mkangi analenga kuwafahamisha wasomaji madhara ya kitendo hiki chao kwa wateja wao. Anasema kuwa kwa sababu ya kupatiwa malipo ya juu kwa uzazi wa upasuaji, waliwafanya akina mama hawa waja wazito kuamini kuwa pale mtoto alipotungiwa sipo atakapotokea. Kwa sababu hii, wengi wakaambukizwa na ugonjwa wa kuzaa kwa kupasuliwa matumbo yao. Ili kuchelea kukosa fidia ya juu kwa wengine kujifungua kikawaida, aghalabu madaktari waliwashona misamba akina mama ili keshoye wawazalishe kwa matumboni. Hivi ndivyo kuzaa kulivyogeuzwa na madaktari hawa wa kibinafsi kutoka kuwa jambo la kawaida na kuwa ugonjwa (uk. 178). Mkangi analenga kuwazindua wasomaji wake kujitahadhari na ubinafsi wa madaktari wa kibinafsi ambao hutumia unafiki wao ili

kujinufaisha bila kujali utu wao. Anahimiza madaktari na wauguzi kutoifanya afya kuwa chombo cha biashara bali iwe ni huduma ya kiutu kwa wote wanaohitaji huduma hiyo. Haya yatatokea tu katika jamii ambayo haina matabaka na mfumo wa utawala unaozingatia haki na usawa kwa wote.

### 4.3.3 Binadamu Kulinganishwa na Popo

Popo ni mnyama mdogo kipofu mwenye mbawa anayefanana na panya, hupenda kula matunda na wadudu na kuruka usiku (TUKI, 2004). Kule kulinganisha binadamu na popo ni istiari ambayo aliitumia Mkangi kurejelea vitendo vya Wachuna. Mkangi alitumia istiari hii kimafumbo kuwakilisha mambo kadhaa katika enzi za Wachuna na jinsi yanavyojidhihirisha katika jamii yake. Kwanza, Mkangi alitumia istiara hii ili kuonyesha kuwa Wachuna watawaliwa wote waligeuzwa na kuwa vipofu. Kwa sababu ya propaganda za mfumo wa utawala wa Wachuna wenye matabaka, watawaliwa walifumbwa macho na kushindwa kuona uhalisia wa mambo. Watawala dhalimu waliwafanya wanaowatawala kuamini kuwa yanayotokea katika maisha yao, yawe mabaya au mazuri ni kwa kudura ya mwenyezi Mungu na hayafai kupingwa. Mwandishi anasema kuwa wakati wa utawala wa Wachuna, watawala walinyakua udongo na kumiliki na kuwafanya wengine wahoihoi. Kutokana na kitendo hiki waliwafanya watawaliwa kuamini kuwa, kula kwategemea bahati ya Mungu tu na binadamu hataishi kwa mkate peke yake. Pia, watawaliwa walifanywa kuamini kuwa, matibabu hayawezekani kwa kila mtu bali itategemea uwezo wa kifedha wa mtu binafsi. Asiyekuwa nao, bahati yake mbaya. Aidha, waliamini kuwa, kazi ni adimu, mtu lazima apate wa kumwajiri akiwa na bahati. Lazima atumikishwe. Kazi ni bahati nasibu wala siyo ya kuadhimisha ubinadamu (uk. 173). Mwandishi anasema:

> ‘‘Lakini tu mapopo. Na ndani ya kiza kikuu tunamoishi, hatuwezi kuona dhuluma kati yetu. Hatuwezi kunusa uvundo wa magonjwa ya kitabaka kati yetu. Hatuwezi kusikia mayowe ya njaa na umaskini kati yetu. Hatuwezi… tutaweza vipi…?’’ (uk.141).

Kutokana na maelezo haya mwandishi anaonyesha kuwa watawaliwa wamefumbwa macho na watawala wao na kwa jinsi hiyo, hawawezi kutambua jinsi ambavyo wananyanyaswa na kudhulumiwa. Mkangi ametumia istiari hii akilenga kuwazindua wasomaji na jamii yake kwa jumla ili waweze kuchunguza vitendo vya viongozi wao wakiwa na lengo la kupigania haki zao. Analenga kuwazindua wasomaji kwa kuwatahadharisha kuwa, wasipofushwe na propaganda wanazotumia viongozi wabinafsi ili kuwanyonya na kuwadhulumu.

Pili, Mkangi alitumia istiari hii kuonyesha jinsi mambo yalivyokuwa kinyume na matarajio wakati wa utawala wa Wachuna. Watawala waligeuza mambo na yakawa kinyume ili wao wenyewe waweze kujinufaisha huku watawaliwa wakiendelea kuteseka. Mwandishi anasema kuwa enzi za Wachuna lililokuwa kubwa ni lile lililomfanya mjinga kuonekana mwerevu na mwerevu kuonekana timamu; muuaji kuonekana mlinda usalama; msema ukweli kuwa mwenda wazimu; na busara kutoka kwa wasaliti (uk. 13). Ni katika harakati hii ya kudumisha upopo huu ndiko kulikomchongea hata yeye Dzombo akatokomezwa. Naye kwa ghafla akatambua kuwa kwa vitendo na matamshi yake hayakuwa ya kutisha hata hivyo, kwa uchache wake aliyasema akiwa katika imani ya kutaka kupindua upopo huu utawalao duniani. Kutokana na maelezo haya mwandishi anajaribu kuonyesha jinsi ambavyo watawala walivyotumia ujanja kwa kugeuza mambo ili kuendelea kujisitiri uongozini. Ili kueleza hali ya mambo enzi hizo, mwandishi anasema:

> ‘‘ Na kama popo, tunaishi kichwa chini miguu juu. Kwani hizi ni mbio za sakafuni nazo zinaishia pale pale ukingoni kaburini. Na kama popo tutaunguka kama jani kavu na kuwa mbolea. Popo angetambua ukweli huu, angejinasua kutokana na laana hii… lakini atawezaje akiwa kichwa chini nyayo juu? Kumpindua ili awe akisimama sawa sawa si mchezo kwa kuwa ana meno makali, masikio mapana na kujikinga ndiyo asili yake…’’ (uk.141).

Kutokana na maelezo haya mwandishi anatuonyesha jinsi mambo yalivyo kinyume cha uhalisia katika jamii. Mkangi ametumia istiari hii ya popo kuishi kichwa chini miguu juu akilenga kuwazindua wasomaji na jamii yake kushirikiana katika mapinduzi dhidi ya mfumo dhalimu wa utawala kwa sababu si rahisi kuleta mapinduzi kama ilivyo vigumu kupindua popo asimame sawasawa kutokana na meno yake makali, masikio mapana na kujikinga kwake.

Aidha, Mkangi alitumia istiari hii ya popo ili kuonyesha jinsi binadamu amejipunguzia hadhi kwa kuthamini zaidi mali wailundikayo na vyombo waviumbavyo, wamevipa roho zao na wamekoma kuwa binadamu. Yaonekana ubinadamu wao unategemea kabisa kusujudia vitu vya mikono yao. Duniani, binadamu ametoa roho yake na akaitia ndani ya vitu vya mikono yake na huku yeye akichukua ‘roho’ ya hivyo vitu vya mikono yake na kuvifanya kuwa ndiyo roho yake. Mwandishi anasema:

> ‘‘Binadamu ameshakuwa popo. Si mnyama wala si ndege; si chombo wala si mtu… makubwa. Robo mnyama, robo ndege, robo kitu na robo mtu… kiumbe gani hiki? … ndiposa tunaumizana. Ndiposa tunachukiana. Ndiposa tunatesana. Ndiposa tunamalizana. Ndiposa tunachinjana ingawaje hatulani nyama… wanyama afadhali basi? … Hatuko kamili.’’ (uk. 140).

Kutokana na dondoo hili ni wazi kuwa Mkangi alitumia istiari hii ya popo ili kuonyesha jinsi binadamu amepoteza utu wake. Kwa hivyo binadamu amekuwa nusu mtu na nusu mnyama. Mkangi alitumia istiari kiuamilifu akilenga kuwazindua wasomaji wa riwaya hii ili waweze kurejesha utu wao na kuanza kuthamini binadamu wenzao zaidi kuliko mali yao au vyombo waviundavyo. Aidha, alilenga kuwazindua wasomaji wake kuwa ukosefu wa utu huzorotesha uhusiano mwema baina ya binadamu. Anatoa wito kwa jamii kudumisha utu kwa sababu hili ndilo kusudio la Mungu alipoumba binadamu. Haya yote yanaafikiana na Nadharia Amali inayoeleza kuwa maana nzima ya wazo huonekana katika matokeo halisi, matokeo ambayo hujitokeza ama kama tabia nzuri za kufuatwa au tajriba inayotarajiwa iwapo hilo wazo ni sahihi.

### 4.4 Namna Ufumbaji Umeendeleza au Kukwamiza Usawiri wa Wahusika katika *Walenisi*

Majina aliyowapa Mkangi wahusika wake katika riwaya hii ya *Walenisi* yamejaa uzito wa yale waliyonayo na kuyasema. Ni kupitia kwa ufumbaji ambapo Mkangi aliweza kuwapatia wahusika wake majina ya majazi. Suala zima la umajazi linaoana na Nadharia Amali kwani majina ya majazi ni kama vile viashiria anavyotaja Morris katika Levinson (1983:2). Viashiria kama vile ah, oh, wuui, vina maana kulingana na muktadha wa matokeo yake na huashiria maana fulani. Vinapotumiwa basi huwa na uamilifu maalum. Wahusika wote katika ulimwengu wa Walenisi, majina yao huanza kwa jina ‘mtu’ na kufuatwa na mengine. Wahusika kama vile: Mtu-Maanani, Mtu-Mwenzio, Mtu-Bint Fikirini, Mtu-Wazo, Mtu-Bint Hekima na Mtu-Tabia, wote hawa Mkangi aliwapa majina yanayoanza na neno ‘Mtu’ kimakusudi ili kuwasilisha maana pana zaidi na nzito kuliko jinsi neno hilo linavyoonekana.

Katika kuelewa ni kwa nini wahusika hawa wakapewa majina yanayoanza na neno ‘Mtu’ inambidi msomaji kutazama vitendo vyao, mazungumzo yao na uhusiano baina yao. Dzombo alipofika katika jamii ya Walenisi baada ya kutokomezwa kutoka kwao duniani, alikaribishwa vizuri sana hata ingawa alikuwa ajinabi kwao. Mwandishi anasema kuwa, huku shikamoo

zikifyatuka kutoka kwa watoto na vijana, wenyeji wawili-mke na mume walijitokeza kuja kumlaki na kumsaidia kutoka mle chomboni. Wakawa wanamkaribisha na kuendelea kumpa pole kwa safari yake ndefu. Hirimu walimwelekeza kwenye jumba moja hapo hapo tu na kumwambia kuwa jishibishe na jinyweshe na chochote utakacho (kur. 37-38). Hiki kitendo cha kumkaribisha mtu ambaye hawakuwa wanamjua kinaonyesha kuwa, Mkangi anajaribu kuwafahamisha wasomaji kuwa wahusika wote katika jamii ya Walenisi ni wahusika wenye utu. Hii ndiyo sababu majina yao huanza na neno ‘Mtu’ ili kuashiria utu wao. Dzombo anadhihirisha hili anaposema kuwa, mwanzoni walipompokea walidhani yeye ni Mungu na alitoka duniani na ingawa sasa wanajua kwa kweli atokako ni Jehanamu, hawajabadili kumchukulia kwa wema mkuu (uk. 102).

Aidha, Mkangi alitumia mafumbo ili kuonyesha kuwa Walenisi walithamini utu zaidi kuliko vitu vyote na ndio sababu majina yao huanza na jina ‘Mtu’. Dzombo anapofika katika ulimwengu huu ajinabi na baada ya kukaribishwa, walimwandaa kwa safari ya utu. Safari hii ilidhamiriwa kumfunza Dzombo maana ya utu na kumwonyesha umuhimu wa utu katika maendeleo ya jamii. Safarini wenyeji wake Dzombo, Mtu-Bint Fikirini na Mtu-Wazo, walionyesha utu wa hali ya juu kwake. Mtu-Bint Fikirini ni mhusika ambaye anafikiria zaidi maslahi ya wengine kama alivyomfanyia mgeni wao Dzombo.

Hata ingawa Wawaleni si mhusika mmoja, ni wahusika wa kijumla ambao Mkangi amewatumia ili kupitisha ujumbe fulani kwa wasomaji. Walenisi ni neno linalotumiwa kimafumbo ili kumaanisha ‘‘Wale ni Sisi na Sisi tu Wale’’. Hawa ni watu ambao walikuwa na umoja usiobandukika. Ulimwengu huu wa Walenisi ni ulimwengu ambao ulikuwa na watu wataratibu, wanaopendana kikweli na wachangamfu. Walikuwa ni watu ambao yaonekana walikuwa wakijijua. Walijua wapi walikotokea na kulikuwa wazi kwao kabisa wapi walikokuwa wakielekea. Halikuwa jambo la pata shika. Ulikuwa ulimwengu wa watu huru. Katu usabasi, katu ugomvi, katu kuumizana, katu kuoneana, katu kupaparurana, katu kuzomeana, katu kudanganyana, katu kunyanyasana, katu kuibiana, katu wivu na katu ubarakala. Aidha, mwandishi anasema kuwa wahusika katika jamii hii ni watu waliozinduka na kujua kuwa maslahi yangu na mwenzangu hayabandukani (uk.146). Kupitia kwa taswira hii wahusika katika jamii ya Walenisi wanafahamika kwa urahisi.

Dzombo ni mhusika ambaye amechorwa kimafumbo. Dzombo ni jina la kilahaja ambalo linafaa kutamkika kama chombo katika Kiswahili Sanifu. Huyu ni mhusika ambaye hana utu hata kidogo kutokana na athari ya jamii yake yenye matabaka. Kwa hivyo, Mkangi alionelea

kuwa ni vyema kumpa jina chombo badala ya jina la kibinadamu kwa sababu hakuwa na ubinadamu wowote. Haya yanafahamika wakati ambapo wenyeji wake katika ulimwengu alioufikiria ndiko mbinguni walikuwa wakimdadisi ili kumfahamu kuwa yeye ni nani na alikuwa akitoka wapi. Walipomwita Mtu-Dzombo alikana kuwa yeye sio mtu bali yeye ni Dzombo tu (uk.40). Walipoenda katika safari ya utu ilifahamika kuwa hakuwa na utu bali alikuwa mbinafsi na ukosefu huu wa utu kwake kuliwafanya wenzake kudhoofika kiafya ilhali yeye akituna kama beberu. Aidha, Mkangi alitumia mafumbo kumsawiri kimafumbo anapotuonyesha namna alivyokaa ndani ya trimi. Mwandishi anasema:

> ‘‘Ungemwona, ungedhani umeona bepari la mabepari, jinsi vile alivyokuwa amejitenga pembeni- nyuma kabisa ya hicho kitumbwi, huku uso wake wote ukiwa tabasamu tupu’’ (uk.36).

Kutokana na dondoo hili ni wazi kuwa Dzombo ni mbinafsi na anawakilisha watu katika jamii ya mwandishi waliomiliki nyenzo za uzalishaji kwa manufaa yao wenyewe. Aidha, Dzombo alichorwa kimafumbo akiwakilisha chombo ambacho kinaweza kutumiwa ili kuleta mapinduzi na kusababisha ujenzi wa jamii mpya. Haya yanajitokeza mwishoni mwa riwaya baada ya kujifunza kuhusu maana na umuhimu wa utu anafunga ndoa na Mtu-Bint Fikirini na kuamua kurudi kwao duniani ili kuleta mapinduzi katika jamii yake.

Kwa jumla, mwandishi ametumia wahusika wake kimafumbo ili kutekeleza malengo yake ya kuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji. Hata hivyo, mwandishi hakufaulu kwa kuwa, wahusika wengi hawajapatiwa nafasi ya kutenda bali wameelezwa tu kimafumbo hasa wahusika katika jamii ya Dzombo. Aidha, kama ilivyo katika riwaya ya *Mafuta* wahusika walipewa lugha yenye kubeba maana nzito, kwa upande mwingine riwaya ya *Walenisi* wahusika wengi hawajapewa nafasi ya kutumia lugha ya mafumbo badala yake ni mwandishi ambaye ametumia lugha hiyo kuelezea visa mbalimbali.

### 4.5 Kiishilio

Sura hii imechunguza ufumbaji kupitia kwa taswira, jazanda na istiari. Katika kuchunguza mafumbo haya, utafiti huu umebainisha kuwa, Mkangi alitumia mafumbo kuwazindua wasomaji wake kuhusu athari za utabaka katika jamii. Licha ya uzindushi mwandishi alilenga kuwatolea wasomaji suluhu la utabaka ambalo ni mapinduzi yatakayoleta ujenzi wa jamii mpya. Mkangi ametumia sanaa kiuamilifu kuelezea matukio yaliyo katika jamii yake na jamii ambayo angalipenda wanajamii kuwa nayo.

Mafumbo anayotumia Mkangi yana lengo la kumzindua msomaji aibadili dunia yake iwe kielelezo cha haki na usawa. Wanyonge wanahimizwa kuwa hawapaswi kupumbazika na itikadi potoshi zinazoendelezwa na tabaka tawala katika jamii zao. Anawafahamisha kuwa, uwezo wanao wa kuyabadilisha maisha yao na kuunda jamii yenye usawa, haki na mapenzi. Mkangi anawazindua wasomaji kwamba haiwezekani jamii kufikia kiwango kizuri cha maisha iwapo wanajamii wataendelea kuiga mambo ya kigeni na kubaguana kwa misingi mbalimbali, vijana kuzembea na kulowela mijini badala ya kujihusisha na miradi ya maendeleo vijijini miongoni mwa mengine.

Aidha, katika sura hii tumechunguza namna ufumbaji umeendeleza au kukwamiza usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Walenisi*. Tumeonyesha kuwa mafumbo yalimsaidia Mkangi katika kuwapa wahusika wake majina ya kimajazi akidhamiria kuwasilisha maana nzito zaidi kuliko ilivyo maana ya majina yenyewe. Kwa upande mwingine, tumetambua kuwa wahusika wengi katika riwaya hii hasa katika jamii ya Dzombo hawakupewa nafasi kutenda bali walielezwa tu kimafumbo na hivyo kupoteza uhai wao. Vilevile katika mazungumzo yao hawajapewa lugha ya kimafumbo kama tulivyowaona katika riwaya ya *Mafuta.*

Katika sura ya tano, utafiti huu utatoa mahitimisho, matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo yanayohusiana na suala la utafiti.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, MATOKEO, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Muhtasari

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza mambo manne makuu. Kwanza, kubainisha aina na ubunifu wa ufumbaji katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi*. Pili, kuonyesha jinsi Mkangi alivyotumia mafumbo ili kumzindua msomaji wake. Tatu, kuonyesha jinsi ufumbaji umeendeleza au kukwamiza usawiri wa wahusika katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Nne, kutathmini namna mazingira ya mwandishi yalivyochangia ufumbaji katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi*. Yote haya yametazamwa kwa mtazamo wa Nadharia Amali ambayo husisitiza matokeo ya matumizi ya kitu fulani.

Utafiti huu una sura tano. Kuna sura ya kwanza ambapo usuli na suala la utafiti limefafanuliwa. Pia, malengo ya utafiti, nadharia tete, upeo na mipaka ya utafiti imeangaziwa. Hali kadhalika, sehemu hii imebainisha sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, msingi wa kinadharia, Mapitio ya maandishi na mbinu za utafiti.

Kisha, katika sura ya pili habari zinazomhusu mwandishi na mazingira yake zimechunguzwa. Kushughulikia maisha ya mwandishi na mazingira yake kulipelekea utafiti huu kubainisha mambo yaliyochangia matumizi ya ufumbaji kama kichocheo cha zinduko katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Aidha, kuchunguza mazingira yaliyomwathiri na kumsukuma kuandika riwaya hizi kumesaidia utafiti huu kuweka msingi bora wa kuelewa namna tajriba ya Mkangi ya maisha ilivyoathiri falsafa, itikadi, imani na mtazamo wake katika uandishi wa riwaya zake. Isitoshe, utafiti huu umeainisha mafumbo yapatikanayo katika mazingira ya Mkangi na katika tahakiki nyinginezo ambazo huenda alizitumia katika kuwasilisha tajriba zake.

Katika sura ya tatu na nne, kazi hii imefafanua aina ya mafumbo yaliyotumiwa na mwandishi kama kichocheo cha zinduko katika *Mafuta* na *Walenisi*. Imebainika kwamba taswira alizotumia Mkangi zimelenga kumzindua msomaji aone hali halisi ya maisha yake. Uchunguzi kuhusu namna ufumbaji huendeleza au kukwamiza usawiri wa wahusika, umeshughulikiwa pia. Vilevile katika sura ya tano, muhtasari, matokeo ya utafiti, mapendekezo na mahitimisho kuhusiana na utafiti yametolewa.

## 5.1 Matokeo

Kutokana na kazi hii ni dhahiri kuwa Mkangi alihiari kutumia ufumbaji ili uchukuane na mazingira ya wakati wake. Wakati ambapo Mkangi alikuwa akiandika riwaya hizi, uhuru wa kuikosoa serikali iliyokuwa mamlakani haukuwepo. Kazi zilizoonyesha uozo wa serikali na jamii waziwazi zilipigwa vita. Mkangi alilazimika kutekelaza haya kichinichini akitumia mafumbo, kuwazindua wanajamii kuhusu hali halisi iliyokuwepo nchini na wakati huo huo kuwatolea suluhu la kukabiliana na hali hizo kupitia mapinduzi, kwa minajili ya kuikwepa mitego ya makachero wa chama tawala cha wakati huo KANU. Aidha, watu waliomwathiri Mkangi walichangia katika matumizi ya mtindo wa ufumbaji kama vile Shabaan Robert ambaye pia alipendelea kuandika kimafumbo. Pia, tajriba ya Mkangi alipokuwa kizuizini ilichangia katika matumizi ya mafumbo kuhusu dhuluma zilizotendewa wafungwa wa kisiasa. Halikadhalika, kusomea kwake katika Chuo Kikuu cha Dar-es- salaam nchini Tanzania kulimwathiri kuhusu mafumbo yanayosawiri uzuri wa mfumo wa ujamaa.

Katika utafiti huu, imebainika kuwa, Mkangi alifumba kazi yake kupitia kwa taswira, jazanda na istiari. Pia, kazi hii imedhihirisha kuwa, mafumbo yaliyotumiwa na Mkangi katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* ni kichocheo cha zinduko kwa msomaji. Imetambulika kwamba, mwandishi ametumia mafumbo ya matope, wateule na wachochole, vidimbwi vya maji, uchi wa Matope, mbuni, na ukame ili kumzindua msomaji kuhusu athari mbaya inayoletwa na mfumo wa kiutawala wenye matabaka katika jamii. Kupitia kwa mafumbo haya, imebainika kwamba, licha ya Mkangi kumzindua msomaji kuhusu athari za utabaka, alilenga kuwahamasisha wasomaji kubadilisha hali hiyo kupitia kwa mapinduzi. Hii ndiyo sababu Mkangi akashadidia haya kwa kutumia fumbo la wanamapinduzi ili kuwazindua wanajamii kuhusu umuhimu wa muungano wa pamoja wa wanaodhulumiwa. Ukombozi na ujenzi wa jamii mpya huletwa kupitia kwa mapinduzi. Haya yatakuwa mapinduzi ya mfumo wa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mapinduzi haya yataleta usawa katika ugavi wa rasilimali za nchi, haki katika mahakama na usawa wa kijinsia miongoni mwa mengine.

Katika utafiti huu imetambulika kuwa, Mkangi alitumia fumbo la njuzi kuwazindua wasomaji kuwa viongozi wa tabaka la juu wanatumia uwongo ili kudumisha tabaka lao. Wanapogundua kuwa tabaka la chini limeanza kujua uwongo huu huwa wanaingiwa na wasiwasi sana. Mkangi alitumia fumbo hili ili kuwazindua wasomaji kuwa, ushindi wa haki na ukweli dhidi ya dhuluma na uongo utapatikana ikiwa wanyonge wote wataungana na kuwaambia wateule ukweli wa yale wanayoyafanya. Aidha, imebainika kuwa, Mkangi alitumia fumbo la nyoka

mkoko akilenga kuwazindua wasomaji kuhusu mgogoro uliopo kati ya wanyonge na wenye uwezo katika jamii.

Fumbo la mwenye mkunazi na mkunazi inaonyesha kuwa suluhu la ubepari ni mfumo wa ujamaa unaozingatia usawa katika jamii. Safari ya Ti nayo inamzindua msomaji kuhusu harakati ziletazo mabadiliko. Imedhihirika kwamba, kupitia kwa fumbo la safari ya Ti, Mkangi alilenga kuwazindua wasomaji kuwa, kupigania mabadiliko si kazi rahisi ni safari inayochukua muda na ina matatizo mengi.

Mafumbo ya mafuta na kitanda imelenga kufichua unafiki wa viongozi kwamba, wakati mwingine viongozi hutumia uongo ili kuwaweka mamlakani. Kulingana na Mkangi viongozi hawa wanapaswa kuondolewa ili kuunda serikali inayozingatia haki. Kutokana na mafumbo katika riwaya ya *Mafuta*, imefahamika kwamba, Mkangi alilenga kuwazindua wasomaji kuhusu hali zao halisi na wakati huo huo kuwatolea suluhu la matatizo yao.

Sura ya nne imefafanua mafumbo ya mwanamke, vijana, mapenzoni, mapacha, Dzombo, nzige na makapi, hirizi za viunoni, popo, majabali, trimi, sayari na kreshi, kidundu safari ya utu na uchawi, moto na mabavu. Kutokana na fumbo la mwanamke, imebainika kuwa, Mkangi alidhamiria kuwazindua wasomaji wake kuhusu umuhimu wa usawa wa kijinsia katika jamii. Aidha, anamzindua mwanamke kudai fursa katika nyadhifa za uongozi ili pawepo na idadi sawa ya wanaume na wanawake katika nafasi za kazi. Kulingana na ulipaji mahari, utafiti huu umetambua kuwa, bei hii ya mahari inamdunisha mwanamke. Mkangi anapitisha ujumbe wa uzindushi kwa mwanamke kwamba ndoa yenye misingi ya ulipaji wa mahari hukandamiza. Utafiti huu umesawiri picha ya mwanamke Mlenisi asiyeuzwa wala kununuliwa kwa mahari ili awe kielelezo cha mwanamke atakikanaye katika dunia ya leo.

Zaidi ya hayo, kupitia kwa mafumbo ya vijana, nzige na makapi, utafiti huu umedhihirisha kuwa, Mkangi anawazindua vijana kuwajibika kupitia kwa kutia bidii kazini ili waweze kuleta mabadiliko katika jamii kwa kuzalisha chakula cha kutosha na kuondoa umaskini katika jamii. Vijana wamemulikiwa umuhimu wa elimu na utafiti kupitia kwa mafanikio makubwa ya kilimo cha kufa na kupona katika ulimwengu wa Walenisi. Vijana Walenisi wanatumia teknolojia ya hali ya juu kupitia elimu na utafiti. Fumbo la vijana limebainisha kwamba Mkangi alilenga kuwazindua vijana wasomaji kuhusu umuhimu wa kilimo ambacho ni uti wa mgongo katika jamii yao na ni lazima waipe sekta hiyo stahiki yake. Aidha, anawatolea wito vijana kupanua kilimo badala ya kuzurura na kulowela mijini wakitafuta kazi zisizopatikana. Halikadhalika, katika utafiti huu kupitia fumbo la makapi na nzige

Mkangi alilenga kuwazindua watawala au viongozi kwa jumla kuwa vijana ni rasilmali muhimu katika maendeleo ya jamii wala sio wazushi wa shida katika jamii na kwa hivyo wanafaa kuthaminiwa na kuhusishwa katika shughuli za ujenzi wa jamii yao. Anawazindua vijana kuwa wao ni viongozi wa leo wala sio wa kesho jinsi ambavyo utawala usiowathamini husema.

Kutokana na kazi hii, imebainika kuwa, mafumbo ya mapacha na hirizi za viunoni yametumiwa na Mkangi kuwazindua wasomaji kuhusu athari zinazotokana na tofauti za kitabaka. Imefahamika kuwa, baadhi ya vifo vya maskini husababishwa na wengine kutokana na ukosefu wao wa utu. Mafumbo ya mapacha na hirizi za viunoni yametumiwa pia kutoa wito kwa madaktari  katika vituo vya afya kuwajibika ili kuokoa maisha ya wanajamii. Aidha, kupitia kwa fumbo la mapacha Mkangi anawazindua wasomaji kuwa magonjwa ambayo huwapata watu wa tabaka la maskini ni magonjwa ambayo hutokana na ukosefu wa lishe bora. Kupitia kwa fumbo la majabali, utafiti huu umetambua kuwa, Mkangi alilenga kuwazindua wasomaji kuhusiana na itikadi zilizopitwa na wakati, propaganda za watawala na migogoro baina ya wanamapinduzi. Mkangi kupitia kwa fumbo hili la majabali, anawafahamisha wasomaji kuwa ili kuleta mapinduzi katika jamii, wanamapinduzi lazima wawe na ujasiri wa hali ya juu. Halikadhalika, Mkangi kupitia kwa fumbo hili la majabali anawazindua wasomaji kuhusu umuhimu wa mapinduzi katika mfumo wa utawala unaowakandamiza wanajamii.

Imetambulika katika utafiti huu kuwa Mkangi alitumia mafumbo ya mapenzoni, trimi, sayari na kreshi kuwazindua wasomaji kuwa vifaa vya zao la utafiti vinafaa kutoa manufaa na starehe kwa kila mtu. Vifaa hivi vya utafiti vinafaa kurahisisha maisha kwa wote kwa sababu nchi ni yetu na uchumi ni wetu pia na hivyo, hatufai kuwa na umwinyi, ukabaila wala ubepari. Fumbo la kreshi lilitumiwa na Mkangi kuwazindua akina mama wasomi kutafuta njia bora za kuwalea watoto badala ya kuwaachia mayaya ambao hawana ujuzi wa kuwatunza watoto hao. Pia imebainika kuwa Mkangi alitumia mafumbo ya uchawi, moto na mabavu akilenga kuwazindua wasomaji kuhusiana na ujanja na hila wazitumiazo watawala ili kumiliki uchumi wa ulimwengu huu na kujisetiri uongozini. Watawaliwa huendelea kuishi kwenye umaskini na uhitaji kwa sababu ya kupumbazika na ujanja huu wa watawala. Hii ndiyo sababu Mkangi akashadidia haya kwa kutumia fumbo la udundu ili kuwazindua wasomaji na wanajamii kuwa matatizo wanayopitia maishani hutokana na ujinga wao unaotokana na kuamini ujanja wa watawala hawa.

Kupitia kwa mafumbo ya safari ya utu, popo na Dzombo, utafiti huu umetambua kwamba, Mkangi alilenga kumzindua msomaji kuhusu umuhimu wa utu na ubinadamu. Imebainika kwamba vitendo vya unyama kutoka kwa binadamu mmoja kwa mwingine husababisha kudhoofika kwa afya yake. Binadamu anapomilikiwa na ubinafsi huwa hajali maslahi ya binadamu wenzake bali hujali tu maslahi yake na hivyo hutumia wenzake kujinufaisha mwenyewe ilhali wao wakiendelea kusononeka maishani. Mkangi anamfahamisha msomaji kuwa zao la ukosefu wa utu katika jamii ni kuzuka kwa ubinafsi, ulafi na matabaka. Tabaka la matajiri huanza kumiliki nyenzo zote za kuzalisha mali na kuacha tabaka la maskini katika hali ya uhitaji na hivyo haki na usawa huwa haba katika jamii hiyo.

Jambo jingine linalodhihirika katika kazi hii ni kwamba, ufumbaji ulimsaidia Mkangi katika kuwasawiri wahusika wake katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi*. Kwanza, imebainika kuwa ufumbaji ulimsaidia Mkangi kuwasawiri wahusika wa kazi yake katika kuwapa majina ya kimajazi. Umajazi unajitokeza moja kwa moja katika *Mafuta* na *Walenisi*. Mkangi ametumia majina ya majazi na uhusika wa kimajazi kwenye riwaya hizi ili kukwepa mitego ya makachero wa chama tawala cha wakati huo KANU ambacho hakikuweza kuvumilia kukosolewa. Matumizi ya mbinu ya majazi katika riwaya hizi mbili inatuwezesha kuwafahamu wahusika hawa kwa urahisi.

Pili, lugha ya mafumbo waliyopewa wahusika inawasaidia kwa kiwango kikubwa kufikia wajibu waliopewa. Tumeona lugha ya kimafumbo kupitia kwa fasihi Simulizi imewasaidia wahusika kufaulu kuwasilisha ujumbe wao kwa njia ya mkato na yenye nguvu zaidi hasa kwenye *Mafuta*. Lugha hiyo ya kimafumbo kupitia fasihi Simulizi imetumika kiamali kupasha ujumbe wa mwandishi. Tatu, ufundi wa Mkangi katika kusawiri wahusika kimafumbo unajitokeza waziwazi hasa katika riwaya yake ya kwanza-*Mafuta*. Wahusika wa Mafuta wanajitokeza kama waliopewa majina na lugha wanayoimudu na wamefungamanishwa na mazingira barabara. Hili linawapa uhai, uhisifu, ukubalifu na uyakinifu. Kwa njia hiyo wanafaulu katika kuleta matokeo aliyokusudia mwandishi. Kwa upande mwingine, wahusika katika riwaya ya pili-Walenisi wahusika wamepewa majina kwa njia ya kimafumbo lakini kwa kiwango fulani hawajaonekana wakitumia lugha ya kimafumbo bali ni mwandishi anatumia lugha hiyo kuwaeleza. Kwa jinsi hiyo, hawajajitokeza kama wahusika ambao wamemudu lugha ya kimafumbo.

### 5.2 Mahitimisho

Utafiti huu umechunguza ufumbaji katika riwaya mbili za Katama Mkangi: *Mafuta* na *Walenisi* na mambo kadha yameweza kugunduliwa kuhusiana na utafiti huu. Kwanza, utafiti huu umebainisha kuwa, wakati ambapo Mkangi alikuwa akiandika riwaya hizi, uhuru wa kuikosoa serikali iliyokuwa mamlakani haukuwepo na kwa hivyo, alilazimika kutumia ufumbaji kuwasilisha ujumbe wake ili kuhepa rungu ya serikali. Pili, alikosomea na waandishi wengine, walimwathiri katika matumizi ya mbinu ya ufumbaji katika uandishi wake. Tatu, kutokana na kazi hii, ni dhahiri kuwa Mkangi alitumia mbinu ya ufumbaji kumzindua msomaji kuhusu athari za utabaka, ubepari, unafiki wa viongozi, sheria na nafasi yake katika jamii, umuhimu wa utu na usawa, umuhimu wa mapinduzi katika ujenzi wa jamii mpya, elimu na utafiti, mchango wa vijana katika ujenzi wa taifa miongoni mwa mengine. Aidha, imebainika kuwa Mkangi alitumia taswira, jazanda na istiari katika kufumba ujumbe wake. Hali kadhalika, imedhihirika kuwa ufumbaji ulimsaidia Mkangi katika usawiri wa wahusika wake kwa kuwapa majina ya majazi na lugha ya kimafumbo.

### 5.3 Mapendekezo

Suala kuhusu ufumbaji katika kazi za sanaa na hasa riwaya ya Kiswahili halijafanyiwa utafiti mwingi hata ingawa vipengele vingine vya lugha vimeshughulikiwa sana na watafiti mbalimbali. Kwa hivyo bado kuna mambo mengi ya kushughulikiwa kuhusiana na ufumbaji kwa kujaribia nadharia za fasihi zilizopo na hata zile za kiisimu. Utafiti huu wetu umeangalia kipengele kimoja tu kwa kutumia Nadharia Amali huku tukiegemea zaidi mtazamo wa hii nadharia kifasihi. Inavyoonekana kuna haja ya kutumia mtazamo wa kiisimu wa nadharia hii hii na kuchunguza lugha ya ufumbaji ili kuona jinsi gani Mkangi alivyotumia lugha hii ya ufumbaji kuwasilisha ujumbe wake kwa undani zaidi. Aidha, tunapendekeza kuwa utafiti zaidi unaweza kufanywa ili kuchunguza maudhui ambayo Mkangi alikusudia kuwasilisha kupitia kwa ufumbaji. Utafiti kuhusu mbinu zingine alizotumia Mkangi akilenga kuwazindua wasomaji wake unaweza kufanywa pia. Halikadhalika, tunapendekeza kuwa utafiti ufanywe ili kuona ni jinsi gani ufumbaji wa ujumbe hutatiza uelewaji wa ujumbe na wasomaji wa kazi zinazoandikwa kimafumbo.

## MAREJELEO


Abrams, M. H. (1981). *A glossary of Literary Terms* (5th Edition). New York: Rinehart and Winston, Inc.

Ameir, I. H. (1983). *Misingi ya Nadharia ya Uhakiki*. Dar-es-Salaam: TUKI.

Chacha, L. M. (2003). *Mwongozo wa Walenisi*. Nairobi: Africawide Network.

Chacha, N. C. (1986). *Marejeo.* Nairobi: East African Educational Publishers

——————— (1987). *Wingu Jeusi*. Nairobi: East African Educational Publishers

Coombes, H. (1953). *Literature and Criticism*. Australia: Chatto and Windus.

Crystal, D. (1987). *The Cambridge Encyclopaedia of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Dhahabu, L.G. (1994). *Uumbaji na Uendelezaji wa Wahusika Katika Tamthilia za Penina Muhando.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).

Doubtfire, D. (1978). *The Craft of Novel-Writing*. London: Allison and Busby.

Fowler, R. (1975). *Style and Structure in Literature*. Basil Blackwell: Oxford University Press.

Guerin, W. (1979. *A Handbook of Critical Approaches to Literature*. New York: Harper and Row Publishers.

Hawthorn, J. (1985). *Studying the Novel*: *An Introduction*. London: Edward Arnold Ltd.

Holman, C. H. (1936). *A Handbook to Literature*. New York: The Odyssey Press Inc.

Hussein, E. (1969). *Kinjeketile*. Nairobi: East Africa Educational Publishers

_________ (1971). *Mashetani*. Nairobi: East Africa Educational Publishers

Jefferson, A. na Robey, D. (1982). *Editors of Modern Literature Theory*. New Jersey: Barnes and Books.

Karanja, P. (1990). *Taswira ya Mwafrika Katika Vita vya Ukombozi Dhidi ya Ukoloni Afrika Mashariki Katika Tamthilia za Kikombozi.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

Kisurulia, j. (2000). Usawiri wa Wahusika Katika Riwaya za Katama Mkangi. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Egerton(Isiyochapishwa).

Khamadi, S. I. O. (1991). *Using the Library and Writing Research Proposals Reports And Papers*. Egerton: Egerton University press.

Kristeva, J. (1984). *Revolution in Poetic Language*. New York: Columbia University press.

Kemoli, J. N. na King'ei K. J. (2001). *Ufundishaji wa Ushairi wa Kiswahili*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Leech, G. N. (1983). *Principle of Pragmatics*. London: Longman Group University Press.

Levinson, S. C. (1983). *Pragmatics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Malenya, M. (2008). *Matumizi ya Lugha ya Jazanda katika Nyimbo za Jacob Luseno*. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

Massamba, D. P. B. na Mlacha, S. A. K. (1987). Vitabu vya Kutafsiriwa na Fasihi ya Kiswahili. *Kiswahili Juzuu* 54/1 na 54/2. Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Mazingwa, S. A. I (1991*). Fasihi ya Kiswahili.* Permilo: Benedictine Publications Ndanda.

Mazrui, A. na Syambo, B. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Heinemann.

Miriji, T. (1991). *Mtindo katika Pungwa ni Hatua katika Kuwasilisha Ujumbe*. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa)

Mkangi, K. G. C. (1984). *Mafuta*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

_____________(1995*). Walenisi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.

Momanyi, J. (1991). *Matumizi ya Taswira Kama Kielelezo cha Uhalisi Katika Utenzi wa*

*Al-Inkishafi*. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa)

Msokile, N. (1993*). Msingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mule, P.K. (1991). *Swala la Mwanamke Katika Tamthilia ya Kiswahili.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta(Isiyochapishwa).

Mulokozi, M. (1979). *Mukwawa wa Uhehe*. Nairobi. East African Educational Publishers.

Musembi, N. N. (2005). *Matumizi ya Taswira na Ukinzano katika Riwaya za Mkangi*. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

Mwenda, N. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College

Mwangi, T. (2005). *Fani na Mtindo Katika Tamthilia za Kiswahili.* Tasnifu ya M.A, Chuo Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).

Ngara, J. (1985). *Vipengele vya Fasihi.* Nairobi: East African Education Publishers

Ngugi, T. na Mugo, G. M. (1974). *Mzalendo Kimath*i. Nairobi: East African Educational Publishers.

Nyanchama, Z. (2004). *Matumizi ya Taswira na Ishara Katika Sauti ya Dhiki Diwani ya Abdilatif Abdalla*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Okwena, S. (2013). *Matumizi ya Jazanda katika Tamthilia Tatu za Arege.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

Peck, J. (1983*). How to Study a Novel*: *students' guide*. London: The Macmillan Press Ltd.

Peck, J. na Coyle, M. (1984*). Literature Terms and Criticism*. London: Macmillan Education Ltd.

Peter, C. B. (1994*).* *A Guide to Academic Writing*. Eldoret: Zapf Chancery Publishers.

Ramkin, D. (1972). *Style and Structure*. Harcourt Brace: Jovanovich Inc.

Short, M. (1988). *Reading, Analyzing and Teaching Literature.* London: Longman.

TUKI. (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar-es-Salaam: TUKI.

TUKI. (2002). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar-es-Salaam: TUKI.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar-es-Salaam: TUKI.

TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar-es-Salaam: TUKI.

Taylor, R. (1981). *Understanding the Elements of Literature*. London: Macmillan.

Vunyoli, A. J. (2004). *Hadithi kama Chombo cha Maudhui katika Riwaya za Mkangi.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

Wafula, R. (1989). *The Use of Allegory in Shabaan Robert's Prose Works*. Tasnifu ya M. A, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).

Wafula, J. (1990). *Mawazo na Mbinu za Uwasilishaji katika Marejeo*. Tasnifu ya M.A, chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

Wamitila, K. W. (1998). Towards Unlocking Katama Mkangi's Walenisi. A case Study of Parabolic Narrative katika *Kiswahili Juzuu 61, 1999*. Dar- es- salaam: TUKI.

Wamitila , K. W. (2000). *Towards Understanding Kiswahili Proverbs*: *An Examination of Schemes, Figurate Tropes and Contextual Issues*. Burlington: The University of Vermount.

_________ (2004). *Kichocheo cha Fasihi*: *Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wangari, M. R. (2011). *Mbinu za Mawasiliano Katika Matangazo ya Runinga Nchini Kenya.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).

Wellek, R. and Warren, A. (1993). *Theory of Literature*. New York: Harcourt, Brace and World Ltd.